يَوْمَ تُبَدَّلُ الْاَرْضُ غَيْرَ الْاَرْضِ وَ السَّمٰوٰتُ

# Nidhamu Mpya

Na

Hadhrat Mirza Bashir ud Din Mahmood Ahmad[ra]
Khalifatul Masihi II

# Nidhamu Mpya

Nizaam-e-Nau (Swahili Translation)

Tafsiri ya Kiswahili ya: Nidham-e-Nau (Kiurdu)

**Mwandishi:**
Hadhrat Mirza Bashir ud Din Mahmood Ahmad[ra]
Khalifatul Masihi II

**Mfasiri:**
Waseem Ahmad Khan

Chapa ya Kwanza (Kiurdu): 1943
Chapa ya Kwanza (Kiswahili): 2020

© Islam International Publications Ltd.

**Kwa Maelezo Zaidi:**

**Tanzania:**
Jumuiya ya Waislamu Waahmadiyya, Tanzania
Mtaa wa Bibi Titi Mohamed S.L.P. 376, Dar es Salaam.
Simu: +255222110473 Fax: +255222121744

**Kenya:**
E.A. Ahmadiyya Muslim Mission
P.O. Box 40554 Nairobi Kenya Simu: +254222111031

Kimechapwa na Ahmadiyya Printing Press
Dar es Salaam, Tanzania / Nairobi, Kenya

ISBN: 978-1-84880-523-1
10 9 8 7 6 5 4 3 2 1

## MAELEZO YA MWENEZI

Hii ni tafsiri ya hotuba ya Hadhrat Khalifatul Masihi wa Pili r.a. aliyotoa mkutanoni mwa mwaka 1942 huko Qadian. Hotuba hii ilitolewa kwa sura ya kitabu mara ya kwanza mnamo mwaka 1943.

Hotuba hii ilieleza kinaganaga itikadi za Ukomonisti na Ubepari, zilivyoenea katika zama hizo. Khalifa Mtukufu[ra] alifafanua vya kutosha manufaa na madhara ya Ujamaa, Ujamaa wa Kimataifa, Umaksi, Ubolsheviki, Unazi na Ufashisti. Akahakikisha kwa hoja imara kuwa mifumo hiyo haiwezi kuleta nidhamu mpya ya kufaa kwa dunia nzima, bali Nidhamu Mpya inayoweza kuwatolea maskini na matajiri haki zao barabara ndiyo ile iliyoletwa na Islam na imetangazwa na mwanzilishi wa Jumuiya Ahmadiyya tangu mwaka 1905.

Mkisoma kitabu hiki kizima kwa makini, mtaweza kutambua uzuri wa Nidhamu Mpya hii kwa marefu na mapana.

Sheikh Wasim Ahmad aliifasiri kwa Kiswahili. Na Sheikh Muzaffar Ahmad Durrani akaidurusu, na kabla haijapelekwa mtamboni kuchapwa, niliisoma tafsiri hii kikamilifu kwa makini na kuilinganisha na matini ya Kiurdu.

Sheikh Ansar Hussain akashughulikia kazi muhimu ya *fometi* yake kwa bidii sana. Nawashukuru wote walioishughulikia kwa njia hii au ile mpaka tafsiri hii iliweza kufika mikononi mwa wasomaji wa Kiswahili ili wapate kunufaika na elimu hii kubwa. Mwenyezi Mungu Awapatie wote hao malipo bora hapa na huko Akhera.

Jamil R. Rafiq
Wakilut Tasnif, Tahrike Jadid
Rabwah, Pakistan 17.02.2020

بِسۡمِ اللّٰہِ الرَّحۡمٰنِ الرَّحِیۡمِ[1]                نَحۡمَدُہٗ وَنُصَلِّیۡ عَلٰی رَسُوۡلِہِ الۡکَرِیۡمِ[2]

# MUUNDO WA NIDHAMU MPYA

Hotuba ya Hadhrat Mirza Bashirud-Din Mahmud Ahmad[ra], Imamu Wa Jumuiya Ya Waislamu Waahmadiyya Aliyotoa katika mkutano wa Mwaka Tarhe 27 Desemba 1942

Baada ya kusoma Tashah-hud, ta'awwudh na sura Faatiha, Hudhur[ra] alisema:

## Umuhimu wa Madhumuni

Mada yangu ya leo ndiyo ambayo nilishatoa ahadi yake katika hotuba moja ya Ijumaa iliyopita (iliyokwisha chapishwa ndani ya gazeti la Al Fazl la tarehe 10 Desemba 1942). Nilisema kwamba, nitawaeleza wanajumuiya Ijumaa ijayo, kipengele kipya na cha muhimu cha Tahrike Jadid. Lakini Ijumaa ilipofika, nia yangu ikabadilika na ni kutokana na umuhimu wa mada hii, kwamba nikaonelea badala ya Ijumaa afadhali niieleze kwenye mkutano wa mwaka ambapo ndugu wengi watajumuika. Kwa hiyo niliahirisha kuielezea mada hii wakati ule, na kutangaza katika hotuba yangu iliyofuata (ambayo imekwisha chapishwa katika gazeti la Alfazl la 16 Desemba 1942), kwamba kwa sasa hivi ninaahirisha kueleza madhumuni hayo, na badala yake

[1] Kwa jina la Mwenyezi Mungu, Mwingiwa Rehema na Ukarimu.
[2] Twamhimidi Yeye na kumsalia Mtume Wake mhashamu.

naielekeza jumuiya kwenye mambo mengine. Baadaye rai yangu tena ikabadilika na nikapenda kuiahirisha zaidi mada hiyo, na badala yake nieleze baadhi ya sehemu nyingine za *Saire Ruhani* "Safari ya Kiroho". Lakini kwa kuwa mpango wa Mungu ulikuwa kwamba madhumuni haya yatangazwe duniani haraka iwezekanavyo, kwa hiyo ilitokea tu kwa bahati ya kuwa nikaugua mfululizo kwa muda mrefu hata, kwamba sikuweza kupata nafasi ya kutafuta marejeo kwa ajili ya madhumuni ya "Safari ya Kiroho". Hatimaye nikafikiri ya kwamba kuanzia tarehe 20, nitaanza kutoa nafasi kwa shabaha hii, lakini katika siku hizo nililazimika kufanya kazi nyingi za kuandika maelezo ya Kurani. Nimekwisha eleza ya kwamba siku hizi ninaandikisha maelezo ya Kurani. Hivyo basi siku zile, kwanza nilikuwa naandikisha maelezo ya Kurani kisha nikadurusu yale maelezo yaliyokwisha andikwa kwa maandishi safi, na kazi hiyo ikachukua muda mwingi sana. Tena siku hizi nimekwishaanza kuzisoma mwenyewe barua, na kazi hii pia ni kubwa sana. (Hapa ningependa kubainisha ya kwamba hapo kabla, kutokana na kazi ya maelezo ya Kurani, nilikuwa sisomi barua mwenyewe, bali watu wa ofisini walikuwa wakinileta muhtasari wa madhumuni ya barua hizo. Lakini tangu miezi minne au mitano iliyopita nasoma mwenyewe barua zote na kuandika majibu ya barua muhimu pembeni mwa hizo, na barua zingine ambazo majibu yao ninakuwa nimeishawaeleza

watu wa ofisini, wao wenyewe wanazijibu. Kwa vyovyote kazi ya kuzisoma barua na kuzijibu pia inaendelea ambayo ni kazi kubwa sana. Kwa hiyo, sikuweza kupata muda wa kuandika muhtasari na kutafuta marejeo kwa ajili ya hotuba ya mkutano wa mwaka. Ilipofika tarehe ishirini, nilisema moyoni ya kwamba sasa kuanzia kesho nitaifanya kazi hiyo. Barua chache pia zilibaki kusomwa, na wasimamizi wa Tahrike Jadid nao waliniambia kwamba ahadi za Tahrike Jadid za ndugu bado hazijaletwa kwetu, basi tuletewe hizo barua za ahadi zao ili ziandikwe. Basi nikaanza kuzipitia barua hizo. Muda huo huo nikashikwa na baridi kali kiasi hiki ya kwamba nikaanza kutetemeka na meno kutatarika kutokana na ukali wa baridi. Wakati huo nikahisi niende haja ndogo na nikataka kusema kwamba wekeni birika la maji lakini kutokana na hali yangu isiyo nzuri sikuweza kutamka hayo kwa dakika nzima. Kisha niijilaza kitandani na kujifunika na mfarishi na kujiwekea ndani mipira miwii ya majimoto, lakini baridi haikupungua. Asubuhi nilipopima halijoto kwa kipimajoto, ilikuwa tisini na tisa na nusu. Saa za mchana hadi Alasiri ilikuwa nafuu, lakini wakati wa alasiri nilianza tena kujisikia vibaya. Wakati huo nikapima tena halijoto kwa thamometa na nikajua kwamba kuna homa kidogo na joto ni kuanzia nyuzi 100 au 100.5, usiku joto likazidi mpaka nyuzi 103. Kutokana na hali hiyo, sikuweza kuandaa mambo ya muhimu kwa ajili ya

hotuba yenye madhumuni ya “Safari ya Kiroho”. Hatimaye nikaelewa ya kwamba matakwa ya Mwenyezi Mungu ndiyo kuwa nieleze kwanza madhumuni yahusuyo Tahrike Jadid. Kwa hiyo baada ya kutayarisha kwa muhtasari mambo kuhusu madhumuni haya, nikaelewa kwamba muda umeishawadia tayari kwamba ujumbe huu adhimu uelezwe mbele ya dunia.

## Umuhimu wa Tahrike Jadid kwa Ujumla

Madhumuni niliyotaka kuyaeleza yalikuwa ni haya kwamba sifa za Tahrike Jadid zimeelezwa mara nyingi kwa watu kwa kupitia tu na zikiwa sehemu moja moja. Lakini umuhimu wa Tahrike Jadid kwa ujumla haujawahi kuelezwa kwa Jumuiya. Au tuseme hivi kuwa hata mimi mwenyewe nimeuelewa polepole uhakika wake. Mambo yote niliyoyaeleza katika hotuba yangu ya kwanza kuhusu Tahrike Jadid, yote hayo nilitiliwa moyoni mwangu na Mwenyezi Mungu, nami nikaendelea kuyabainisha jinsi Mwenyezi Mungu Alivyoendelea kunifahamisha. Hivyo, ukweli ndio huu kwamba mwanzoni hata mimi mwenyewe sikuzifahamu shabaha kadhaa za Tahrike Jadid, wala faida na hekima zake nyingi hazikunidhihirikia. Ndiyo sababu umuhimu wa Tahrike Jadid kwa ujumla haujabainishwa kwa Jumuiya. Au inawezekana Mungu alikusudi kwamba madhumuni haya yaelezwe pindi yatakapohitajika. Kwa vyovyote vile mwendeleo huu una athari yake kimataifa

pia na ni muhimu uelezwe kwa mapana na marefu, kwani madhumuni haya hayajawahi kuelezwa.

## Muhtasari wa Madhumuni

Muhtasari wa mada nitakayoieleza sasa hivi ni huu kwamba Tahrike Jadid iliyoanzishwa nami, au tuseme kwa maneno yaliyo sahihi kuwa Tahrike Jadid iliyoanzishwa nami kwa takwa la Allah, ndani yake mbegu imepandwa ya kutimiza kusudio adhimu la Kiislamu na kuimarisha mizizi ya ubinadamu. Sasa nawaelekeza wanajumuiya kwenye jambo hili kwamba baada ya sentensi hii madhumuni yatakayofuata, kidhahiri yataonekana ni tofauti, na itaonekana kana kwamba nimeiacha madhumuni husika ya Tahrike Jadid. Lakini nawahakikishia wanajumuiya kwamba kama watavuta subira na kusikiliza kwa makini, madhumuni yote haya yataonekana kulingana na Tahrike Jadid, niliyoitaja hapo kabla.

## Mazingira ya Tahrike Jadid

Vitu vyote vinavyoonekana duniani vinapendeza katika mazingira yao; kama kitu fulani kitolewe nje ya mazingira yake, uzuri wake wote hupotea. Hivyo basi, ndugu hawawezi kuujua uhakika wa mpango huu mpaka nieleze mazingira yake. Kubainisha mazingira haya ni muhimu, hususan kwa sababu hii pia kwamba wanajumuiyya wetu wengi ni wakulima ambao, kwa

kawaida, huwa hawajui mambo ya kielimu. Kwa hiyo ni muhimu kwamba nieleze kwanza hali halisi ya dunia iliyotulazimisha kufikia hatua hii, na niseme ya kwamba kuna mabadiliko gani wakati huu yanayotokea duniani, na mabadiliko hayo yataathiri vipi katika mustakabali, na ni nini athari zake kwa Jumuiya yetu na jumuiya zingine. Ikiwa athari hizi ni baya, basi tunawezaje kujiepusha nazo; na kama ni nzuri, yafaa tuzikubali kiasi gani.

## Tofauti Baina ya Matajiri na Maskini wa Zama Hizi na Matokeo yake

Kwanza kabisa ningependa kueleza ya kwamba tofauti inayoonekana duniani baina ya mwenye hali ndogo na hali nzuri, asiye na bahati na mwenye bahati njema, maskini na mkwasi imesababisha kuzuka mabadaliko ya aina mbili. Badiliko la kwanza linalotokea ni hili kwamba tofauti hiyo inaendelea kujitokeza zaidi. Na badiliko la pili linalozalika ni kwamba hisia zihusuzo tofauti hiyo zinaendelea kupata nguvu zaidi duniani. Hata zamani pia matajiri walipatikana, lakini kuna tofauti kubwa sana baina ya matajiri wa zamani na wa siku hizi. Matajiri wa zamani, ambao baadhi ya vizazi vyao bado wanaishi mpaka leo katika maeneo ya milimani, hali yao ilikuwa kwamba walikuwa wakipata kwa wingi fedha, nafaka na mazao mengine, nao pia walikuwa wakivigawa kwa watu kwa wingi. Safari moja tajiri mmoja wa jimbo la Panjab aliugua mjini Lahore.

Nami pia, kwa bahati, nilifika Lahore kwa kazi fualni. Hapo nikajua kuwa pengine watu mia tatu au mia nne wa eneo lake wanakuja kumtembelea katika wakati mmoja. Na hao wanaokuja baadhi yao wanamletea kondoo, mwingine mchele, mwingine sukariguru na vitu vingine, kwa sababu tu kwamba Mheshimiwa ni mgonjwa na haifai kumtembelea mikono mitupu. Na yule mheshimiwa pia alikuwa na wapishi kumi au kumi na watano hivi. Wanyama waletwapo, yeye akawachinjisha na kupikisha ndani madegi na kuwalisha watu. Hivyo, kwa sababu ya ugonjwa wake, mjumuiko mkubwa wa watu uliendelea kuwepo kwa miezi miwili, mitatu, naye akaendelea kuwalisha mfululizo mamia ya watu.

## Hali ya Matajiri wa Zama Hizi na Watumishi wao Kulinganishwa na Zama Zilizopita

Basi, bila shaka, zamani pia walikuwepo matajiri, lakini mali yao ilikuwa ikigawiwa kwa njia isiyowachukiza watu. Halafu, katika zama zile, maana ya mtumishi ilikuwa tofauti na mtumishi wa leo. Katika zama zile, mtumishi alifahamiwa kuwa ni sehemu ya familia. Hakuna shaka yoyote kwamba hata wakati ule baadhi ya tofauti zilikuwepo, kama vile hawakupenda kumwoa mtumishi wa kike au binti yako kuolewa na mtumishi. Hata hivyo walikuwa wanaishi pamoja hivi kwamba kama tajiri aliketi juu ya zulia, na mtumishi wake pia alikaa pamoja naye au kama mama akikaa basi mjakazi

wake pia amekaa naye. Lakini leo inakuwa hivi kwamba tajiri ameketi kitini na mtumishi wake amesimama mbele yake akikunja mikono yake, hata kama akichoka hathubutu kuketi mbele ya tajiri wake. Vivyo hivyo angalieni vyombo vya usafiri ambavyo hapo awali kulikuwa hakuna tofauti kubwa sana. Iliwezekana kwamba farasi wa mmoja ni ghali na wa mwingine ni wa bei rahisi. Lakini siku hizi tofauti iliyopo baina ya daraja ya tatu kulinganishwa na daraja ya kwanza na ya pili ni kubwa mno. Halikadhalika kunaonekana tofauti kubwa sana kati ya ujenzi wa nyumba za matajiri na za maskini. Kuna aina nyingi za samani ambazo maskini hawezi kuzinunua. Matajiri walipoendelea kutandika zulia, maskini nao walitandika zulia la bei rahisi au kitambaa; lakini sasa kuna aina nyingi sana za samani ambazo maskini hawezi kabisa kuzinunua hata samani ya bei ndogo. Mwanzoni, kama matajiri walitengeneza busati, Wakashmiri (waliokuwa mafundi wa mikeka), walitengeneza mikeka. Lakini sasa kuwaiga matajiri katika kununua makochi, viti au meza na kadhalika, ni nje kabisa ya uwezo wa maskini. Ilmuradi tofauti hii baina ya wakubwa na wadogo imezidi kiasi hiki ya kwamba inaumiza.

## Msimamo Mpya na Matokeo yake Kulinganishwa na Nadharia ya Zamani Ihusuyo Utajiri na Umaskini

Kisha, kuna tofauti nyingine pia vilevile kwamba sasa hisia nazo pia zimekuwa kali zaidi. Katika zama za

awali, kwa kawaida, ilifikiriwa kuwa mali yote ni ya Allah. Kama kuna yeyote mwenye njaa, ni Mwenyezi Mungu Aliyemweka katika hali hii, na kama mtu anapata riziki, ni kwa sababu Mwenyezi Mungu Anamruzuku. Lakini sasa, kutokana na kuenea kwa elimu na falsafa, inafikiriwa kwamba kama maskini wanasumbuka na njaa basi sio kuwa Mungu amemweka katika hali hii, bali ni matajiri ndio waliowanyang'anya mali yao. Na kama matajiri wapo katika raha, basi si kwa sababu Mwenyezi Mungu Amewajaalia hali hiyo, bali ni kwa sababu hao wamewapora maskini mali yao. Hivyo, basi, siku hizi mtazamo umebadilika na kutokana na mabadaliko haya ya mtazamo, hisia za watu zimekua kali na matokeo yake ni hasira kuchemka sana. Mtu wa zamani alikuwa na subira, na kama alikuwa anampenda Mwenyezi Mungu, basi akishikwa na njaa alimshukuru kwa kusema 'subhanallah', na akila pilau kasema 'subhanallah! Kwani alikuwa anafahamu kuwa hayo yote ndiyo kutoka kwa Allah. Na kama mtu alikuwa hana na imani, yeye naye alifikiri kuwa siwezi kumwendea Mungu, basi afadhali nikae kimya. Lakini leo, lawama zote zilizokuwa zinamwangukia Allah, zinawaangukia watu na inasemwa kwamba matajiri na wenye nguvu wanataka kuwapiga na kuwakaba maskini. Basi, kutokana na kubadilika kwa mtazamo, hisia zimekuwa kali sana.

## Ubunifu wa Mashine Wasababisha Tofauti Kuzidi Baina ya Utajiri na Umaskini

Ingawaje tofauti hii imekuwa ikipatikana tangu kale, na kama ichunguzwe vizuri inaweza ikafika hadi zama zilizo karibu na Hadhrat Adam[as], lakini kidhahiri ilidhaniwa kuwa kadiri utamduni utakavyoendelea kukua, basi tofauti hiyo itazidi kufutika. Kwa hiyo mwanzoni, mashine zilipotengenezwa, watu walifanya uasi mwingi mkubwa sana. Matajiri walisema kwamba kwa njia hii hali ya maskini itaboreka na watu wengi watapata ajira. Na maskini nao wakasema kuwa mtambo mmoja utafanya kazi ya watu kumi na hivyo wafanyakazi watakosa ajira. Sasa matukio yamekwisha thibitisha ya kwamba watu wengi wamepata ajira au hawakupata, lakini ubunifu wa mashine umeongeza sana tofauti baina ya matajiri na maskini.

## Jitihada za Kuboresha Hali ya Maskini na Sababu ya Kushindwa katika hizo

Hakuna shaka kwamba baadhi ya marekebisho pia yalifanyika. Mwanafalsafa fulani mwenye moyo mzuri alijitokeza na kuleta mpango wa ustawi wa maskini; au mfalme fulani au mfanyabiashara mwema akainuka na kufanya marekebisho katika idara fulani ya serikali au katika viwanda, lakini marekebisho ya dunia ambayo amani ya watu wote iliyategemea, hayakufanywa kwa ujumla, na taabu za umma zikabaki kama zilivyokuwa.

Hata hivi leo, inashuhudiwa mara nyingi kwamba mbwa wa tajiri wanalishwa makombo ya kaki za mezani kwake, ilhali watoto wa maskini wanalala na njaa wakiililia chapati kavu. Siyo kupiga chuku, ni hakika kuwa wapo maelfu, bali malaki ya wazazi wanaowalalisha watoto wao kila siku na njaa. Matajiri hawawezi kuwasaidia hata kama wapende kufanya hivyo. Kwani, tajiri atajuaje kuwa katika bonde la mlima Himalaya, ndani ya kibanda kuna mtoto wa mama maskini, anayekaribia kufa kwa njaa. Matajiri wa Delhi na Lahore wataelewaje hali na matatizo wanayokabiliana nayo maskini waishio sehemu za mbali duniani? Kwanza hawapati hamu ya kuwasaidia maskini, na kama wakipata hamu, wanakosa miundombinu, ambayo kwayo wanaweza kutatua matatizo ya maskini wa dunia nzima, kwani hawajui kuwa maskini wako wapi na wapi na sehemu gani na wanazo haja gani?

## Hali Mbaya Isiyoweza Kuvumilika ya Maskini Ikilinganishwa na Ile ya Matajiri

Matajiri wanapougua, pengine daktari akiwaambia dawa za Rupia hamsini anaondoka, na hali yao ni kuwa huzinunua dawa hizo vichapa sita-saba na kufungua kimoja kati ya hivyo na kuonja, kisha wanasema dawa hizi hazifai, basi mwiteni daktari mwingine. Daktari mwingine anakuja na kuandika dawa zingine za *Patent* za Rupia 30-40 na kuondoka. Ilmuradi, wantumia Rupia 200-400 juu ya maradhi madogo madogo kama mafua na kikohozi. Kinyume na hayo, mtoto wa mama

maskini akiugua kichomi, tabibu anamwambia *'Arke Mkoo'* au *Joshanda* la *Lasura*.' — dawa za mitishamba — Yeye mama huyo anapita-pita mtaa mzima akiomba *paisa* nusu ili aweze kumtengenezea dawa hiyo *Joshanda*, lakini hakuna mtu ampataye hata *paisa* nusu. Kwa vyovyote vile jinsi yalivyo ya mama maskini ndivyo yalivyo ya mama tajiri. Lakini huko hali inakuwa kwamba mtoto akipiga tu chafya, madaktari huanza kuja mmoja bada ya mwingine, mtoto huanza kupewa dawa mbalimbali, mayaya hukaripiwa kwamba hawakumfunika vizuri ndiyo maama amepata baridi; lakini mama mwingine huhangaika nyumba hadi nyumba bila kupata *paisa* nusu mpaka mtoto wake anakufa kwa taabu. Ziangalieni nyumba zenu pembezoni mwenu, ulizeni katika mitaa yenu, mtapata siyo mamia bali maelfu ya mifano ya namna hiyo. Umaskini wakati mwingine unakuwa umezidi kiasi cha kushindwa kuvumilika.

## Hali Iumizayo ya Maskini na Mandhari yake Yatishayo

Safari moja mama mmoja maskini alinijia, na kabla hajaeleza haja yake akatoa maelezo marefu na akajinyenyekeza sana na kusema mara kwa mara kwamba nimekujia na matumaini makubwa sana. Nami kadri nilivyomwambia, 'mama ueleze tu shida yako, nikiweza nitakusaidia, ndivyo alivyozidi kujinyenyekeza na kunisifu-sifu sana. Nilifikiri pengine kuna harusi ya

mwanaye au bintiye na kwa hiyo anahitaji Rupia thelathini au arobaini, lakini niliposisitiza sana na kumwambia aeleze shida yake akasema anahitaji *Anna* nane (thumuni) kutimizia haja yake fulani. Bado sijasahau athari ya tukio hili mpaka leo jinsi alivyoeleza maneno mengi kabla ya kueleza haja yake na kunyenyekea na kunisifusifu mno, na tena haja yake ilikuwa ndogo sana ya kupewa *Anna* nane. Jambo hili linaeleza wazi ya kwamba kwake mama huyo jambo moja kati ya mambo mawili lilikuwa ni la yakini. Ama alikuwa anafikiri kuwa mwenye fedha mfukoni hana moyo wa kumsaidia maskini hata *Anna* nane, au kutokana na umaskini wake, alikuwa akifahamu kwamba mtu mwenye bahati nzuri aliye na *Anna* nane anaweza kupatikana duniani kwa nadra. Kila nadharia kati ya hizo mbili ni ya hatari na ya kutisha. Ikiwa hisia hii ya mama huyo iwemo pia ndani ya nyoyo za maskini kwamba hata kama tukipatwa na shida namna gani, hakuna yeyote atakayejitokeza kutupatia hata *Anna* nane, basi inadi na budhudha nyingi hata namna gani zikizalika mioyoni mwao dhidi ya matajiri, bado ni kidogo tu. Na kama maskini wawe wamefikia hali duni kiasi hiki kwamba kwa kuwaona wengine wakila chakula kizuri na kuvaa mavazi mazuri, bado wanafikiria kuwa watu hawana hata *Anna* nane, na kama yupo mtu mwenye *Anna* nane, basi huyo ndiye mwenye bahati

njema sana, basi fikra hii ni ya hatari kiasi gani kuhusu kurudi nyuma kwa dunia!

## UANZISHWAJI WA MIPANGO MBALI MBALI KWA KUSTAWISHA HALI YA MASKINI

### Demokrasia

Hali hii inaendelea tangu muda mrefu na kama nilivyoeleza, watu walijaribu kuiboresha pia lakini mpaka sasa hakuna mabadiliko yaliyotokea. Tangu mwishoni mwa karne ya kumi na nane, hali hiyo ilianza kupata kuenea zaidi kielimu, na sura ya kwanza ambayo hisia hizi za mwamko zilichukua ilipewa jina la demokrasia. Yaani iliamuliwa kwamba watu hawawezi kuuondoa umaskini, bali ni serikali tu inayoweza kuufutilia mbali. Kama nilivyotangulia kusema kuwa mtu anayekaa Lahore au Delhi anawezaje kujua kuwa huko kwenye bonde la milima ya Himalaya mtoto mmoja wa mama maskini anakufa na njaa, au wakazi wa miji wanawezaje kufahamu matatizo ya maskini waishio vijijini, lakini serikali inaweza kupata taarifa hizi kwa urahisi. Hivyo basi waliamua kuwa serikali ibebe jukumu hili. Lakini ni lazima ndani ya serikali wawepo watu wengine pia pamoja na mfalme na mawaziri, ili wote waweze kuwakilisha maeneo yao na kuleta taarifa katika makao makuu. Kwa msingi huu, mwanzoni mabadiliko madogo madogo yalifanyika. Kwa mfano, ilielezwa kuwa mfalme akiwa nyumbani

atajuaje kuhusu mahitaji ya wakulima wa kijiji cha Shahpur? Lakini wakulima wa Shahpur wanayaelewa vizuri mahitaji yao. Au mfalme hawezi kuyajua matatizo ya wakazi wa Jhang, lakini watu wa mji huo wanayajua vizuri matatizo wanayokabiliana nayo. Hivyo uundwe utaratibu fulani wa kuifikisha sauti ya watu hao katika makao makuu ya serikali.

## Badiliko la Kwanza Chini ya Demokrasia

Basi kutokana na demokrasia, badiliko la kwanza lililofanyika lilikuwa ni kwamba wananchi walidai kuwa wanayo haki kuwa katika serikali ili waweze kuiarifu serikali mahitaji ya maeneo yao na kuipa serikali ushauri ufaao. Kwa muda fulani njia hii ilifuatwa na bila shaka kwa kiasi fulani ilileta mafanikio. Kwani, mfalme alikuwa hawezi kujua hali ya watu wote, lakini sawa na njia hii wawakilishi walileta taarifa mbalimbali na kuishauri serikali na kurudi makwao wakitulia.

## Ulindaji wa Haki kwa Kupitia Demokrasia na Jitihada za Wafayabiashara na Wasanii

Mwanzoni wawakilishi hawa walitokana zaidi na wakulima, kwa hiyo walizungumzia tu haki za wakulima. Wakulima wakubwa wakubwa walikuwa wanajua na kuwanufaisha zaidi watu wao kutokana na uhusiano wao na watu wakubwa. Hapo mpango mpya ulianza uliokuwa wa wafanyabiashara na wasanii. Waanzilishi wa mpango huo walitangaza kuzilinda haki za

wafanyabiashara na wasanii. Sasa, kutokana na mpango huu ulioitwa msiamamo wa kupenda mabadiliko, wafanyabiashara na wasanii nao pia wakapata uhuru kama wakulima na kufanya mabadiliko katika serikali yaliyoondoa matatizo ya wafanyabiashara na mambo ya wasanii yakawa mapesi.

## Ujamaa

Hali hii iliendelea kwa muda, kisha kundi jingine la watu likajitokeza na kujitahidi kupata haki zao. Kundi hili lilikuwa la vibarua na wafanyakazi katika viwanda na maofisi mbalimbali. Walipoona kwamba wakulima, wasanii na wafanyabiashara walisha pata haki zao, nao pia wakadai wakisema, 'Hamwoni taabu zetu, kwa hiyo sisi pia tutatuma wawakilishi wetu serikalini'. Basi katika baadhi ya sehemu, wawakilishi wa wafanyakazi pia walianza kuchaguliwa kama kawaida kwa uchaguzi na mahali pengine kwa ugomvi. Siku hizi Ujamaa una nguvu sana na kwa hakika hili ni jina la mpango ule ule ambamo vibarua wanapewa haki zaidi kuliko matajiri. Watu hao, kwa lengo la kulinda haki za watu wa kawaida wanataka kutwaa utatwala na wafikiri kuwa kwa njia hii watapatiwa vibarua haki zao.

## Ujamaa wa Kimataifa

Kisha kuendelea mbele watu walisema kwamba bila shaka mipango hii yote inafaa lakini athari zao

zinakomea tu katika baadhi ya nchi maaluum, na hili haliwezi kuwa jambo la furaha kamili. Kama tukifanikiwa kuboresha hali ya watu wa Uingereza, lakini watu wa Ufaransa wanaendelwa kufa na njiaa, basi tunawezaje kupata furaha? Kwa hiyo, maskini na wafanyakazi wa nchi mbalimbali wanapaswa kukubali kusaidiana wao kwa wao. Kidhahiri ilisemwa ya kuwa tunapanua eneo la marekebisho lakini kwa hakika yenyewe ni kuwa matajiri wa nchi moja walipopata hasara kwa sababu ya mpango huo, matajiri wa nchi nyingine wakawasaidia wapinzani wa mpango huo kwa mali, ili mpango huo usifike nchini mwao. Kwa hiyo, vibarua pia walikata shauri kwamba maskini wan chi mbalimbali wakubaliane kusaidiana wao kwa wao, na bila kufanya hivyo hawatapata kufaulu. Hivyo, ujamaa wa kimataifa ulianzishwa baada ya ujamaa wa kitaifa, yaani sio tu kwamba vibarua waiangalie nchi yao tu, bali waziangalie nchi zingine pia.

## Nadharia Tatu za Karl Maksi za Kuboresha Hali ya Maskini

Baada ya hapo mtu mmoja aitwaye Carl Marx[1] alijitokeza. Yeye alikuwa Mjerumani mwenye asili ya Kiyahudi, lakini alikuwa Mkristo. Yeye alitafakari sana juu ya suala hili na kufikia uamuzi huu kwamba ujamaa unaotaka kuleta marekebisho polepole na kuwasukumiza matajiri ili wawapatie wafanyakazi na

maskini haki zao, hauwezi kultea mafanikio hata ndani ya miaka hamsini, mia, bali miaka elfu. Uharibifu wenyewe ni kwamba wanaotawala hawajirekebishi, basi njia rahisi ya kurekebisha huku ni kuitwaa serikali. Yeye anasema kwamba ina maana gani kwamba kama serikali haichimbi mferji mahala fulani kwa miaka mingi, tuing'ang'anie kwa miaka mia kwa ajili ya mfereji. Itwaeni serikali na kuchimba mfereji. Au badala ya kupoteza miaka mingi katika kuisisitiza serikali irekebishe matatizo ya kiwanda fulani, jambo lililo rahisi ni kuuchukua utawala na kurekebisha uharibifu wote. Basi, Maksi alishika kanuni hii ya kwamba hatuwezi kufanya marekebisho ya kuiutamauni pasipo kuijingiza katika siasa. Maadamu hatutwai saisa na madhali hatushiki madaraka ya utawala, marekebisho yoyote ya kisiasa au ya kiutamaduni hayawezekani

## Umaksi na Kanuni yake ya Kwanza

Basi Umaksi, ambao ni tawi moja la ujamaa wa kimataifa, unaruhusu kupata masilahi yako kwa nguvu na unatetea kupata uhuru kwa kupitia mapinduzi ya kisiasa badala ya kupitia mabadiliko ya kiuchumi. Pamoja na hayo, Umaksi unaeleza pia kwamba Wajamaa hawakufanikiwa kwa sababu walianza kufanya kazi kwa kushirikiana na matajiri, ilhali utawala wao ni wa siku nyingi sana kiasi hiki ya kwamba maadam huo bado upo, maskini hawawezi kupata haki yoyote.

Sawa na mawazo ya Maksi, kanuni ya demokrasia si sawa kabisa wala ushirikiano baina ya maskini na tajiri pia si sahihi. Kulingana na maoni yake, matajiri wachukuliwe kama sio wanadamu na maskini wakipata mamlaka yoyote basi wayashike kabisa.

## Kanuni ya Pili ya Umaksi

Nadharia ya pili aliyoieleza ilikuwa ni kwamba ili kupata lengo hilo yapasa kutumia nguvu; undeni kundi na kuishambulia serikali ili kuuteka utawala. Hiyo ndiyo ilikuwa nadharia ya Maksi iliyozalisha Ubolsheviki baadaye.

## Kanuni ya Tatu ya Umaksi

Marksi alitoa rai nyingine pia kwamba wakulima na wasanii wenye mali wamepata nguvu nyingi, na wafanyakazi wamekuwa hawajiwezi, bali hata baada ya kuivunjilia mbali serikali iliyopo hawataweza kulinda haki zao kwa muda mrefu. Kuna kichekesho fulani maarufu kwamba kulikuwa na mtunza farasi aliyekuwa akipata Rupia nane au kumi kwa mwezi. Safari moja mtu fulani alimwambia kuwa siku hizi kila mtu anapata Rupia arobaini au hamsini, lakini wewe unaendelea na mshahara wa rupia nane au kumi tu. Kwa nini humwambii tajiri wako akuongezee mshahara? Kasema nimwambieje? Yule mtu akasema wewe si mtumwa wake, akiongeza mshahara wako, ni vizuri, la sivyo

ufanye kazi mahali pengine. Mwishowe baada ya kufahamishwa sana akawa tayari, na akafunga nia moyoni ya kuwa leo atakapokuja tajiri wangu, nitamwambia waziwazi kuwa amwongeze mshahara wangu, waila naacha kazi. Tajiri wake alikuwa ametoka nje akiwa amepanda farasi, aliporudi mtuuza farasi akasimama mbele yake na kusema, Bwana sikiliza jambo moja. Yeye akasema, 'Ni nini hilo'? Kasema, wote wanapata mshahara mkubwa na mshahara wangu ni mdogo sana. Basi, ama uongeze mshahara wangu waila... hapo tajiri wake akachukua kiboko na kumchapa na kumwuliza "waila utafanya nini? Akasema waila nitavuta subira kwa rupia nane tu. Nitafanya nini tena! Akasahau maneno yote yale. Yaani, alitaka kusema ya kuwa 'Waila nitaacha kazi', lakini baada ya kuchapwa mjeledi mmoja tu akasema "Nitafanya tu subira kwa nane tu, nitafaya nini tena'?

## Matokeo ya Utumwa wa Muda Mrefu

Hivyo, basi, baada ya kuishi muda mrefu utumwani, tabia ya asili ya mtu hubadilika kabisa. Mimi mwenyewe nimeshuhudia kwamba hata kama ujitahidi namna gani kuwanyanyua matopasi na watu wanaohesabiwa kuwa duni kwa kuongea nao lengo hili kwa muda mrefu namna gani mwishowe watasema wakitabasabu — kana kwamba tumerukwa na akili — kwamba jinsi Alivyoumba Mola, ndani yake mabadiiko gani

yanawezaje kutokea sasa. Kana kwamba sawa na mawazo yao, warekebishaji wote wamerukwa na akili. Hiyo ndiyo aliyoisema Karl Maksi kwamba watu hao hawawezi kubadilika. Kama watu wa kawaida wakipewa madaraka, basi wao watajisalimisha kwa kuogopa, kwa hiyo mwanzoni mtu mmoja miongoni mwa wenye kuwahurumia wafanyakazi apewe udikteta, ambaye akiisha waunganisha watu vizuri na kuwaamsha waajiriwa na kufuta kabisa tofauti zote zilizopo baina ya matabaka mbalimbali na kuwatilia vizazi vijavyo nguvu ya kuongea na matajiri ana kwa ana, hapo ndipo warejeshewe watu serikali, lakini si kabla ya hapo, la sivyo utawala utapotea.

## Jitihada za Lenin na Wenzake kwa Kustawisha Hali ya Maskini

Maksi kafa. Baada yake dhuluma ilipofikia upeo, kilijitokeza chama kimoja kilichoanza kuleta umoja baina ya watu sawa na mafundisho ya Maksi. Miongoni mwa watu mbalimbali waliounganika vizuri kulingana na mafundisho ya Maksi mmoja wao ni Lenin[2] aliyekuwa dikteta wa kwanza wa Urusi. Lenin na wenzake waliyafuata kikamilifu mawazo ya Maksi. Kwa muda fulani waliendelea kufanya kazi kwa pamoja na kuwahamasisha maskini kwa kuwaambia ya kwamba nyinyi mnatembea rabana na mnashinda na njaa, lakini kuna matajiri wa nchi hii hii wanaoishi kwa

starehe na raha. Wakati mwingine wakasema kuwa huu ni uadilifu wa aina gani ya kwamba katika kiwanda kimoja tu mfanyakazi mmoja anafanya kazi mchana hadi jioni, na jioni anapewa ujira kidogo sana hata kwamba kwa taabu anawalisha mkewe na watoto wake na upande mwingine watoto wa mmiliki wa kiwanda hicho wanavaa mavazi ghali sana na kula chakula kizuri. Kwa njia hii wakatia harara katika nchi nzima na vyama vingi vikaibuka dhidi ya matajiri.

## Uanzishwaji wa Vyama vya Bolsheviki na Mensheviki

Nguvu yao ilipozidi sana na walipofikiri ya kwamba sasa tumeshafikia hatua kuwa tutaupata utawala karibuni, basi waliitisha kikao kwa shabaha ya kujipangia kwamba baada ya kupata utawala kwa njia gani tutafanya kazi. Katika kikao hiki kulitokea hitilafu kati yao. Na Martov, ambaye alikuwa kiongozi mwenye nguvu kama Lenin katika chama, alihitilafiana na Lenin, basi vikaibuka vyama viwili, kimojawapo kikaitwa Bolsheviki na kingine Mensheviki. Jina Bolshevik likachaguliwa kwani maana yake ni wingi. Kwa kuwa Lenin alikuwa na wanachama wengi, kwa hiyo chama chake kikaitwa Bolsheviki, na Mensheviki, maana yake ni uchache na kwa kuwa wapinzani wake walikuwa wachache kwa hiyo chama chake kikaitwa Mensheviki.

# HITILAFU BAINA YA NADHARIA ZA LENIN NA MORTOV KUHUSIANA NA NIDHAMU YA SERIKALI

## Hitilafu ya Kwanza

Lenin, alikuwa akimfuata Maksi katika mambo mengi. Yeye alikuwa ameweka kanuni hii kwamba sisi tunatakiwa tujitenge na vyama vingine vyote, na bila ya kufanya hivyo hatuwezi kupata malengo yetu sawasawa. Lakini Mortov alikuwa na fikara kwamba kabla hatujapata nguvu, tunapaswa kuwa na ushirikiano mzuri na wenye nguvu ambao ni watendaji bora.

Ilmuradi, nadharia ya Lenin ilikuwa ni kwamba hatuhusiani na wengine na chochote tutakachopata tutapata kwa nguvu zetu bila hisani ya yeyote. Kwa maneno mengine, Lenin alikuwa na nadharia hii ya kwamba sisi hatutaungana na wengine, tunao ukweli nasi tuna yakini kuwa hatimaye tuapata ushindi.

## Hitilafu ya Pili

Tena Lenin alikuwa na fikara ya kwamba mwanzoni hatuwezi kumudu bila udikteta. Lakini Mortov alikuwa na wazo hili kwamba yafaa tangu mwanzo iundwe serikali ya kidemokarasia. Mortovu alifahamu kwamba Lenin ndiye atakuwa kiongozi sio mimi, kwa hiyo alipenda tangu mwanzo utawala wa kidemokrasia uwekwe.

## Wazo la Mortov la Kufuta Adhabu ya Kifo

Kisha Mortov, kulingana na kanuni ya kiujamaa, alitaka adhabu ya kifo ifutiliwe mbali katika serikali mpya, lakini Lenin akasisitiza kuwa japo adhabu ya kifo yapasa kuondolewa, lakini ikiwa itafutwa wakati huu Tzar — matamshi yake Zaar — hataweza kunyongwa. Lenin alifikiri kuwa kama Tzar atakuwa hai hata baada ya kusimamishwa, itakuwa vigumu kwao kuendesha mambo ya serikali. Kwa hiyo, Lenin alisema ya kuwa hata kama kumwua Tazar peke yake sheria ya kutoa adhabu ya kifo yahitajika, basi yafaa ibaki tu. Kana kwamba moyoni mwake uadui wa Tzar ulikuwa umezidi kiasi hiki kwamba hata kwa kumnyonga Tzar pekee kama kanuni hii ikihitajika, basi lazima ibaki tu. Kutokana na hitilafu hizi, Lenin alipata kura zaidi na wenzake walipata haki ya kukiongoza chama, na kutokana na wingi wao wakaitwa Bolsheviki. Na wapinzani wao, kwa sababu ya uchache wao, wakaitwa Mensheviki. Baada ya Tzar kuondoka, kwanza Chama cha Mensheviki kilipata utawala wa nchi, kwani vyama vingine vya nchini vilifikiria serikali yao kuwa yenye faraja zaidi. Kisha baadaye chama cha Bolsheviki kwa kutumia nguvu wakaimarisha serikali yao.

## Kanuni Sita za Ubolsheki za Kiuchumi na Matokeo yake

Sasa hebu niwaambieni kanuni za kiuchumi za Ubolsheviki ni nini. Ikumbukwe kuwa sababu kuu ya

kuunda kanuni hizi ilikuwa ni kufuta tofauti baina ya tajiri na maskini. Kama tajiri anavyopewa dawa akiwa mgonjwa, ndivyo ambavyo maskini pia aipate; maskini avae mavazi mazuri kama anavyovaa tajiri na kama anavyoshiba tajiri maskini vilevile ashibe, asiwe na njaa. Vivyo hivyo dhuluma zipungue na matatizo yote ya kiuchumi wanayoyakabili maskini yatatuliwe. Kwa shabaha hiyo, kanuni za kiuchumi zilizoundwa na Ubolsheviki sawa na kanuni za Maksi ni hizi zifuatazo.

## Kanuni ya Kwanza

Kwanza, mtu alazimishwe kutoa sawa na uwezo wake. Kwa mfano, mtu mmoja ana shamba la ekari kumi na mwingine ana shamba la ekari mia moja. Sasa hawatafanya hivi kwamba wachukue Rupia chache kutoka kwa mwenye ekari kumi na Rupia chache kutoka kwa mwenye ekari mia moja, bali wataangalia ya kwamba mwenye ekari kumi ana mahitaji kiasi gani na mwenye ekari mia kiasi gani. Na fedha zitakazozidi baada ya kutimiza mahitaji yao, zitachukuliwa na serikali. Kwa mfano, watakapoona kuwa mwenye ekari kumi anawalisha mkewe na watoto wake na mwenyewe pia anakula na anawalisha wanyama wake pia, kisha fedha kiasi kadha inabaki kwake, basi serikali itasema kwamba fedha hiyo siyo yako, bali ni ya serikali. Na vivyo hivyo mahitaji ya mwenye ekari mia au mwenye ekari elfu moja ndivyo yatahesabiwa,

na kiasi chochote cha fedha kitakachosalia kitachukuliwa na serikali, kwani wanasema kwamba ndivyo ilivyo kanuni yetu ya kuwa mali iliyozidi kuliko mahitaji ya mtu, ichukuliwe na serikali.

## Kanuni ya Pili

Kanuni ya pili waliyoweka ilikuwa ni kumpa mtu sawa na mahitaji yake. Ilmuradi, sawa na kanuni ya kwanza, mapato ya ziada ya mwenye ekari kumi au mwenye ekari mia yachukuliwe, na sambamba na kanuni hii ya pili, mtu apatiwe sawa na mahitaji yake. Kwa mfano serikali ikipokea Rupia elfu tano kutoka kwa mtu mwenye ekari mia, lakini mtu huyo anao wanafamilia wawili au watatu, kwa hiyo hatapewa fedha nyingi, bali atapewa sawa na idadi ya wanafamilia wake. Kwani, hela iliyochukuliwa kutoka kwake, ilichukuliwa sawa na kanuni hii ya kwamba, kitu cha ziada kichukuliwe na serikali, naye atapewa sawa na kanuni nyingine ya kuwa mtu apewe kulingana na mahitaji yake. Na ataambiwa kwamba ulikuwa na fedha nyingi, kwa hiyo serikali imechukua nyingi na kwa sababu mahitaji yako ni madogo kwa hiyo unapewa fedha kidogo.

## Kanuni ya Tatu

Kanuni ya tatu waliyoiweka ilikuwa ni kwamba serikali inayo haki ya kuchukua mazao yanayozidi mahitaji ya mtu, ambayo yapasa yatumika kuiboresha hali ya nchi

kwa ujumla. Kwa mfano, kuna wakulima wawili, na kila mmoja wao ana shamba la ekari kumi, mmoja wao alifanya kazi kwa bidii zaidi na akapata kwa kila ekari mazao *Mann* 30 — *mann* ni sawa na ratili 82.6, au karibu kilo 41.3 — na mwingine alipata mazao *mann* 3 tu kila ekari. Yaani, mmoja amepata *mann* 300 na mwingine *mann* 30. Sasa aliyepata mazao *mann* 300, mahitaji yake, kwa mfano, ni mann 40 tu, basi serikali itamwambia achukue *mann* 40 tu na *mann* 260 azitoe kwa serikali. Kadhalika mtu wa pili aliyepata mazao *mann* 30, kama *mann* 10 za nafaka zatosha kwa ajili yake, serikali itamwambia kuchukua *mann* 10 za nafaka na nyingine *mann* 20 azitoe kwa serikali. Basi kanuni yao ya tatu ni hii kwamba, mazao yanayozidi kutokana na juhudi au kwa bahati tu, yachukuliwe kwa sababu hii ni haki ya serikali.

## Kanuni ya Nne

Kanuni ya nne waliyoiweka ilikuwa ni kwamba yapasa utawala usiwe juu ya watu, bali uwe juu ya vitu. Walisema kwamba kanuni hii ya kuchukua tu mazao ya zaida haitoshi, kwani kwa njia hii ni watu tu wanaotawaliwa, ilhali kimsingi mamlaka yanatakiwa yawe juu ya vitu. Kwa mfano, katika maeneo fulani, zao la miwa linastawi vizuri, basi wanasema serikali iwe na madaraka ya kuwaamuru wakazi wa eneo hilo wapande miwa tu. Au katika sehemu nyingine ngano inastawi

sana, basi serikali iwe na mamlaka ya kutoa amri ya kupanda ngano tu, na mtu asiweze kupanda kitu kingine sehmu hiyo minghairi ya ngano. Au ikiwa serikali yataka kutoa amri ya kwamba katika eneo fulani pamba ipandwe au mtama upadwe, basi wote walazimike kufuata amri ya serikali, na mtu yeyote asiikiuke amri hiyo. Basi kulingana na kanuni ya nne walikata shauri kwamba sisi ndio tuakaogawa mazao na kuamua kuwa katika maeneo fulani vitu fulani vipandwe na watu watawajibika kupada tu kitu hicho.

## Kanuni ya Tano

Kanuni ya tano waliyoweka ilikuwa ni kwamba vipawa pekee vya kiakili havina thamani yoyote bila ya kufanya kazi kwa mkono. Walisema kuwa kusema kwamba mtu fulani anatafakari juu ya jambo fulani la kielimu ni upuuzi tu; kitu cha msingi ni kufanya kazi kwa mkono. Wafanyao kazi ya akili nao wanapaswa kufanya kazi za mkono; wasipofanya kazi kwa mikono, basi hatutawasaidia hata kama wafe kwa njaa.

## Kanuni ya Sita

Kanuni ya sita waliyoiweka ilikuwa ni kwamba kwa ajili ya msimamo wetu siku zote ichaguliwe njia ya kushambulia badala ya kujitetea. Haipasi kujitetea, bali yapasa kuwashambulia wengine, kwa msimamo wetu.

## Matokeo ya Kanuni ya Kwanza: Kunyang'anya Rasilimali Zote za Matajiri

Matokeo ya kanuni ya kwanza ni kwamba Ubolsheviki ulitwaa rasilimali za matajiri wote kwa sababu walikuwa wamekwisha amua kwamba chochote wanachopata wachukue tu. Yatwaeni mashamba, viwanja na mali zingine. Kadhalika chukueni tu kwa nguvu chochote alicho nacho mtu yeyote.

## Matokeo ya Kanuni ya Pili: Kuwapatia Vifaa Wanaofanya Kazi kwa Mkono, Sawa na Mahitaji yao

Sawa na kanuni ya pili, Ubolsheviki ulibeba jukumu la kumpatia vifaa kila anayefanya kazi kwa mkono sawa na mahitaji yake. Kwa mfano, katika nyumba moja kuna watu watano, sasa watawaamulia mara moja ya kwamba watu hao watano wapewe nguo kiasi fulani nafaka kiasi fulani na kuni kiasi fulani. Vivyo hivyo waganga watateuliwa watakaowatibu bure wakiugua. Ilimuradi kwa njia hii, kila mmoja atapata nguo ya kuvaa, nafaka ya kula na dawa. Kazi ya serikali itakuwa ni kutayarisha orodha na kutimiza mahitaji yote ya watu. Na kwa hakika, kama ichunguzwe vizuri, Ubolsheviki umeondoa shida hii, na kama kazi ifanyike kwa njia hii, basi hakuna mtu atakayeonekana mwenye njaa au rabana, isipokuwa mtu wa dini, kama vile padre n.k., kwani sawa na nadharia yao, bila kufanya kazi kwa

mkono, vipawa vya kiakili havifai kitu. Basi, hao wanawachukulia mapadre, watu wa dini, maulamaa, na wanafalsafa kuwa ni watu wasiofaa, na wanasema kwamba watu hao wanapaswa wafanye kazi yoyote kwa mkono, waila serikali haitawajibika kitu kama wanashinda na njaa.

## Matokeo ya Kanuni ya Tatu: Uamuzi wa Serikali wa Kuvichukua Vitu Vilivyozidi Kiwango Kilichokadiriwa na Serikali

Sawa na kanuni ya tatu, waliamua kuvichukua kutoka kwa wakulima na matajiri, vitu vyote vilivyozidi kiwango kilichowekwa na serikali. Yaani, ikiwa mtu fulani anazalisha shambani mwake *mann* 50 za nafaka, lakini *mann* 20 tu zinatosha kwa mahitaji yake, basi *mann* 30 za nafaka zitachukuliwa na serikali, kwa madai kwamba hizo zimezidi kuliko mahitaji yako, kwa hiyo ni haki ya serikali. Au kama kuna mtu anayemiliki ardhi kubwa, na anaweza kujikimu kwa ardhi kidogo tu, basli mtu huyo ataachiwa sehemu inayomtosheleza na itakayobakia itachukuliwa na serikali.

## Matokeo ya Kanuni ya Nne: Ukosefu wa Uhuru wa Utendaji

Sawa na kanuni ya nne, uhuru wa utendaji wa wakulima, wafanyabiashara na wasanii umenyang'anywa na walilazimishwa kufanya kazi za kilimo, biashara na ufundi sawa na matakwa ya serikali. Kwa mfano,

ikaamriwa ya kwamba katika eneo fulani la maili mia, ngano tu ndio ipandwe au katika sehemu fulai ipandwe miwa tu na sehemu fulani pamba pekee. Katika nchi yetu, mara nyingi wakulima wanapanda mtama mrefu katika *Marla* mbili — *marla* ni yadi 30 za mraba — pamba katika *Marla* mbili na miwa katika *Marla* mbili. Wakulima wadogo hawafanyi hivyo, lakini wenye ardhi ekari 10-12 lazima wanafanya hivyo. Ubolsheviki ulitoa uamuzi kuhusu sehemu mbalimbali ya kwamba hapa isilimwe ngano bali limeni miwa tu. Kuna wilaya ambapo hulimwa ngano tu, kuna wilaya ambazo inalimwa miwa tu na katika baadhi ya wilaya inalimwa pamba tu, kwani wanasema sehemu hizo zinafaa kwa mazao haya, hivyo tunaamuru kitu kingine kisipandwe hapo. Na kama mtu akisema kuwa nitapata ulaji toka wapi, hapo wanasema kuwa sisi ndio tutakupatia chakula na nguo, unao wasiwasi gani? Wewe utalazimika kulima kile tu tutakachokuambia. Hivyo, mkulima amekuwa kama mfanyakazi tu.

## Matokeo ya Kanuni ya Tano: Kuingilia kati Nidhamu ya Kidini

Sawa na kanuni ya tano, waliingilia kati nidhamu ya kidini na kusema kuwa mapadre hawastahili kupewa chakula mpaka wafanye kazi kwa mikono. Wakasema ya kuwa maadamu mapadre hawafanyi kazi kwa mikono, basi hao ni wazembe, na wazembe hawana haki ya

kupewa riziki. Basi ama mapadre wanalazimishwa kufanya kazi au mapadre wanafanya ibada kidogo na katika muda uliobaki wanatumia kufanya kazi.

## Hila ya Kuzalisha Upagani

Kutokana na uadui huo wa kidini, wakatafuta njia mpya na wakaamua kuhusu dini ya kuwa kila mmoja awe huru kuchagua dini. Wazazi na wazee hawana haki yoyote ya kuwafundiha watoto wao mambo ya dini katika utoto wao; kuwafundisha kuwe kikamiifu mkononi mwa serikali. Wanasema, angalieni, watoto wanafanyiwa dhuluma namna gani kwamba wanaziathiri nyoyo zao kidini utotoni mwao. Matokeo yake ni kwamba watoto wa Waislamu wanakuwa Waislamu, watoto wa Mabaniani wanakuwa Mabaiani na watoto wa Waparsi wanakuwa Waparisi. Hii haitakiwi hata kidogo, bali watoto wawe huru na athari ya aina yoyote ya kidini. Mtoto akibalehe, ajichagulie dini yoyote aipendayo. Kabla hajabalehe, kutia athari ya din yako moyoni mwa mtoto kwa nguvu ni dhuluma kabisa. Basi, matokeo ya kanuni hiyo kukawa sumu kwa ajili ya dini. Wanawatenga watoto na wazazi na kuwafundisha katika shule zao ambapo watoto hawapati hata kusikia jina la dini. Na anapofikia umri wa miaka kumi na minane au ishirini na akiwa mpangani kamili, hapo wanasema kuwa sasa ameshabalehe na kufikia umri wa kutumia akili yake sawasawa, hivyo sasa ajichagulie dini yoyote

aitakayo. Lakini, wakati huo anawezaje kuwa na fahamu ya kujichaggulia dini ambapo upangani unakuwa umeishapenya ndani yake kikamilifu. Ilmuradi, wao wanasema, sisi hatuwadhulumu watoto, bali tuaniacha mioyo yao iwe safi, isiyo na alama yoyote, ili baadaye watoto wenyewe waitilie nakshi yoyote waipendayo. Lakini kuweka safi mioyo yao kunamaanisha Upagani tu. Wanawatilia masikioni mwao sawa na matilaba yao kwa miaka 18-20, basi kusema kwao kwamba sisi tunaiacha mioyo yao iwe safi ni uongo mtupu. Kwa hakia wao huwatumbukiza kwenye shimo la Upangani. Basi kanuni hii imewafanya vizazi vijavyo kuwa Wapagani.

## Matokeo ya Kanuni ya Sita: Usambazaji wa Mawazo yao katika Nchi zingine

Kulingana na kanuni ya sita, walianza kueneza mawazo yao kuwachochea watu katika nchi zingine, kwani, walikuwa wameshaamua kuwa siku zote washike njia ya kushambulia badala ya kujitete. Kwa hiyo walianza kuwatuma maajenti wao katika Ujerumani, Japani na Italia. Katika nchi za nje wakajulikana kwa jina la Wakomunisti. Katika Panjab pia Wakomunisti wanapatikana. Wapo katika mikoa mingine ya India pia, kama vile Bihar na kadhalika. Hivyo serikali ya kanuni iliyoenezwa na Maksi, (Mjerumani mwenye asili ya Kiyahudi) ikapatikana katika Urusi na Mwendeleo huo

ulianzishwa kwa lengo hili kuwa kila mtu atapata chakula, mavazi, umaskini utatoweka na usawa utapatikana baina ya matajiri na maskini. Kwa kuwa Mwendeleo huo ulianza taratibu kuiathiri dunia nzima, kwa hiyo matokeo mengine ya Mwendeleo huo pia yakajitokeza.

## Upingaji wa Ubolsheviki katika Ulaya kwa Sura ya Uanzishwaji wa Miendeleo Mitatu

Mawakala wa Ubolsheviki walipoenea katika nchi za Ulaya na wakaanza kuzileta nchi zingine chini ya athari za mwendeleo huu, hapo nchi zingine za ulaya, kama vile Ujerumani na Italia, zilizokuwa zikiota ndoto ya kutwaa uchumi na siasa ya dunia, baada ya maanguko ya serikali zenye nguvu za wakati huo waliona matamanio yao kutotimia. Nchi hizo zilikuwa zikifikiri ya kuwa Ufaransa, Uingereza na Marekani zimekwisha itawala dunia kwa muda mrefu, na sasa baada yao kutawala kwa muda mrefu zimeingia starehe na anasa za kidunia na zinaendelea kudhoofika, kwa hiyo sasa ni haki yetu ya kuitawala dunai.

Basi Ujerumani, Italia na Uhispania, ambazo zilikuwa zikiota ndoto ya kuwa serikali za Uingireza, Ufaransa na Marekani sasa zimeshazeeka, hivyo sasa yapasa sisi tupewe nafasi badala yao, ili nasi pia tupate ladha ya kuawala, Mwendeleo huo ulipofika huko, zikapatwa na mahangaiko na wasiwasi mwingi. Hali yao ilifanana

na hali ya mwewe na tai wanayemwona ng'ombe yuko karibu kufa, basi huwa wanasubiri kwa hamu sana kuwa afe haraka ili wampapure na kula nyama yake. Vivyo hivyo, Wajerumani na Waitalia walikuwa wakisubiri maanguko ya serikali za Uingereza, Ufaransa na Marekani, ili waziteke serikali zao na kufaidika na mali ya dunia kama hao walivyofaidika nayo kwa muda mrefu sana. Watu hao waliingiwa na wasiwasi mwingi kutokana na Mwendeleo huo, kwani walitaka kuipata serikali, lakini mwendeleo huu una lengo la kuziangamiza serikali zote. Matokeo yake ni kwamba upinzani ulipatikana katika nchi hizo. Basi, nchini Italia ukazalika Ufashisti chini ya uongozi wa Mussolini, na katika nchi ya Ujerumai, Hitler alianzisha Unazi na nchini Uhispania Mwendeleo wa Franco na Ufalangi ukaibuka.

## Lengo la Miendelio Mipya Dhidi ya Ubolsheviki

Shabaha ya Miendeleo hii mitatu ilikuwa ni moja tu, nayo ilikuwa kupambana na Ubolsheviki. Wao walifahamu ya kuwa mawazo haya yakienea baina ya watu, basi maendeleo yetu yatakwama. Mwendeleo wa Ubolsheviki ulikuwa lazima uwavutie watu wa kawaida, kwa hiyo watu maskini waliuunga mkono mpango huo, kwa sababu walisema kuwa kwa kupitia mpango huo tutapata nguo, chakula na dawa na tutatimiziwa mahitaji yetu yote. Ngoma za mbali hunoga. Katika India pia

kuna watu wanaouunga Mwendeleo wa Ubolshaviki, kwani wanaelewa ya kwamba watu waserikai hiyo humjia kila mtu na kumpatia suruali na shati vilivyoshonwa tayari. Kadhalika nafaka na mahitaji mengine wanapaliwa na serikali mara moja. Lakini watu hao hawajui kwamba, ikiwa mpango huu uanze duniani,hapo ingawaje kila mmoa atapata chakula na nguo, lakini kile kitakachosalia kitachukuliwa na serikali. Lakini watu wa kawaida huwa haawayatafakari mambo hayo, wanachokiangalia ni hiki tu kwamba sisi sote tuapata chakula na nguo, na hakuna yeyote atakayekuwa rabana au mwenye njaa.

## Njia Mbalimbali za Italia na Ujerumani Kuunga Mkono Ufashisti na Unazi na Kuupinga Ubolsheviki

Ilmuradi, katika Ujerumani na Italia pia watu wa kawaida walianza kuathirika na Mwendeleo huo na wakaanza kusema yafaa kuwa hivyo nchini mwetu pia, kwani kila mmoja atapata utulivu na shida na taabu itatoweka.

## Njia ya Kwanza ya Kufanya Propaganda Dhidi ya Ubolsheviki Katika Ujerumani na Italia

Mwishowe, Hitler na Mussolini walitatua tatizo hilo na kuwaambia watu kuwa msiwe na wasiwasi, kwani Ufashisti na Unazi pia utachukua mali ya matajiri na kwa kuteka biashara na viwanda vyote vya nchi na kuwapatia maskini haki zao. Hivyo, basi, katika mustakbali hakutakuwa na mahusiano ya moja kwa

moja baina ya wafanyakazi na matajiri bali yatakuwa kwa kupitia serikali, na kwa njia hii hawatapata taabu zile walizokuwa wakizipata kutoka kwa wafanyabiashara au kwa wenye viwanda, kwani serikali zetu zenyewe ndizo zitakuwa na mamlaka juu ya biashara na viwanda na kuwapatia maskini haki zao. Pamoja na hayo walisema pia kwamba kwa kuitajirisha nchi, kuna haja ya kuwa na viwanda vikubwa vikubwa na biashara kubwa kubwa, ili kwa kuchukua mali kutoka kwa matajiri, itumike kwa maendeleo yenu. Kwa kulipata lengo hilo, ni muhimu kufanya biashara na nchi za nje na baada ya kupora mali yao, itumiwe katika kuboresha hali ya maskini wa nchi yetu. Kwa mfano, waliwaambia watu kuwa hamwezi kuipokonya China, Marekani, Uingereza au Ufaransa. Njia ya kupokonya ni moja tu ya kwamba tuwe na meli kubwa kubwa na viwanda vikubwa vikubwa na biashara kubwa kubwa, halafu wafanyabiashara wetu waende katika nchi za nje na kunyang'anya mali zao na kuzileta nchini. Basi waliwafundisha wananchi wao ya kwamba wawaache matajiri wa nchi yao wachume mali kisha tutawanyang'anya mali zao na kuwapatia ninyi. Na kama isitokee hivyo, basi itakuwa sawa na mfano huu kwamba kulikuwa na mtu fulani aliyekuwa na koo mmoja ambaye kila siku alikuwa akitaga yai moja la dhababu. Mtu huyo alishikwa na tamaa ya kwamba ikiwa atamlisha zaidi, basi koo huyo atataga mayai

mawili kwa siku. Basi siku moja alimlisha sana mno, lakini matokeo yake yule koo akafa, naye akalikosa hata lile yai moja la dhahabu. Vivyo hivyo, serikali za Ujerumani na Italia ziliwaambia watu wao ya kwamba kama hatutawapa matajiri nafasi ya kuchuma mali, basi baada ya kuwanyang'anya mali zao mara ya kwanza, watakuwa maskini, na mtaweza kuwanyang'anya mara moja tu. Lakini baada ya kuwanyang'anya mali, mkiwapa tena nafasi ya kuchuma mali, basi baada ya wao kuchuana mali mtaweza tena kuwanyang'anya mali zao. Kwa hiyo, mtaweza kupata mali zao mara kwa mara. Basi waacheni wafanyabisashara wakubwa wachume mali, na kila mara watakapokuwa na fedha nyingi, basi zitachukuliwa kutoka kwao na kupewa nyinyi.

## Njia ya Pili ya Kufanya Propaganda Dhidi ya Ubolsheviki

Jambo la pili walilowaambia wananchi lilikuwa ni kwamba Ubolsheviki unaupinga Ubeberu na hautaki serikali ya wageni. Lakini hali yenyewe ni kwamba Waingereza kwa kutawala nchi nyingi kwa muda mrefu, wameshakusanya mali nyingi, na hiyo ndiyo hali ya Marekali na Ufaransa ya kwamba zinatawala siasa na uchumi wa dunia. Lakini sasa, ilipofikia zamu yetu, hoja zinatolewa kuwa hiyo ina hasara kadha wa kadha. Hoja hizi hatuzikubali. Sisi pia tutaziteka nchi zingine na kuzileta mali zao nchini mwetu na kuwagawia

wananchi wenye hali ndogo. Maskini walilipenda sana jambo hilo, nao pia hatimaye walianza kuunga mkono Mwendeleo huu.

## Njia ya Tatu ya Propaganda Dhidi ya Ubolsheviki

Kisha waliwaeleza wananchi wao ya kuwa Mwendeleo wa Ubolsheviki hauendelei kupata nguvu wenyewe, bali kwa hakika unasaidiwa na watu wa Marekani, Ufaransa na Uingereza, ili Wajerumani na Waitalia wasiweze kupata sehemu katika mali yao. Hivyo, jazba dhidi ya Ubolsheviki ilizalika sana nchini.

## Njia ya Nne ya Propaganda Dhidi ya Ubolsheviki

Tena waliwaambia wananchi wao jambo jingine, na wakasema kwama tukiwapokonya matajiri wa nchi yetu leo, hata hivyo hakitainuka kiwango cha uchumi wetu. Kwani nchi yetu ni maskini na ina mali kidogo sana, na ugawaji wa fedha kidogo hauwezi kuwatajirisha watu wa nchi hii. Kwa mfano kuna maskini mia moja na fedha iliyopo ni Rupia hamsini tu, hapo kila mmoja atapata *Anna* nane (thumuni). Na thumuni haiwezi kuiborehsha hali ya maskini. Basi waliwafahamisha maskini kwamba tayari nchi zetu ni maskini na hata kama ukija Mwendeleo wa Ubolsheviki, kiwango cha uchumi cha nchi nzima hakitainuka kwa kiasi kilichopo katika nchi za Uingereza, Marekani na Ufaransa bila mwendeleo wa

Ubolsheviki. Basi Ubolsheviki utakuwa ni kama sumu inayoua kwa nchi zao. Naam, kama ikikubaliwa sera yenye hima ya Ufashisti na Unazi, basi upande mmoja nidhamu yetu yenye nguvu itazileta mali za Marekani, Uingereza na Ufaransa baada ya kuzishinda, na upande mwingine kwa kuziteka nchi zingine itazitajirisha nchi zetu hizi. Matokeo yatakuwa ni kwamba baada ya kupata mali nyingi, chini ya nidhamu ya utawala wa taifa wa kijamaa, hali ya maskini itakuwa bora zaidi kuliko ile ambayo inaweza kuwa chini ya nidhamu ya Ubolsheviki. Kwani, ugawaji wa mali kidogo hauwezi kumtajirisha kila mwananchi, lakini ugawaji wa mali nyingi utawafanya wananchi wote kuwa na raha.

## Kukubaliwa kwa Ufashisti na Unazi katika Italia na Ujerumani

Nadharia hizo zilikuwa ambazo — licha ya kuwepo kwa mawakala wa Ubolsheviki katika Italia, Ujerumani na Uhispania — watu walianza kuelekea kwenye Unazi na Ufashisti, kwani walisema ya kwamba tunaweza kushiba vizuri zaidi kwa Unazi na Ufashisti, na hatushibi kwa Ubolsheviki. Basi, wakaamua kuwapa nguvu viongozi wa nchi yao ili wakipata ushindi juu ya Uingereza, Ufaransa na Marekani wazilete mali zao na kuzigawa katika Italia, Ujerumani na Uhispania.

## Njia ya Tano ya Propaganda Dhidi ya Ubolsheviki yaani Harakati za Kuangamiza Dini Zilizotokana na Utawala wa Nje

Watu hao waliodai kuwa na Ujamaa wa Kitaifa, walieneza pia jambo jingine, nalo ni kwamba kama Wamarekani, Waingereza na Wafaransa wanavyotupatia hasara kwa njia ya Ubolsheviki, ndivyo hivyo mataifa haya yenye mali yanavyosababisha fitina nchini kwa njia ya athari ya dini yao ya nje. Kwa hiyo, dini yoyote isipate madaraka nchini ambayo iko chini ya nguvu za kigeni. Basi kwa sababu iyo hiyo, Hitler alianza kufuta dini ya Katoliki na dini ya Uyahudi, bali kwa hofu hii kwamba siku za usoni watu wanaotokana na kizazi cha Kiyahudi. Bali kwa kuogopa kwamba katika siku zijazo Waisraeli wasianze kueneza athari ya Kibolsheviki, kwani huko Urusi Wana wa Israeli wanayo madaraka, yeye aliamua kuwaangamiza pia Wakristo wa Kiisraeli. Sababu hasa ya Hitler kuwa mpinzani wa Wayahudi ni hii tu kwamba dini zote ambazo makao makuu yao yako nje ya Ujerumani, zisipatiwe nafasi ya kupata nguvu nchini. Hii ndiyo sababu hasa ya Hitler kuipinga dini ya Kikatoliki. Watu wengine kwa kuwa hawana makao makuu nje ya Ujerumani, kwa hiyo hawataangalia popote nje ya Ujerumani. Yaani, dini yao watakayoifuata, hata iwe yeneye kutoa maamrisho ya kishenzi namna gani, wao peke yao watakuwa nayo.

## Matokeo ya Jitihada za Kuangamiza Dini Zilizo chini ya Nguvu za Nje

Kutokana na athari hii imeanza katika Ujerumani. Miendeleo ya kidini inayowaelekeza watu kwenye itikadi za zamani za kuabdu masanamu. Basi, Mwendeleo mmoja ambao walishughulikia sana Jenerali Ludendroff[3] na mkewe ni huu kwamba katika zama za kale Wajeruami walikuwa wakiabudu mbwa, sasa wanatakiwa tena kuelekea upande huo. Haya ni matokeo ya mafundisho yale ya Hitler ya kwamba chagueni njia ambayo kwayo kaumu yoyote isiweze kuleta mfarakano nchini kutokana na athari zake za kidini za nje, na yapsa kuwa isiwepo dini yoyote nchini ambayo makao yake makuu yako nje ya Ujerumani. Kwa msingi huo huo, Ujerumani imeanza kufuta dini ya Roman Katoliki na ya Kiyahudi. Waitalia hawakufanya hivyo, kwani Roma ndiyo makao makuu ya dini ya Katoliki, na kwa sababu hiyo chama cha Ufashisti hakikuipinga sana dini hiyo, lakini walijaribu kupunguza madaraka yake ili jumuiya ya kidini ya nchi isiweze kuleta kikwazo katika kazi ya chama cha kisiasa. Badaaye, kutokana na athari ya Hitler, walianza kuwapinga Waisraeli pia, kwani waliambiwa kuwa kwa upande mmoja, kaumu hiyo inaeneza athari ya Ubolsheviki na upande mwingine kwa kuwa na athari maalum katika serikali zinazotawala, inaiimarisha pia

athari yao. Uhispania ilianza kuupinga Ubolsheviki na mataifa yaliyopo madarakani, lakini haikuwapinga Wayahudi kwa kiasi ambacho walipingwa katika nchi za Ujerumani na Italia.

## Njia ya Sita ya Propaganda Dhidi ya Ubolsheviki

Kisha kuna nadharia nyingine iliyoenezwa na Hitler na Mussolini kwa lengo la kuwashawishi watu ili waungane nao, nayo ni kwamba inafahamika kutokana na kutafakari juu ya nadharia ya mageuko ya pole pole kwamba kitu kilicho bora kabisa duniani kinasonga mbele, na kutokana na kitu hicho kusonga mbele, kila hatua ya dunia inaelekea kwenye maendeleo. Kwa msingi wa nadharia hiyo, alisema ya kuwa taifa la Kiaria ni lenye kipaji zaidi kuliko mataifa yote, kwa hiyo, hasa kizazi cha Kijerumani, na vizazi vingine vya Kiaria, kwa kawaida, wawekwe mbele. Hapo siwezi kuacha kusema kwamba katika jambo hilo Hitler anakuwa ni mwanafunzi wa Pandat Dayanand, kwani Pandat Dayanand ndiye aliyeeneza nadharia hiyo kwa mara ya kwanza kabisa kuwa kizazi cha Kiaria ni bora kuliko vizazi vyote. Kwa vyovyote, kwa kuwa Wajerumani wanatokana na asili ya Waaria, na sawa na kanuni ya Hitler, kizazi cha Kiaria ni bora kuliko vyote, kwa hiyo Hitler akiitilia wazo hili mioyoni mwa watu ya kwamba kizazi kilicho bora kinapaswa kupewa utawala.

Yeye anasema kuwa watu wanafuga ng'ombe au farasi bora na hawapendi kufuga farasi au ng'ombe wasiokuwa bora. Lakini la kushangaza ni kutojali jambo hilo katika mambo ya utawala na kupuuza ya kuwa watu wenye ubora ndio wanaostahii duniani kutawala. Na kwa kuwa hivi sasa sisi ndio bora kuliko wote, kwa hiyo ni haki yetu kutawala na kuwafanya wengine kuwa watumwa kama binadamu anavyomfanya punda kuwa mtumwa wake. Haiwi kuwa yeye amfuate punda. Jinsi ambavyo si dhuluma kumweka punda chini ya utumishi wako, ndivyo ambavyo ni wajibu wetu kuwaweka watu chini ya utumishi wetu na kuwatawala. Nadharia hiyo nayo pia watu walipenda sana, na hivyo nchi nzima ikawaunga mkono Hitler na Mussolini. Muhtasari ni huu kwamba kwa sasa kuna Miendeleo mitatu iliyopata nguvu duniani kwa lengo la kuondoa matatizo ya umaskini.

## Faida Waliyoipata Wafanyakazi wa Uingereza, Ufaransa na Marekani Kupitia Ujamaa

Kwanza kabisa ni Ujamaa wa nchi zinazotawala, ambao unaunga mkono kuwapa taratibu haki zaidi maskini wa nchi zao na kuipa serikali mamlaka zaidi juu ya mali ya nchi. Mwendeleo huu unaendelea katika Uingereza, Ufaransa na Marekani, na lengo lake ni kuwapa wafanyakazi wa kawaida madaraka zaidi katika serikali na kuwapa maskini haki zaidi na biashara ya nchi

ikuzwe kiasi hiki ya kwamba tatizo la umaskini wa maskini litatuliwe kabisa. Kwa kuwa katika nchi hizo, Mwendeleo huo upo tangu muda mrefu, kwa hiyo, bila shaka, maskini wa nchi hizo wamepata faida kiasi hiki kwamba tajiri wa nchi yetu anakuwa sawa na maskini wa Uingereza. Hapa kwetu mtu akipata mshahara Rupia mia tatu, basi anajifahamu kuwa ni tajiri sana. Nchini kwetu cheo kikubwa ni cha Disii au cha Jaji, na jaji mdogo na Disii hupewa mshahara wa Rupia mia mbili na hamsini tu, ambao ni mshahara wa mfanayakazi wa Uingereza; na huko Marekani mishahara ni mikubwa zaidi. Huko mfanyakazi wa kawaida wakati mwingine anapata dola 100 — 200 kwa mwezi ambazo ni sawa na Rupia kama mia tano au mia saba, lakini huitwa tu mfanyakazi wa kawaida. Ilmuradi, kwanza wameinua kiwango cha maisha yao na la pili wameweka kanuni hii kwamba biashara ya nchi na hali yake ya kiuchumi ikuzwe sana, na kwa njia hiyo mali ya nchi itaongezeka, na kama mali ya nchi ikiongezeka basi maskini pia watapata maendeleo. Haya ni matokeo ya Mwendeleo wa Ujamaa wa Uingereza, Ufaransa na Marekani. Lakini Mwendeleo huu unawasaidia zaidi maskini wa nchi yao. Hao wanapenda kuzifarifji nchi nyingine pia, lakini hawapendi kuwa athari na mamlaka yaliyo nayo mataifa yao katika nchi zingien yafutike. Likija suala la India, bila shaka watajaribu kuifariji, lakini kila wanapotaka kuipatia India chochote, hawataki madraka yao

yaathirike vibaya. Kana kwamba wanawatendea watu wa India kama alishwavyo chakula kizuri mnyama anayefugwa. Mfugaji huwa anamlisha mnyama wake chakula kizuri, lakini hajihasirishi mlo wake. Vivyo hivyo watu hao kila wanapotaka kuipa India haki yoyote, papo hapo wanapenda pia kwamba ubeberu wao usipate kuathirika vibaya. Wanafikiri kuwa leo mfanyakazi wetu anapata Rupia mia nne kwa mwezi, ikiwa kesho akianza kupata mia mbili, basi hali yetu itakuwa kama hali ya maskini wa India na Afughanistan. Kuna hasara mbili kubwa za mwendeleo.

## Hasara Mbili Kubwa za Mwendeleo wa Ujamaa: Ukosefu wa Huruma kwa Nchi Zingine na Kutoijali Dini

Kwanza kabisa mpango huu hauna huruma kwa dunia nzima, bali unayaona tu masilahi ya nchi yao, kana kwamba mpango huo unashirikiana na ubeberu ndani kwa ndani na unauunga mkono umataifa ili mataifa mengine yasisonge mbele. Dosari ya pili ya mpango huo ni kuizingatia dunia tu na kuipuuza dini. Yaani, hata kama mpango huo uondoe kasoro ya awali, kwa kuingiza kanuni ya kuihurumia dunia nzima ndani ya nidhamu yake, hata hivyo dini haitakuwa na nafasi yoyote, ilhali mahitaji ya kidini ni muhimu zaidi kuliko mahitaji ya kimwili. Watu hao si maadui wa dini, lakini pia hawana huruma yoyote kwa ajili ya dini, na kama

hawana huruma kwa ajili ya dini basi watachangia nini kwa ajili ya dini?

Mpango wa pili ulioanzishwa kwa lengo la kuyatibu maradhi haya upo nchini Urusi, ambao unadai ya kuwa bidii ya mtu binafsi ifutwe kabisa na mali yote imilikiwe na serikali. Wafanyao kazi kwa mikono wapewe posho sawa na hali yao. Lakini wale wanaoshughulikia tu mambo ya kielimu na kazi ya dini, wachukuliwe kama sehemu isiofaa ya jamii na wasipewe msaada wowote na serikali. Na mali inayobakia baada ya kuwalipa wafanyakazi iwe mikononi mwa serikali na serikali iamue wafanye kazi gani na wapi. Na wazazi wasiwe na hiari ya kuwapa watoto wao mafundisho ya kidini, na mfumo huo uenezwe duniani kote mpaka mataifa yote ya dunia yaingie ndani ya mfumo huu. Ingawaje hao wanauunga mkono utawala wa watu, lakini mwanzoni hawako tayari kuwapa watu utawala kwa muda mrefu. Mfumo huu unajulikana kama Ubolsheviki, na Ukamunisti katika Urusi na Ukomunisti katika nchi zingine. Dosari za msingi za mfumo huu ni hizi:

## Dosari ya Kwanza: Dosari Saba za Msingi za Ukomunisti

Dosari yake ya kwanza ni hii kwamba njia ya jitihada ya kila mtu binafsi imefungwa kabisa. Hii ni dosari ya hatari katika mfumo huu, ambayo ingawaje haihisiki kwa sasa, lakini lazima siku za usoni itakuja kuhisika katika muda fulani. Mwenyezi Mungu Ameliweka jambo

hili katika tabia ya asili ya mtu kwamba mtu hufanya kwa shauku ile kazi inayompatia faida yeye au kuwanufaisha watu wengine kumpitia yeye. Lakini haoneshi shauku kubwa katika kazi inayomfaidisha yeye au watu wengine kwa kumpitia mtu mwingine. Ikiwa mtamfanya mtu aendelee tu kufanya kazi hata kama matokeo ya kazi hii yaonekane au hapana, basi ni lazima yeye atakosa raghba ndani yake, kwani raghba hupatikana kwa kuona matokeo. Sasa mtu anayeshughulika kupata elimu anafikiri kwamba nikipata fadhila ya masomo ya uzamili au nikishika nafasi ya kwanza katika mtihani wa Chuo Kikuu, basi nitapata ajira nzuri. Au mwingine anawaza atakuwa Luteni jeshini, mwingine anafikiria kuwa E.A.C., mwingine anafikiri kuwa atakuwa mfanyabiashara mkubwa sana na hivyo nitachuma mali nyingi na kuwahudumia vuzuri wazazi wangu na ahali zangu, na kwa sababu hiyo yeye huonesha shauku na bidii katika masomo yake.

Lakini kama motisha hii haipo, na serikali iamue kuwa wanafunzi wote wanaoendelea kusoma, kila mmoja wao atapata Rupia kumi na tano aliyemaliza na aliyeshindwa kumaliza shule ya msingi pia atapata Rupia kumi na tano, mwanafunzi aliyepata shahada ya uzamili pia atapewa Rupia kumi na tano, na mwanafunzi aliyemaliza kidato cha pili naye pia atapewa Rupia kumi na tano tu, basi matokeo yake ya lazima ni haya ya

kwamba juhudi, shauku na jadhba, zote zitakwisha. Na mtu wa kawaida atasema kuwa ana haja gani ya kufanya kazi kwa bidii, rafiki yangu anaenda sinema kuona filamu kila siku kwa nini mimi nisione, na kwa nini nijitahidi kupata shahada ya uzamili, na kwa nini nisiishie kwenye kidato cha nne tu, maana mwishowe nitapata rupia kumi na tano tu kwa hiyo kuna haja gani ya kusoma zaidi. Ni wachache sana watakaokuwa na raghba ya kupata elimu, na hawatacha masomo hata kama wakiadhibiwa ili kuacha. Wengi watakuwepo ambao katika mazingira haya hawatakuwa na shauku na raghba ya kusoma. Vivyo hivyo wataalamu wa fani mbalimbali wataacha kujielimisha zaidi na matokeo yake yatakuwa ni kwamba akili ya mwanadamu itaanza kuporomoka na vile vipawa maalumu vinavyoendelea kizazi hata kizazi vitatoweka.

Msidhani kwamba sifa za baba haziwezi kurithiwa na mtoto, kwani uzoefu unaonyesha kwamba wale walio mahiri katika hisabati, kwa kawaida, miongoni mwa watoto wao wanazaliwa walio mahiri wa hisabati. Halikadhalika yule aliye mahiri wa fani fulani, fani hiyo kwa kawaida hurithiwa na watoto wake. Kutokana na sayansi pia imethibitika kwamba chembechembe za khulka za mtu ziwe nzuri au mbaya, zinahamia katika kizazi chake. Jinsi zinavyokuwa khulka za mtu, ndivyo chembechembe za aina hiyo zinavyohamia katika vizazi

vyake; ushujaa, ukweli, utakaso, raghba ya elimu au khulka zingien kama hizo, zinahamia katika kizazi hata kizazi. Sifa kama hizi hudhihirika katika kizazi cha pili au cha nne, na wakati mwingine katika kizazi cha nane au cha kumi, ilhali sifa hizo zilikuwa zikipatikana kwa babu yake fulani au kwa mababu zake. Wapanjabi wanaiita *Tukhm Tathir* — athari ya mbegu — kwa sababu hiyo. Hakuna shaka ya kwamba marafiki pia wanaathiri sana, lakini huu pia ni ukweli ya kwamba baadhi ya khulka na sifa zinahamia kizazi hata kizazi lakini kitu hicho kitapungua sana katika mataifa ambayo yataathirika na mfumo wa Bolsheviki, kwani kwa ajili ya kupata maendeleo, sifa ya kuwa na fikira pana na motisha fulani lazima ipatikane, na katika mfumo huo motisha hii imedhoofishwa sana.

## Kasoro ya Pili ya Ukomunisti: Utumiaji wa Nguvu na Matokeo yake

Kasoro ya pili iliyomo ndani ya mpango huu ni kwa kutumia nguvu umeanzishwa ufisadi. Kama waanzilishi wa mpango huo wangewazoesha polepole matajri na kuchukua mali yao ingekuwa si vibaya. Lakini waliwapora mali yao mara moja, na waliokuwa na watumishi wengi saa zote wakanyimwa raha hiyo. Au kwa maneno mengine waliozoea kuishi katika majumba ya fahari, wakapelekwa katika nyumba za matopasi. Matokeo ya lazima ya mabadiliko kama haya huwa fujo kuzuka kwa sababu kabla ya kila mabadiiko ni muhimu

kuandaa mazingira yanayofaa. Mtunzaji mzuri wa bustani anapoung'oa mti fulani, huung'oa katika mazingira yafaayo na kuupanda sehemu nyingine kwa mazingira hayo hayo yanayofaa. Isipozingatiwa hiyo, basi mti huo hautaweza asilani kutoa matunda. Kwa kuwa kanuni hii haikuzingatiwa ndani ya mfumo huo, matokeo yakawa kwamba matajiri wa zamani wakakimbilia nchi zingine na kuanza kuwachochea wenyeji wa huko dhidi ya Urusi, wakati mwingine wakaichochea Marekani, wakati mwingine Uingereza na wakati mwingine Ufaransa, ili wazichochee nchi hizi ziipinge Urusi. Na hivyo, kama wameangamia, basi na Urusi pia iangamie.

## Kasoro ya Tatu ya Ukomunisti: Kupinga Dini na Matokeo yake

Kasoro ya tatu: Kwa kuzipinga dini, wakaifanya dunia nzima ya kidini kuwa wapinzani wao. Hili ni jambo la lazima kwamba wale watu waipendao dini, hao hawatakuwa kamwe wenye kuuhami na kuusaidia mfumo huo.

## Kasoro ya Nne ya Ukomunisti: Uanzishwaji wa Udikteta Nchini

Kasoro ya nne: Wakaifungua njia kwa udikteta. Bila shaka watu hawa, kikanuni, ni wenye kuuhami utawala wa watu. Lakini kama vile nilivyokwishasema sasa hivi, wao hawako tayari kuyakabidhi mwanzoni mamlaka

haya kwa watu. Bali husema kwamba mwanzoni udikteta ni jambo la lazima. Lakini haukuwekewa kikomo chake. Baada ya Lenin, Stalin[4] akawa dikteta, baada ya Stalin atakuwa Molotov,[5] kisha itakuja zamu ya Tov mwingine. Na kwa hivyo mfumo huu, kwa vitendo, ni wenye kufungua njia ya udikteta.

## Kasoro ya Tano ya Ukomunisti: Kizuizi Kwenye Njia ya Elimu

Kasoro ya tano: Matokeo ya lazima ya mfumo huo ni kuzalika kizuizi kwenye njia ya elimu. Kwa sababu hii pia kwamba wakati kila mtu apatapo rupia kumi na tano au ishirini, basi moyoni mwake haiwezi kuwa shauku ya kupata maendeleo ya kielimu. Yeye hufahamu kwamba hata kama nipate elimu ndogo au kubwa, nitapata malipo yangu sawa tu na mahitaji yangu. Sasa kwa nini nipate elimu zaidi? Na kwa sababu hii pia kwamba kwa ajili ya kupata maendeleo kiakili na kielimu, ni muhimu kwenda katika nchi zingine na kujionea hali za huko. Na historia inatuambia kwamba kaumu zipatazo maendeleo ni zile tu ambazo watu wake wanatembelea kwa wingi nchi zingine na kupata kutoka huko habari zenye manufaa. Kama watu wachache makhsus tu ndio waende kutembelea nchi nyinginezo wao pia hawawezi kupata habari zile wanazoweza kuzipata watu wa nchi mbalimbali na wa kaumu mbalimbali waendao katika nchi za nje. Kwa sababu Allah Ameweka ndani ya

ubongo wa kila mtu vipawa vya aina mbalimbali. Katika jambo fulani akili ya Mchina inafanya kazi vizuri, katika jambo lingine akili ya Mjapani yafanya kazi vizuri katika jambo fulani akili ya Mwirani yafanya kazi vizuri katika jambo fulani akili ya Mfaransa yafanya kazi vizuri na katika jambo fulani akili ya Mhindi yafanya kazi vizuri. Melimeli ya Dhaka ilikuwa maarufu sana iliyokuwa ikitengenezwa na wafumaji wa hapo. Waingereza waliunda mashine kubwa kubwa na walitengeneza nguo nzuri nzuri, lakini hadi sasa hawajaweza kutengeneza melimeli za Dhaka. Halikadhalika Wamisri walikuwa mashuhuri sana kutia maiti mumiani. Sasa kidhahiri Waingereza na Wafaransa wameendelea sana kielimu, lakini juu ya kujaribu kwa bidii zote, hadi sasa hawajaweza kutengeneza dawa walizokuwa wakitengeneza Wamisri. Mimi mwenyewe nimeziona maiti zilizotiwa mumiani. Zinaonekana kana kwamba zimekata roho sasa hivi, ilhali miaka maelfu imeshapita tangu wafe, kiasi hiki kwamba hata ulaini wa miili yao huonekana kwa uwazi. Kinyume chake, dawa ya kuhifadhi maiti inayotumika sasa huharibika baada ya muda mfupi tu.

Sasa tazameni, huu ulikuwa ni uvumbuzi mmoja wa akili ya Wamisri ambao hadi sasa watu hawajaweza kuufahamu. Kadhalika huko Delhi kulikuwa na hamamu fulani ambayo kuhusiana nayo inasemekana

kwamba chini yake ilikuwa inaweka taa ya udongo uliookwa, ndani yake mna mafuta na utambi, na kwa sababu hiyo saa zote majimoto yalikuwepo katika hamamu hiyo. Waingereza walioitwala Delhi wakasema kwamba twataka kuibomoa na kuona hamanu hii inakuwaje na majimoto kwa taa moja. Basi, wakaivunja, lakini hawakuweza tena kuirejesha kama ilivyokuwa. Hivyo, akili tofauti zina raghba tofauti kwa kazi mbalimbali. Wanapokutana pamoja basi akili ya mmoja inapata mwanga toka kwenye akili ya mwingine, na kwa njia hii akili na elimu huendelea kuzidi. Tunapoketi na mkulima na kuongea naye, hapo tunafahamu sifa zake makhsus. Tunapokaa na seremala, twafamu kuwa kuna sifa gani makhsus za seremala huyo, na kwa kukutana nao na kuongea nao mambo mapya kadha twayajua na roho yetu pia inahuika. Vivyo hivyo tuendapo Kashmiri au UP (Uttar Pradesh), twapata elimu mpya. Ndiyo sababu Allah Amesema ndani ya Kurani Tukufu *Siiruu fil Ardhi,*[6] yaani kama mkipata uwezo, basi itembeleeni ardhi ili elimu yenu iongezeke na yapatikane maendeleo ya kiakili na kielimu. Mtu atakapoenda Uarabuni, basi kwa upande mmoja atapata ladha ya kusafiri baharini na kwa upande mwingine ataziona katika safari hii nchi za Iran, Iraq na nchi zingine nyingi, na kwa njia hii atapata elimu nyingi zenye faida. Lakini kama watu wote wa nchi wapate kiasi kile kile cha fedha, wapate chumvi ile ile, pilipili ile ile, na masala basi watawezaje kwenda

kuzitembelea nchi zingine. Zamani ilikuwa hivi kwabma walikuwepo matajiri na pia masikini. Matajiri walikuwa wakienda kutalii nchi za nje, lakini baada ya mfumo huo, ambapo wote wakawekwa kwenye kiwango kimoja, na hali yao ya kifedha kuwa hivi kwamba watapata matumizi kwa ajili tu ya kujikimu, sasa watawezaje kutalii nchi za nje? Na kwa kuwa hawatatalii, basi mlango huu wa maendeleo ya elimu utakuwa umefungwa kwa ajili yao, ilhali kwa ajili ya maendeleo ni lazima yawepo makundi fulani ya watu ambao wautumie wakati wao wa fursa kwenda nchi za nje, wazitembelee na mawazo mema ya huko wayaeneze katika nchi zao.

Wanaweza kusema kwamba wafanyakazi wa serikali wanaweza kufanya safari za aina hiyo, lakini si lazima kwamba watu wa serikali walio hodari katika siasa wawe pia hodari katika kutalii. Kama watu wa kawaida waende kuzitembelea nchi za nje, basi wakili ataleta kitu sawa na akili yake, daktari ataleta kitu sawa na akili yake, mhandisi ataleta kitu sawa na akili yake, mchoraji ataleta kitu sawa na akili yake, mshairi ataleta jambo kulingana na akili yake. Vivyo hivyo kiongozi wa kidini akienda, yeye ataleta jambo kulingana na akili yake. Lakini bongo za kisiasa za ofisi ya balozi zitaleta nini? Wao watakuwa wamejikita tu kwenye mazingira yao na kwa sababu hii mtazamo wao pia utakuwa finyu mno. Kama wataleta,

basi wataleta vitu vichache tu, na hivyo kwa njia yao nchi haiwezi kupata faida inayoweza kupatikana kwa utalii wa wtu wa kawaida. Kama waseme kwamba serikali kwa gharama zake inaweza kuwatuma watu wa kawaida kwa makusudio haya, basi suala ni hili kwamba kwa njia hii mfarakano utazalika tena na utatokea kanuni ile ya ukosefu wa usawa ambayo mfumo huo ulianzishwa kwa ajili ya kuivunja, na swali hili litazalika kwamba je moyo wa Zaid wapenda kwenda Amerika, na moyo wa Bakari haupendi? Hapo tena uadilifu hautakuwepo na hivyo chochote kitakachofanywa, kitakuwa kimefanywa kinyume na roho ya asili ya mfumo huu.

## Kasoro ya Sita ya Ukomunisti: Mfarakano wa Watu

Kasoro ya sita: Matokeo ya mfumo huo ni kaumu kugawanyika vipande vipande na matajiri wataanza kuuawa.

## Kasoro ya Saba ya Ukomunisti

Kasoro ya saba: Ndani ya kanuni ya Ubolsheviki kuna kosa jingine hili kwamba kudhoofika kwake kutakuwa ni hatari mno. Katika mifumo mingine, mfalme mmoja anapokufa, mfalme mwingine anatawala mahali pake. Bunge moja linapovunjika, bunge lingine linaibuka. Lakini kama ukidhoofika mfumo wa Ubolsheviki, basi huo utaangamia mara moja na mahali pake Tzar tu

atakuja. Haitakuja serikali nyingine yoyote, kwani ndani yake hamna nafasi yoyote ya unaibu kama inavyokuwa ndani ya mifumo mingine. Sababu ni hii kwamba upaji umefutiliwa mbali. Na kwa kufutwa upaji, akili ikarudishwa nyuma, basi matokeo yatakuwa ni kwamba maanguko yatakapotokea, wakati huo hakutakuwa na yeyote mwenye akili nzuri awezaye kuuondoa maanguko haya. Hivyo, mfumo huo utakapoanguka, basi utaanguka kikamilifu, kama ilivyotokea huko Ufaransa kwamba waasi walipodhoofika, hapo mtu aliyekuwa dikteta kama Napoleon akachukua mamlaka kamili mahali pao. Miongoni mwa umma, yeyote aupendaye ujamhuri hakuweza kuchukua nafasi hii.

## Ujamaa wa Kitaifa na Kasoro zake

Mfumo wa tatu ni wa Ujamaa wa Kitaifa. Makusudio ya mfumo huu ni kwamba masikini ni lazima wapewe angalau haki kadha, lakini upaji wa mtu binafsi usipondwe. Na kwa kuwa wenye kuuhami mfumo huu wanafahamu kuwa upaji wa mtu unahusikana na kaumu zao tu, kwa hiyo sera yao ni kwamba wainuliwe maskini wa Ujerumani, Roma na Uhispania, lakini mataifa mengine yakandamizwe na mali zao zichukuliwe na kuwatajirisha Wajerumani, na Wahispania. Sasa Japani pia imekuja na kuungana na mfumo huu wa mwisho. Kasoro za kimsingi za mfumo huu ni hizi:

## Kasoro ya Kwanza

Kwanza mfumo huu unayapa mataifa machache tu fursa ya kunufaika. Hautaki ustawi wa dunia nzima.

## Kasoro ya Pili

Pili, ndani ya mfumo huu pia hakuna utulivu wa kiroho, yaani haikuwekwa njia yoyote kwa ajili ya dini, bali huu unaweka vikwazo vya aina nyingi katika njia ya dini. Ni dini gani ile ambayo mwanadamu anaweza kuiwekea vikwazo! Dini inateremshwa kutoka kwa Mwenyezi Mungu na ni Yeye Mwenyewe Aiwekeaye mipaka.

## Kasoro ya Tatu

Tatu, ndani ya mfumo huu, ubinafsi umehamasishwa kiasi ya kwamba sauti ya pamoja ya nchi nzima imekomeshwa kabisa mbele yake, ilhali yaweza kuwa mara nyingi sana kwamba akili ya mtu fulani, hata iwe nzuri kiasi gani, jambo liingialo akilini mwake linaweza kuwa si bora kuliko rai ya wengine, hata kama si wenye akili nyingi sana. Ndio sababu sheria yetu imesema kwamba kuwe na Khalifa mmoja wa Waislamu ambaye ashauriane na Waislamu kaitka mambo ya muhimu na kadiri iwezekanavyo aukubali ushauri wao. Naam, kama kuna hitilafu muhimu kiasi hiki kwamba yeye anafahamu kwamba kama wakati huu nikifuata rai ya watu wengi basi nchi na kaumi itapata hasara, basi wakati huo anaweza kutoa uamuzi ulio kinyume pia na

ushauri wao. Kwa vyovyote vile, sawa na njia ya Kiislamu, mambo yote hayo mawili yanazingatiwa. Upande mmoja huchukuliwa rai ya watu, na upande mwingine mwenye akili ile iliyo bora zaidi anapewa hiari ya kupima, na ule ushauri ulio na madhara kwa nchi na kaumu asiukubali, ushauri mwingine aukubali. Lakini ndani ya mfumo wa Ujamaa wa Kitaifa mtu mmoja amepewa umuhimu kupita kiasi, ilhali wakati mwingine huwa hivi kwamba kijiji chote kinakuwa kwenye makosa na mkulima mmoja mzee anasema jambo lililo sahihi. Na wakati mwingine mzee huwa amegota kwenye makosa na vijana wanakuwa wanasema jambo lililo sahihi. Kwa vyovyote vile hawa wote wameelekea uchechefu au wamepita kiasi.

## Vita Iliyopo na Matokeo yake

Vita inayoendelea ni matokeo ya mvutano huu huu. Warusi wanataka kwamba nadharia yao ndio istawi, na hali zilizozalika huko Urusi zienee katika nchi zote zilizobakia. Na Wajamaa wa Uingereza, Ufaransa na Marekani wanasema kwamba mali tulikwishanyakua, ziwe tu mikononi mwetu, zisiende mikononi mwa Wajerumani, Waroma Wajapani, na Wahispania. Vita ya Kwanza ilikuwa ni kati ya Wajamaa na Wajamaa wa Kitaifa. Wajamaa walipigana vita ili kusitokee tofauti yoyote katika madaraka yao ya sasa. Na Wajamaa wa Kitaifa walishambulia ili waiteke mali ya wenye

madaraka na kuileta katika nchi yao. Mfumo wa tatu ulikuwa ni wa Ubolsheviki. Wakati huo, kwa ujanja, Wajerumani walifanya mapatano na Urusi na kuidanganya kwamba kama madola haya yakianguka, basi Wabolsheviki pia watakuwa na hisa katika uporaji huu. Wabolsheviki wakadanganyika na kufanya mapatano na Wajamaa wa Kitaifa. Lakini nguvu ya ufaransa iliposambaratika na huku nchi za mashariki zikaanza kushindwa, basi Hitler, kutokana na mahitaji ya kivita na pia kwa kufikiria kwamba Uingereza haiwezi kwa wakati huu kushambuliwa, na kama maaskari wakikaa tu hivi basi watafadhaika, na pia kwa fikara hii kwamba sasa hakuna yeyote wa kukabiliana nasi, basi na tuufuate Ubolsheviki pia, akaishambulia Urusi. Matokeo yakawa kwamba Ubolsheviki ukaungana na serikali zenye madaraka zilizoungana. Na sasa kukawa na mifumo miwili upande mmoja na mfumo mmoja upande mwingine. Kama Wajamaa wa Kitaifa wakishinda, basi masikini wa Ujerumani, Italia, Uhispania na Japani ni lazima watafaidika, lakini hali ya maskini wa mataifa mengine itakuwa mbaya zaidi kuliko ilivyokuwa hapo awali. Yaani, umaskini utafutika katika nchi nne, na katika mamia ya nchi zingine utaimarika zaidi kuliko ulivyokuwa hapo awali. Na kama kundi lingine likishinda, basi sehemu fulani ya dunia itapata uhuru wa kisiasa kiasi fulani chini ya athari ya Ujamaa. India pia itazipata haki kadha. Lakini kuhusiana na suala

la uhuru wa kibiashara na kiuchumi, juhudi za muda mrefu zitalazimika kufanywa na nchi hizo. Kwani, kizuizi kilichopo kupata uhuru huu hakisababishwi tu na jumuiya zenye misimamo mikali au zenye misimamo ya wastani, bali kutokana na hofu ya kuporomoka kwa kiwango cha maisha, jumuiya za kiujamaa pia zitakuwa zikipambana na nchi zingine. Lakini kuhusiana na uwiano, watu hawa wakishinda, hali ya nchi zingine kwa yakini zitakuwa bora zaidi kulinganishwa na matokeo ya ushindi wa Wajamaa wa Kitaifa.

## Faida ya India Kutokana na Ushindi wa Waingereza katika Vita ya Sasa

Rai yangu kuhusiana na jambo hili na ambayo nimeshaieleza hapo kabla pia mara nyingi, ni hii kwamba kama Ujerumani itashinda, hali ya nchi yetu itakuwa mbaya zaidi kuliko ilivyokuwa hapo awali. Na kama Waingereza washinde, basi hali ya nchi yetu, kwa yakini, itakuwa bora kuliko ilivyokuwa hapo awali. Kwa kawaida hudhaniwa ndani ya nchi yetu kwamba kama mtu analazimika kuwa mtumwa, basi kuna tofauti gani akiwa mtumwa wa huyu au wa yule. Lakini jambo hili si sahihi na kuna dalili kubwa ya kulisaidia, ambayo nimeshaieleza pia hapo awali, nayo ni hii kwamba haya mataifa yaliyoungana katika vita, kutokana na kupata madaraka ya kiuchumi kwa muda mrefu, kwa sasa yameshaipoteza nguvu ile ya kusonga mbele iwezayo

kupatikana ndani ya mataifa mapya yanayosonga mbele. Basi, mataifa haya mapya yanayochipukia yatazitendea nchi zingine kama Jat (mtu wa kabila la Rajput) mwenye njaa, na serikali zenye madaraka kama mfanyabiashara mzee. Yule mfanyabiashara aliyekwishachuma fedha nyingi sana, yeye pia anakuwa bahili, naye pia anataka mali yake iongezeke, lakini anafurahia hali yake pia kuwa ibaki iwe hivyo hivyo. Na wakati mwingine wazo hili lamjia moyoni kwamba mimi nimeshachuma sana, sasa yanipasa nichukue kiinua mgongo cha kazi yangu. Hivyo serikali hizi zenye mamlaka hazina jadhba ile iwezayo kuwepo ndani ya serikali mpya. Tazameni, basi, Uingereza iko wapi lakini Waingereza wanatawala hadi Uchina. Halikadhalika madaraka ya kiuchumi ya Marekani yameenea dunia nzima na sasa tumbo lao limejaa kiasi hiki kwamba inawawia vigumu hata kutembea. Na yule aliyeshiba kiasi hiki huwa hafanyi dhuluma au hufanya kidogo. Mfano wake, fahamuni, ni kama wa yule mtu ambaye tumbo lake limejaa, hata kama muweke pilau mbele yake, basi atakula matonge mawili matatu tu na atakoma. Lakini kama sahani hiyo hiyo ya pilau ukimwekea mwenye njaa, basi yeye hatakula tu pilau hiyo, bali yawezekana akala hata chakula chako pia. Kwa sasa Wajerumani na Waroma na Wahispania wana njaa, kwa hiyo kama utawala wao ukija, basi wao kwa muda fulani watajitahidi kuendelea kupora mali, kama vile Waingereza walipoiteka India,

basi wao nao pia wakaitawala sana hali ya kiuchumi ya India. Utashi huu huu utakuwa ndio utakuwa wa Wajerumani na Waroma. Hao nao wataseam kwamba tumeyateka machimbo haya ya madaini, hivyo nasi pia tufaidike na mafuta ya hapa na dhahabu na vitu vingine. Na wataendelea kufanya hivyo kwa muda wa miaka mia hadi mia na hamsini. Lakini mfano wa Waingereza ni kama mfano wa mfanyabiashara anayezeeka. Bila shaka ndani ya tabia yake kuna tamaa ya kuongeza mali, lakini wakati mwingine anajiwa na wazo hili kwamba nimeshachuma mali nyingine, sasa yanipasa nichukue tu kiinua mgongo. Vivyo hivyo hata ndani ya mioyo ya mataifa hayo wakati mwingine laingia wazo la kutaka zaidi lakini wakati mwingine yajiwa pia na wazo hili kwamba sisi tumeshachuma sana, sasa yapaswa tukinai. Halikadhalika kama wakati fulani linazalika ndani mwao wazo la kudhulumu, wakati mwingine laja pia wazo la huruma. Wale watu ambao hali ya akili yao ni namna hii, utulivu zaidi hupatikana kutoka kwao, kwa sababu wao wanakuwa wameshachoka baada ya kutawala.

Pili, mataifa haya hayapendi kuingilia mambo ya dini. Hawapendi hata kushinikiza kwa siri katika masula ya dini isipokuwa kwa haja fulani ya kisiasa au ya kiuchumi. Na kama kuna Mungu, na Mitume huja duniani kutoka Kwake, na kama kuyatekeleza mafundisho yao ni muhimu kwa ajili ya kuyaboresha maisah yetu ya

Akhera, basi ingawa miendendo ya mataifa hayo sio yenye uadilifu kamili, bali kwa kiwango fulani ni yenye kujipendelea, hata hivyo kila mpenda dini ataupenda zaidi ushindi wa mataifa hayo kuliko ushindi wa Wajamaa wa Kitaifa.

## Ushindi wa Ubolsheviki Utokanao na Ushindi wa Waingereza na Matokeo yake

Lakini ikumbukwe pia kwamba katika hali iliyopo sasa, pamoja na ushindi wa mataifa haya, ushindi wa Ubolsheviki pia ni jambo la lazima, na Ubolsheviki ni adui mkubwa wa dini kuliko ule wa Wajamaa wa Kitaifa. Hivyo, ingawa kwa yakini, kutokana na ushindi wao, dunia itasalimika na hatari za Ujamaa wa Kitaifa, lakini mvutano mpya utaanza kati ya wenye dini na wasio na dini.

## Mipango ya Dini Mbalimbali kwa Ajili ya Kuboresha Hali za Masikini

Hadi sasa nimeongelea kuhusiana na mifumo ya kidunia. Sasa naongelea kuhusiana na mifumo mbalimbali inayotolewa na watu wa dini mbalimbali kwa kukamilisha nidhamu mpya ya dunia. Miongoni mwa dini hizo, dini zilizo kubwa zaidi ni hizi, Uhindu, Ukristo, Uyahudi na Islam. Wakati huu kama wachunguzwe wafuasi wa dini zote hizo, mfuasi wa kila dini atasikika akidai kwamba dini iliyo bora kuliko zote ni ile anayoifuata na ni mafundisho yake tu yawezayo

kuondoa shida na maumivu ya dunia. Wahindu wanasema kwamba siku moja sisi tutasimika bendera ya Om — ya Kihindu — huko Makka (Mungu Apishe mbali). Wayahudi wanasema kwamba mafundisho ya Kiyahudi ndiyo bora kuliko yote. Wakristo wanasema kwamba aliyosema Yesu Masihi ndiyo yanayopaswa kufuatwa. Kukabiliana nao, Waislamu pia wanayo jadhba, nao wanadai na wanadai, kwa usahihi, kwamba Islam tu yatoa tiba ya kufaulu kuondoa machungu na maumivu yote. Kwa vyovyote vile dini zilizo kubwa ndizo hizi, Uhindu, Uyahudi, Ukristo na Islam. Mimi hivi sasa sielekei kwenye sala na saumu, bali ninabainisha madhumuni haya kwamba dunia inakufa kwa njaa na dunia imeanzisha baadhi ya mifumo kwa kukabiliana na hali hiyo. Badala ya mifumo hii ya kidunia, dini zinatoa nadharia gani kuhusiana na hali hiyo, na ni nidhamu ipi mpya ambayo dini hizo zinataka kuistawisha duniani? Kwa kusudio hili, kwanza kabisa naieleza dini ya Kiyahudi.

## Muundo wa Nidhamu Mpya Ndani ya Uyahudi na Matokeo yake

Nidhamu inayotolewa na Uyahudi kwa ajili ya dunia ni ya kitaifa tu. Hamna jambo lolote humo la kimataifa. Kwa mfano, Uyahudi unasema kwamba Mwenyezi Mungu Anawapenda tu vizazi vya Yakubu, wengine wote waliobakia wameumbwa kwa ajili ya kuwa

watumwa wao. Kama dini hii wakati wowote ule ipate kutawale dunia, kwa yakini, sawa na fundisho hili, dhuluma zitazidi, haitapungua. Au, kwa mfano Uyahudi unasema, usimkopeshe ndugu yako kwa riba lakini waweza kumkopesha kwa riba mtu yeyote mwingine.[7] Sasa kama kukopesha kwa riba ni jambo baya, kuna sababu gani kwamba Myahudi asikopeshwe kwa riba lakini asiye Myahudi akopeshwe kwa riba? Sababu yake ni hii tu kwamba Uyahudhi ni dini ya kitaifa. Unasema wengine watozwe riba lakini nduguzo Wayahudi wasiotozwe. Basi, kama dini hii ipate kutawala duniani, kazi yake itakuwa kwamba utawatoza watu wote kodi kuzigawa kwa Wayahudi. Halikadhalika Uyahudi unatoa agizo la kutoa sadaka lakini unasema ni kwa kupewa Wayahudi tu. Sasa kama Myahudi akiwa Mfalme, basi sawa na fundisho hili, kodi zote zitakazopatikana, zote watapewa Wayahudi. Kadhalika Uyahudi hausemi kwamba usimfanye yeyote kuwa mtumwa, bali unasema kwamba usimfanye ndugu yako kuwa mtumwa wa kudumu yaani, kwanza usimfanye nduguyo kuwa mtumwa na kama ukimfanya, basi usimfanye awe mtumwa wa kudumu. Kuhusiana nayo kuna amri ndani ya dini ya Kiyahudi kwamba kila mtumwa aachiwe huru katika mwaka wa saba.[8] Kama mtu amnunue mtumwa mara tu baada ya kupita miaka saba, basi mtumwa huyo atakuwa huru baada ya miaka 6. Kama mwaka mmoja umeshapita, yeye atakuwa huru baada ya miaka 5. Miaka miwili ikishapita, atakuwa huru baada ya miaka minne.

Miaka mitatu ikishapita, atakuwa huru baada ya miaka mitatu. Na kama miaka minne imeshapita, basi atakuwa huru baada ya miaka miwili. Na kama mnamo mwaka wa sita mtu amnunue mtumwa basi mwakani yeye mwenyewe atakuwa huru;[9] yaani, Myahudi anaweza kuwa mtumwa hadi kwa miaka saba tu. Haiwezekani kumuweka yeyote kuwa mtuwa kwa muda ulio zaidi ya huu. Watu wengine wa dunia nzima hata kama wabakie kuwa watumwa maisha yao yote, Uyahudi haujali chochte juu yao. Halafu ndani ya mafundisho ya Kiyahudi kuna jambo lingine kwamba yanaamuru kuwatendea vikali watu wa mataifa mengine. Basi, ndani ya Torati imefundishwa kwamba:

> Utakaposongea karibu ya mji kwenda kupigana juu yake, ndipo utakapowapigia ukelele wa amani. Itakuwa utakapokujibu kwa amani, na kukufungulia, ndipo watu wote watakaoonekana humo watakufanyia kazi ya shokoa, na kukutumikia. Na kwamba hautaki kufanya amani nawe, lakini utafanya vita juu yako, ndipo uuhusuru; na BWANA, Mungu wako, autiapo mkononi mwako, mpige kila mume aliyemo kwa makali ya upanga; lakini wanawake na watoto, na wanyama wa miji, na vilivyo mjini vyote, navyo ni nyara zake zote, uvitwae viwe mateka kwako; nawe utakula

> nyara za adui zako alizokupa BWANA, isiyokuwa miji ya mataifa haya.[10]

Hilo ni agizo kwa ajili ya watu wa nchi zingine. Amri hiyo haihusikani na ardhi ya Kanaani iliyokuwa ardhi ya ahadi. Bali kuhusiana na Kanaani kuna hukumu hii:

> "Lakini katika miji ya matafia haya akupayo Bwana, Mungu wako, kuwa urithi, usihifadhi kuwa hai kitu chochote kipumzikacho, lakini uwaangamize kabisa ..."

(kumbukumbu la Torati 20:16-17)

Hii ni nidhamu inayotolewa na Uyahudi. Kama Uyahudi upate mamlaka, basi kila mwanaume atauawa, kila mwanamke na mtoto atafanywa kuwa mtumwa. Na sio tu wanaume wa Kikristo wanaoishi Kanaani na wanawake na watoto, bali hata farasi wa huko na punda na mbwa na paka na nyoka na mijusi, wote watauawa, kwa sababu agizo ni hili kwamba kila kitu kinachopumua kiuawe. Chini ya nidhamu hii Wayahudi pengine watapata utulivu kwa kiasi fulani, mataifa mengine yataangamia kabisa.

## Ujumbe wa Ukristo kwa Ulimwengu

Ujumbe wa Ukristo kwa dunia ni huu tu kwamba sheria ni laana.[11] Sheria inapokuwa ni laana, basi ujumbe wake wowote ule unakuwa ni laana. Ukristo unatoa tu fundisho la upendo ambalo hata wenyewe haulitekelezi. Kama kungekuwepo na yeyote mwenye kulitekeleza

fundisho lake la upendo, kwa nini leo zingepiganwa vita katika Ulaya. Baada ya kusema kuwa sheria ni laana, haiwezekani kwa Ukristo kuweka mpango wowote makhsus kwa ajili ya dunia, kwa sababu mpango wowote utakaokuwa, utakuwa ni laana, na kuutekeleza kutaongeza matatizo ya watu, hakutayapunguza. Kisha ni jambo la ajabu kwamba kwa Ukristo sheria ya Mungu, hata iwe fupi kiasi gani, inakuwa ni laana. Lakini adhabu za watu, hata kama ziwe ni kubwa kiasi gani zinakuwa ni rehema. Matokeo yake yakawa kwamba kaumu yoyote ya Kikristo inapotawala duniani, makusudio yake husemwa kuwa ni makusudio ya Ukristo. Falsafa yoyote inayoshinda, inasemwa kuwa ni falsafa ya Kikristo, na utamaduni wowote unaoshinda nao ndio utamaduni wa Kikristo. Kama Ujerumani ishinde, watasema kwamba Ujamaa wa Kikristo ndio umeshinda. Kama Uingereza ishinde, watasema kwamba Ujamaa wa Kikristo umeshinda. Kama Marekani ishinde basi watasema kwamba Ujamaa wa Kikristo ndio umeshinda. Kana kwamba Ukristo umekuwa kwa kudumu rafiki wa kila ashindaye. Na kitu chochote kile kipatacho maendeleo duniani, basi hicho husemwa kuwa ni ushindi wa utamaduni wa Kikristo. Kulikuwa na wakati kutotoa talaka ilikuwa ndio kanuni hasa ya Ukristo, na sasa hali ni hii kwamba kutoa talaka imekuwa ndio sifa hasa ya Ukristo. Dini yao ni nini? Ni — kama wasemavyo kwa Kiurdu — "pua ya nta", igeuze

upendavyo haitovunjika. Basi, Ukristo kama dini haukuweza kuweka mbele ya dunia, mpango wowote ule, wala hauwezi kuuweka wala hautaweza kuuweka.

## Sawa na Nadharia ya Kihindu, Haiwezekani Kuleta Nidhamu Mpya

Uhindu umeifunga kabisa njia ya amani kwa ajili yao wenyewe na kwa mataifa mengine, kwa kuiletea duina mafundiosho ya *Tanaasukh* na ya *Varn.* Kwani haiwezekani, chini ya mafundisho ya *Tanaasukh* kwamba nidhamu yoyote mpya istawi ambamo iondoke tofauti kati ya tajiri na maskini. Wenye kuiaimi *Tanaasukh* wanapokiri kwamba kama Mungu Amemuumba mtu fulani kuwa masikini, basi hiyo ndiyo adhabu ya matendo yake aliyoyatenda katika uwepo wake uliopita kabla ya kuzaliwa upya safari hii. Hivyo, kwa kuwepo kwa itikadi hii, yawezekanaje kufutilia mbali tofauti kati ya tajiri na maskini. Sawa na itikadi hii, kama Mungu Amemfanya mtu fulani kuwa Tzar, basi ni kwa ajili ya malipo ya matendo aliyoyatenda katika uwepo wake uliopita. Na kama Amemfanya mtu fulani kuwa maskini, basi ni kwa kumuadhibu kutokana na matendo yake. Sasa hakuna yeyote awezaye kubadili hali hii. Hivyo kwa kuwepo kwa *Tanaasukh,* Uhindu hauwezi kutoa mpango wowote mpya wa maendeleo ya dunia, kwani mpango mpya waweza kuwa ule tu utakaoibadilisha hali iliyopo na kuleta hali mpya. Na

wakati hali iliyopo ya dunia inapokuwa ni matokeo ya matendo ya uwepo uliopita, basi kwa maneno mengine itasemwa kwamba hali hii hii ndiyo iliyokadiriwa kuwepo duniani. Na hali hii hii inapokuwa imekadiriwa na Mungu kuwepo, sasa ni nguvu ya nani iwezayo kuibadili hali hii.

Pili ndani ya dini hii kuna kanuni ya *Varna*, — firka nne za Uhindu: *Barhaman, Kashatri, Vesh* na *Shudar* — ambayo sawa nayo *Shudar* hawezi kufanya kazi ya *Barhamna* na *Vesh* hawezi kufanya kazi ya *Shudar*. Halikadhalika *Kashatri* hawezi kufanya kazi ya *Vesh*. Ndiyo kusema kwamba kila mmoja ana eneo lake la utendaji wa kazi, na mtu anakuwa hawezi kuingia ndani ya eneno la utendaji kazi wa mtu mwingine. Kanuni hii ni ya aina hii kwamba sawa nayo haiwezekani asilani kufutika tofauti kati ya tajiri na maskini. Kwa sababu nidhamu mpya iwezayo kuondoa tofauti hiyo ni ile ambamo maskini na fukara pia huangaliwa. Kama kuna mtopasi yeyote au mtu duni kabisa, basi haki zake zihifadhiwe, na serikali ifanye mpango wa kumpatia kila mtu chakula na mavazi. Halikadhalika ifanye mpango wa kuwapatia mali walio maskini ili waweze kutimiza mahitaji yao. Lakini, Manu anasema:

> "Kama *Shudar* akusanye mali, basi ni faradhi kwa Raja kumpokonya mali hiyo, kwani

> *Shudar* anapokuwa mwenye mali, huwa amwudhi *Barhaman*."[12]

Sawa na kanuni hii, kama *Barhaman* au *Vesh* anazo Rupia milioni moja, na *Shudar* ajiwe na wazo kwamba nami pia nikusanye Rupia tano kwa mwezi, kwani mwakani kutakuwa na harusi ya binti yangu, fedha hizi zitatumika wakati huo, basi ni faradhi kwa Raja kumnyang'anya fedha zote hizo, kwa sababu yeye ni *Shudar*, na *Shudar* hana haki ya kukusanya fedha. Sasa, hebu, semeni kwamba sawa na kanuni hii nidhamu mpya yawezaje kuimarika na kama nidhamu hii istawi, basi chini yake hali ya maskini yawezaje kuboreshwa.

Hali kadhalika akaandika kwamba:

> "Kama *Barhaman* amekopa kwa mtu wa tabaka la chini lakini asiweze kumlipa, basi *Shudar* analazimika kutochukua fedha kutoka kwa huyo *Barhaman*. Lakini kama *Shudar* ni mwenye kulipa fedha kwa *Barhaman*, na *Shudar* huyo ni maskini, basi huyo atalazimika kufanya kazi ya kibarua kwa watu wa tabaka la juu na kulipa fedha kwa *Barhaman*."[13]

Ndiyo kusema kama *Barhaman* ndiye anayekopa na yule aliyekopesha ni wa kaumu ya tabaka la chini, hapo kama yeye hawezi kulipa deni hilo, basi mtu wa tabaka la chini analazimika kutomdai fedha zake. Katika sura hii yeye

hawezi kumshtaki *Barhaman* mahakamani na kupata fedha zake, bali katika sura hiyo aelewe kuwa suala hilo limeshaisha, na huyo *Shudar* anapaswa aondoe kabisa moyoni mwake wazo la kuzipata fedha hizo. Lakini kama *Shudar* anakopa kwa *Barhaman*, halafu asiwe na uwezo wa kulipa, basi kulingana na hukumu za Manu inakuwa ni faradhi kwake kwamba afanye kazi kama kibarua kwa wale wenye tabaka la juu na kulipa deni kwa njia hii.

Na jambo haliishii hapa, bali athari ya fundisho hili inaendelea mbele zaidi. Basi, imeandikwa kwamba kama mtu akifariki, naye ana wake wengi, basi kwa hali ya aina hii:

> "Watoto wa mke mmojawao aliye *Barhaman* wachukue sehemu tatu za mali hiyo ya urithi, na wale watokanao na mke *Kashatri* wachukue sehemu mbili za mali hiyo, na wale watokanao na mke *Vesh* wachukue sehemu moja na nusu ya mali hiyo, na watoto wa mke *Shudar* wachukue sehemu moja ya mali hiyo."[14]

Sawa na fundisho hili, kutoka katika mali za marehemu, watoto wa *Barhaman* watapata hisa tatu, watoto wa *Kashatri* watapata hisa mbili, watoto wa *Vesh* watapata hisa moja na nusu na watoto wa *Shudar* watapata hisa moja. Sasa hebu semeni chini ya nidhamu hii, wale walio duni wanawezaje kuinuka?

Kisha ameandika:

> "*Barhaman* achukue mali kutoka kwa *Shudar*, asisite kwa sababu mali aliyokusanya sio yake bali ni ya *Barhaman*."[15]

Chini ya fundisho hili, *Mabarhaman* wamerahisishiwa sana kuchukua mali, kwani wamepewa ruhusa ya kwamba wakati wowote muonapo mali kwa *Shudar*, mumpokonye hiyo mara moja na wala msifikirie kwamba upokonyaji huo ni dhambi, kwani mali ya *Shudar* si yake bali ni yenu. Wakati wowote mtakapoiona mali kwa *Shudar*, mumpokonye hiyo mara moja na kuimiliki. Hili ndilo fundisho linalotolewa na dini ya Kihindu. Na kwa kuwa ndani ya dini ya Kihindu kwa kuacha *Mabarhaman, Makashatri* na *Maveshi*, wengine wote wanafahamika kuwa ni *Mashudar,* hivyo Masharifu, Wamughali, na Mapathani n.k., wote hao, kwa Wahindu ni *Mashudar*, na kuhusiana na hao wote, *Mabarhaman* wamepewa hiari ya kuipokonya mali yao. Kama mtu yeyote achume mali na *Barhaman* ampokonye mali hiyo, basi yeye hatakuwa na haki yoyote ya kushtaki mahakamani. Na kama akishitaki mahakamani, basi sawa na fundisho hili la Manu ataambiwa: U mwongo, hiyo haikuwa ni mali yako, hiyo ilikuwa ni mali ya *Barhaman*. Ndiyo kusema kuwa mfano wake ni kama inavyosemekana kwamba mtu fulani alikuwa akipita sehemu fulani, yeye aliona kuwa watu wamembeba mtu

mmoja kitandani wakienda kumzika, na yule aliyekuwa amebebwa kitandani alikuwa akipiga mayowe kwamba niokoeni kwa ajili ya Mungu. Kwa kuona mkusanyiko wa watu, yeye naye pia akasimama na kusema kuna nini? Wakamwambia kwamba Bwana Jaji ametoa hukumu kwamba mtu huyu azikwe, kwani ameshakufa. Akasema lakini yu hai na anapiga kelele kwamba niokolewe. Wao wakasema, hata itokee nini, jaji ameshatoa hukumu hii hii kwamba mtu huyu ameshakufa na azikwe. Mtalii huyo akasema kwamba sijaelewa jambo hili. Wale wenye kulibeba 'jeneza' wakamwambia kwamba uelewe usielewe, lile alilolisema Jaji ndilo sahihi, mtu huyu anaongopa tu asemapo eti mimi sijafa. Hatimaye mtalii huyo akaenda kwa Jaji na kumwambia kwamba leo nimeona mandhari fulani na ninashangaa kwani nashindwa kuelewa kwamba wewe umesemaje kwa mtu aliye hai kuwa mfu! Jaji akamwambia kwamba u mjinga tu usiyeielewa hali ilivyo. Kama ungetumia ujuzi, hata wewe ungemfahamu kuwa mfu.  Ukweli wenyewe ni kwamba mwaka umeshapita aliponijia mwanamke fulani na akasema kuwa mume wangu alikuwa ameenda nchi za nje, sasa nimesikia kwamba yeye amekufa. Hivyo uniruhusu niolewe na mtu mwingine. Nikasema lete mashahidi. Akaniletea mashahidi wawili wenye kutegewa waliokula kiapo na kusema kwamba walimuona mume wake akifa katika nyumba ya kupokea wageni na wao wenyewe wakamzika. Hivyo mwanamke

huyu akapewa ruhusa ya kuolewa. Sasa baada ya muda fulani mtu huyu akaja na akasema kwamba mimi ni mume wa mwanamke huyu nami niko hai, nipatiwe mwanamke huyo. Mimi nikamfahamisha sana kwamba wewe huwezi kuwa mume wa mwanamke huyo, kwani huyo alishakufa na tunao mashahidi wawili. Lakini yeye akaendelea kusema, hapana mimi nipo hai. Hatimaye nikasema kwamba mimi siwezi kumwamini hayo, wapo mashahidi wawili wenye kutegemewa wanaosema kwamba mume wa mwanamke huyu alikufa mbele yao. Na kwa kuwa kutokana na maelezo ya mashahidi hao kufa kwa mume ni jambo lililoyakinika, hivyo mimi siwezi kufanya chochote minghairi ya hii kwamba kama dai lako hili ni la kweli kwamba wewe ndiwe mume wa mwanamke huyu, basi nikuzikishe kwa gharama ya serikali. Hivyo ni kwa msingi huu huu nikawatuma watu wangu waende kumzika. Hiyo ndiyo hali ya Uhindu. Mtu yeyote aliyekusanya fedha, *Barhaman* azipore na mtu huyo maskini aendapo mahakamani kushitaki, basi hakimu atasema huyu anaongopa kabisa. Yeye alikuwa hana fedha, kwani kulingana na mlango fulani na aya fulani ya hizo Manu, hizo zilikuwa ni fedha za *Barhaman* alizozichukua.

Lakini kumbukeni kwamba mimi sisemi kwua Dini hizi zilipoanza, manabii wao walitoa mafundisho haya haya yanayotolewa sasa, bali kuna baadhi ya mafundisho

yaliyokuwa ni ya muda fulani na kwa watu tu fulani ambayo yalikuwa ni sahihi kwa zama hizo lakini siyo sahihi kwa sasa. Na kuna baadhi ya mafundisho ambayo hayakutolewa asilan na manabii hao, wanayanasibisha tu kwao. Kwa vyovyote vile, kutokana na mafundisho haya, haiwezi katika zama hizi kupatikana amani wala utulivu wowote.

## Mafundisho Yasiyo na Kifani ya Kiislamu Kulinganisha na Dini Zingine na Taswira ya Nidhamu Mpya Kwa Mtazamo wa Islam

Sasa nazungumzia Uislamu na kueleza kwamba Islam inatoa tiba gani ya shida hii. Kuhusiana na tiba ya msiba huu na shida ya dunia ambayo nimeieleza katika utangulizi, Islam yasema kama ifuatavyo:

## Kuufuta Kabisa Utumwa Duniani

Kwanza, utumwa ambao uliendelea kuwepo kwa maelfu ya miaka, Islam imeuondoa na kuufutilia mbali kabisa. Nionavyo, miongoni mwa dini zote zilizopo duniani, ni Islam tu ndiyo dini ile iliyoufuta utumwa juu ya uso wa ardhi, waila katika dini zilizotangulia kulikuwa na desturi ya utumwa na hakuna dini yoyote ile iliyoifuta. Kulingana na desturi za dini ya Kiyahudi na Kihindu, utumwa ni kitengo cha dini na hakiwezi kuondolewa. Ukristo nao ni tawi la Uyahudi. Humo pia mmekuwemo na utumwa, na kama utumwa ulifutika ndani ya Ukristo, basi sababu ya kufutika

kwake sio Ukristo, bali ilikuwa ni maendeleo ya falsafa ya khulka. Yaonekana kwa uwazi kabisa katika historia ya Kanisa kwamba mara nyingi sana juhudi zilifanyika katika nchi za Kikristo ili kuufuta utumwa, lakini wapinzani wake wakubwa walikuwa ni Mapadri. Halikadhalika kwa mfumo wa kitabaka, dini ya Kihindu iliupanua utumwa kwa kiwango kikubwa sana kwa kutumia Varno, kiasi ya kwamba mtumwa wa kununuliwa alikuwa si kitu mbele ya mtumwa wa Varn — mtumwa aliyenunuliwa halingani kabisa na mtumwa wa Ki-Varn — itikadi ya kitabaka. Lakini Islam ikaufuta kabisa utumwa huu.

## Islam Imeweka Masharti Kuwa na Wafungwa wa Kivita

Naam, liko jambo fulani lililomo ndani ya Islam ambalo watu wanaliita kuwa ni utumwa, na jambo hilo ni kukamata wafungwa wa kivita. Lakini, je kuna sehemu yoyote duniani yenye desturi ya kwamba wakati mataifa mawili yapiganapo vita na wakamatane mateka wakati wa mchana halafu wafungwa wote hao waachiwe huru wakati wa jioni na kuambiwa nendeni nyumbani kwenu, kesho mrudi tena tupigane vita. Sisi twaona kwamba watu wachezapo mchezo wa mieleka wa *Kabaddi* wale wachezaji wa upande wa pili wanaowakamata huwa hawawaachii bali huwaketisha chini. Sasa yawezekanaje kwamba ipiganwe vita, halafu baada ya vita wafungwa

wote wa kivita waachiliwe. Kama haiwezekani hata kuchezwa mchezo wa *Kabaddi* pasipo kumkamata aliyeshindwa na kukalishwa chini, basi vita zawezaje kumalizika bila ya kufanya hivyo. Basi, hakuna mtumwa yeyote ndani ya Islam, bali kuna mfungwa wa kivita. Hivyo, Allah Anasema ndani ya Kurani Tukufu:

مَا كَانَ لِنَبِيٍّ اَنْ يَّكُوْنَ لَهٗٓ اَسْرٰى حَتّٰى يُثْخِنَ فِى الْاَرْضِؕ تُرِيْدُوْنَ عَرَضَ الدُّنْيَا ۖ وَاللّٰهُ يُرِيْدُ الْاٰخِرَةَؕ وَاللّٰهُ عَزِيْزٌ حَكِيْمٌ ﴿٦٨﴾ [16]

Yaani haijuzu kwa nabii yeyote kwamba aendelee tu bila sababu kuwafanya watu kuwa watumwa. Kwa maneno haya sio tu kwamba Mwenyezi Mungu Ametangaza kuwa haijuzu kwa Muhammad[sas], Mtume wa Allah, kumfanya mwanadamu yeyote kuwa mtumwa, bali lawama zote zile pia ziliondolewa na Mungu zilizokuwa zikiwarejea manabii kwa sababu ya Uyahudi, Ukristo na Uhindu. Kwani Amesema: مَا كَانَ لِنَبِيٍّ اَنْ يَّكُوْنَ لَهٗٓ اَسْرٰى Yaani haikujuzu pia hata kwa nabii yeyote yule kuwafanya tu watu kuwa watumwa. Hivyo, Krishna[as] hakufanya hivyo wala Ram Chandra[as], wala Musa[as] wala Isa[as]. Wale wasemao hivyo, wanawazulia uwongo. Naam, Amesema kwamba kitu kimoja kinaruhusiwa, nacho ni hiki حَتّٰى يُثْخِنَ فِى الْاَرْضِؕ , kutakapokuwa na umwagaji damu ardhini, basi hapo ndipo inaporuhusiwa kukamata wafungwa wa kivita. Yaani kuwe na vita, nayo iwe ni kali kiasi hiki kwamba damu imwajike sana. Taifa lilishambulie taifa

na nchi iishambulie nchi nyingine na damu nyingi sana iwe imemwagika, katika hali kama hii, hakuna shaka yoyote kwamba inaruhusiwa kukamata wafungwa wa kivita. Lakini hakuna ruhusa ya kukamata wafungwa wa kivita kwenye mapigano ya kawaida tu, kwa mfano yale mapigano ya koo au ya watu. تُرِيْدُوْنَ عَرَضَ الدُّنْيَا Enyi watu wote mnaotaka kuwafanya watu kuwa wafungwa wa kivita au kuwafanya kuwa watumwa bila ya kupignwa vita, kwa maneno mengine mnataka kuipata dunia? Kama mkifanya hivyo basi mtafahamika kuwa ni wenye kuipenda dunia, hamtakuwa wenye kumpenda Mwenyezi Mungu, وَ اللهُ يُرِيْدُ الْاٰخِرَةَ ilhali Mwenyezi Mungu Anataka muwe wenye kuipenda Akhera. وَاللهُ عَزِيْزٌ حَكِيْمٌ Na Allah ni Mshindi Mwenye Hekima. Amri zake zote huwa zenye hekima kubwa kubwa. Kama mtaendeleza utumwa, basi matokeo yatakuwa kwamba ninyi wenyewe pia mtakuwa watumwa. Historia inaeleza kwamba zile kaumu zilizokuwa na watumwa wengi, hatimaye kaumu hizo zikaitwa kuwa ni watumwa. Katika zama za Banu Abbas kulikuwa na watumwa wengi na matokeo yakawa kwamba wafalme wote wakawa ni wazao waliotokana na wajakazi. Na kwa kuwa ndani ya mtumwa kunakuwa na hisia za kitumwa, hivyo ingawa walikuwa ni huru lakini kimaana walikuwa bado watumwa.

Katika lugha ya Kiarabu, maana ya إِثْخَان ni vita kali ya kumwaga damu sana. Yaani haijuzu kuwafanya watu kuwa watumwa katika vita za kawaida, bali watumwa wanaweza kufanywa ambapo zipiganwe tu vita kubwa sana. Vita za kawaida hutokea kati ya Waingereza na Mapathani mipkani. Lakini katika vita hizi hawakamatwi watu na kufanywa wafungwa. Wfungwa wa vita hukamatwa ambapo vita inakuwa imetangazwa rasmi. Kukamata wafungwa wa aina hii kwenye mashambulio ya kawaida wakati wa usiku huwa haijuzu. Kama kaumu fulani haitapenda kuwafanya watu wake kuwa watumwa, kwa nini itawashambulia wengine? Na kama ishambulie na vita ichukue sura ya إِثْخَان فِي الْاَرْض basi hapo kukamtata wafungwa hakutafahamika kwa vyovyote kitendo cha kulaumiwa.

## Katika Mafundisho ya Islam, Vita yoyote si Halali Ila Ile ya Kujitetea

Kisha kuhusiana na vita, Islam inaagiza kwamba hakuna vita yoyote inayojuzu isipokuwa ile ya kujihami. Yaani, haijuzu kwamba uwashambulie tu wengine na kuwafanya watu kuwa watumwa. Hivyo Anasema:

أُذِنَ لِلَّذِيْنَ يُقٰتَلُوْنَ بِاَنَّهُمْ ظُلِمُوْاؕ وَ اِنَّ اللّٰهَ عَلٰى نَصْرِهِمْ لَقَدِيْرُ ۙ﴿۴۰﴾ الَّذِيْنَ اُخْرِجُوْا مِنْ
دِيَارِهِمْ بِغَيْرِ حَقٍّ اِلَّاۤ اَنْ يَّقُوْلُوْا رَبُّنَا اللّٰهُؕ وَ لَوْ لَا دَفْعُ اللّٰهِ النَّاسَ بَعْضَهُمْ بِبَعْضٍ لَّهُدِّمَتْ
صَوَامِعُ وَ بِيَعٌ وَّ صَلَوٰتٌ وَّ مَسٰجِدُ يُذْكَرُ فِيْهَا اسْمُ اللّٰهِ كَثِيْرًاؕ وَ لَيَنْصُرَنَّ اللّٰهُ مَنْ يَّنْصُرُهٗؕ

إِنَّ اللّٰهَ لَقَوِيٌّ عَزِيْزٌ ﴿٤٠﴾ اَلَّذِيْنَ اِنْ مَّكَّنّٰهُمْ فِى الْاَرْضِ اَقَامُوا الصَّلٰوةَ وَاٰتَوُا الزَّكٰوةَ وَاَمَرُوْا بِالْمَعْرُوْفِ وَنَهَوْا عَنِ الْمُنْكَرِ ؕ وَلِلّٰهِ عَاقِبَةُ الْاُمُوْرِ ﴿٤١﴾ [17]

Anasema kwamba ruhusa ya kupigana vita wamepewa tu wale ambao walianza kushambuliwa na kwa sababu walidhulumiwa. وَاِنَّ اللّٰهَ عَلٰى نَصْرِهِمْ لَقَدِيْرُ Na wameruhusiwa kwa sababu kwamba Waislamu walishambuliwa kwa kiasi ambacho Mwenyezi Mungu sasa Anataka Kudra Yake ifanye kazi duniani na Amwadhibu mdhalimu kwa dhuluma yake, na Amsaidie mwenye kudhulumiwa. Yawezekana kwamba mdhalimu awe ni mwenye nguvu na mdhulumiwa awe dhaifu. Katika hali hii kama mtu aliye dhaifu atapigana, basi badala ya kushinda ataangamia. Kuna kisa fulani mashuhuri kwamba kulikuwa na mshindani mweleka fulani akipita eneo fulani. Nyuma yake mtu mmoja mwembamba alikuwa anakwenda. Mshindani mweleka yule alikuwa amenyoa kipara na kukipaka mafua. Yule mtu dhaifu alipomuona yule mshindani mweleka katika hali ile, basi moyoni mwake ikamjia shauku ya kufanya utukutu kiasi ya kwamba akashindwa kujizuia na akampiga konzi kichwani. Mshindani mwereka yule akakasirika sana, akamuangusha chini na kumpiga mateke. Dhaifu yule akawa anapokea kipigo na huku akiendelea kusema : 'Nipige utakavyo, lakini ladha niliyoipata kwa kupiga konzi, wewe huwezi kuipata hata kama uendelee kunipiga maisha yako yote. Sasa hebu tazameni, kwa

kuwa yeye alikuwa ni dhaifu, akaliona jambo hili kuwa ni la fahari kubwa kwamba aliugusa mwili wa mtu mwenye nguvu. Hivyo yawezekana kwamba kukawepo na mtu aliye ni mdhalimu lakini ni mwenye nguvu, na mwenye kudhulumiwa asiweze kumshinda. Lakini Anasema kwamba ruhusa Tuliyoitoa, Tuliitoa kwa sababu wao walishambuliwa na kudhulumiwa na Tumetoa ruhusa kwa sababu ni faradhi Yetu kuwasaidia, nasi twalazimika kuwafanya dhaifu hao wawashinde wenye nguvu. Basi, hatukuwapa tu ruhusa ya kupigana vita, bali tumeshika nao ahadi kwamba Sisi Tutakuwa pamoja nanyi mpaka mtakapowashinda wadhalimu.

Kisha Anasema: اَلَّذِيْنَ اُخْرِجُوْا مِنْ دِيَارِهِمْ بِغَيْرِ حَقٍّ , walitolewa majumbani mwao bila ya wao kufanya kosa lolote, اِلَّآ اَنْ يَّقُوْلُوْا رَبُّنَا اللّٰهُ dhambi yao ilikuwa ni hii tu kwamba wao waliiamini Islam kuwa ni ya kweli na wakasema kwamba Allah Ndiye Mola wetu. وَلَوْلَا دَفْعُ اللّٰهِ النَّاسَ بَعْضَهُمْ بِبَعْضٍ لَّهُدِّمَتْ صَوَامِعُ وَ بِيَعٌ وَّ صَلَوٰتٌ وَّ مَسٰجِدُ يُذْكَرُ فِيْهَا اسْمُ اللّٰهِ كَثِيْرًا Anasema kwamba katika zama zijazo watatokea watu ambao watasihi kwa jina la upendo na ubinadamu kwamba kwa vyovyote vita ni kitu kibaya na haipaswi iwepo kwa vyovyote. Allah Anasema kwamba waambieni watu kama hao kwamba kama kusingekuwepo na kanuni hii ya Allah, kwamba dhuluma za baadhi ya watu zifutwe kwa njia ya wengine, basi nyumba za ibada, na maskani ya wanazuoni,

majumba ya ibada ya Wabudha na ya Wakristo na Wayahudi na misikiti, yote hayo yangeteketea na jina la Mwenyezi Mungu lisingetajwa tena humo. Kwani, kutokana na kutopigana nao dhamira za watu hawa zingebadilikaje, ambao kwa kupanua eneo la utawala wao wanataka kuitawala dini pia na kuwalazimisha watu kuwa au kutokuwa na dini sawa na matakwa yao. Watu hawa watajasiri baada ya kusikia tangazo la kukataza kabisa kupigana vita, na sio tu wataanza kuingilia mambo ya kidunia bali watazifuta pia dini za watu na kuziboмoa nyumba za ibada. وَ لَيَنْصُرَنَّ اللّٰهُ مَنْ يَّنْصُرُهٗ ؕ اِنَّ اللّٰهَ لَقَوِيٌّ عَزِيْزٌ. Anasema, yeyote atakayesimama ili kuifanye dini ya Mungu iwe huru, Mungu Atamsaidia, Naye ni Mwenye nguvu na Mwenye ushindi kamili. Kaumu ile Anayoisaidia huwa haishindwi asilan. Kisha Anasema, wale watu ambao hujitolea nafsi zao na mali zao kwa ajili ya kustawisha uhuru wa kidini, hao ni watu wa aina hii اَلَّذِيْنَ اِنْ مَّكَّنّٰهُمْ فِي الْاَرْضِ اَقَامُوا الصَّلٰوةَ وَ اٰتَوُا الزَّكٰوةَ وَ اَمَرُوْا بِالْمَعْرُوْفِ وَ نَهَوْا عَنِ الْمُنْكَرِ ؕ, Yaani kama wataitawala dunia, basi hawatawapora wengine ijapokuwa ni wenye nguvu, bali watafanya ibada ya Mwenyezi Mungu. Watawapa maskini mali. Nao wenyewe watajiepusha na mambo mabaya. Wataamuru kufanya mema na kukataza maovu.

Sasa hebu niambieni kwamba je Waislamu wanayo hiari kupigana vita za aina hii kwamba wakati wowote watakapo tu waanzishe kupigana vita na kuanza

kuwakamata makafiri kuwa wafungwa. Adui tu anaweza kuwakamatisha wafungwa wa kivita wa aina hii. Wakati ambapo kuiepuka imo ndani ya uwezo wake, kwa nini anapigana vita ya aina hii. Ama yu mwendawazimu au anastahili kuwa mfungwa. Kwa sababu alikuwa na hiari ya kutoshambulia na kutowadhulumu wengine. Asingeanzisha vita kwa ajili ya dini na angejiepusha na kuwa mtumwa.

## Kuwaachia Huru Wafungwa wa Vita Kulingana na Mafundisho ya Kiislamu

Lakini kama shambuluzi la aina hiyo litokee, na baadhi ya watu wafanywe kuwa wafungwa, basi wale watakaokuja wakiwa mateka wa vita, kwa ajili yao kuna amri hii iliyo safi na yenye maneno ya wazi kabisa kwamba:

فَإِذَا لَقِيتُمُ الَّذِينَ كَفَرُوا فَضَرْبَ الرِّقَابِ حَتَّىٰ إِذَا أَثْخَنتُمُوهُمْ فَشُدُّوا الْوَثَاقَ فَإِمَّا مَنًّا بَعْدُ وَإِمَّا فِدَاءً حَتَّىٰ تَضَعَ الْحَرْبُ أَوْزَارَهَا[18]

Yaani, kama litokee shambulizi la aina hiyo, nanyi mlazimike kupigana vita, basi Mwenyezi Mungu Anawaamuruni kwamba muwakamate mateka baadhi yao, lakini kisha muwatendee vipi? Kuhusiana na hilo Tumeweka kanuni mbili, nanyi mnalazimika kufuata mojawapo katika hizo mbili. Kanuni zenyewe ni hizi kwamba kwanza فَإِمَّا مَنًّا بَعْدُ , yaani muwafanyie hisani na kuwaachia huru mkisema nendeni tumewasameheni, au muwaachie huru wa kuchukua fidia toka kwa wafungwa

hao kuwiana na gharama ya vita. Yaani hamna budi kufuata moja kati ya sura hizo mbili: ama mtalazimika kuwafanyia hisani na kuwaachia huru au mtalazimika kuwaachia huru baada ya kuchukua fidia kuwiana na gharama za vita toka kwa kila mateka wa vita. Haiwezekani kutochukuliwa sura mojawapo kati ya hizo mbili. Naam, kama kuna mtu ambaye hataki kuwafanyia hisani ya kuwaachia huru, basi anaweza kuwatumikisha hadi wakati ule watakapolipa fidia ya vita kwa kujikomboa. Zitazameni tu nchi za Ulaya za siku hizi. Wafungwa wa Ufaransa waliotekwa na Hitler, yeye atachukua kutoka kwao fidia ya kujikomboa na wakati huo huo anawatumikisha. Kila mahali barabara hutengenezwa kwa kuwatumia wafungwa wa kivita, sehemu nyingine huchimbishwa udongo na sehemu zingine hufanyishwa kazi nyingine. Hakuna shaka wao hufanyishwa kazi kulingana na vyeo vyao, lakini hawawaachi tu bila ya kuwafanyisha kazi. Hivyo, hata sasa wafungwa wa kivita hutumikishwa kazi mbali mbali, na hili ndilo agizo la Islam, tofauti ni hii tu kwamba kwao fidia ya kujikomboa hutiliwa kipaumbele, na Islam yasema kwamba agizo letu la kwanza ni kwamba wafanyieni hisani na kuwaachia huru, na kama hamwezi kufanya hisani, basi agizo letu la pili ni hili kwamba chukueni toka kwao fidia ya vita na muwaachie huru.

## Kulingana na Fundisho la Islam la Kumwachia Huru Mfungwa wa Kivita kwa Makubaliano ya Kutoshiriki Tena katika Vita Dhidi ya Waislamu

Inathibitika pia kutokana na utekelezaji wa Mtume Muhammad[sas] kwamba wakati wa kuwaachia huru wafungwa kwa hisani, mapatano haya yanaweza kukubaliwa ya kuwa hawatashiriki tena katika vita dhidi ya Waislamu, kwani inawezekana mtu fulani aachiwe huru na halafu ashiriki tena katika vita dhidi ya Waislamu. Ndiyo sababu Mtume[sas] akaruhusu kutoa sharti la aina hii. Kuna tukio lililotokea katika zama zake mwenyewe Mtume[sas] ambalo linaonyesha kuwa hatari za aina hii zaweza kutokea wakati wa kuwaachia huru wafungwa wa kivita. Safari moja Mtume[sas] alimwachia huru mfungwa mmoja aitwaye Abu Uzza. Mtu huyo alikuwa amekamatwa katika vita vya Badri. Mtume[sas] akamwachia huru kwa kuchukua ahadi ya yeye kutoshiriki katika vita yoyote dhidi ya Waislamu, lakini alijitokeza tena katika vita vya Uhud kwa kupigana dhidi ya Waislamu na mwishowe alikamatwa mateka katika vita ya Hamraaul Asad na kuuawa. Hivyo, kwa ajili ya wafungwa wa vita, Islam inapendekeza sura mbili tu: (1) Waachwe kwa hisani, na kama hilo haliwezekani, basi (2) waachiwe huru baada ya kupokea kutoka kwao fidia ya vita ya kujikomboa.

## Kuwatumikisha Wafungwa wa Vita

Naam, wanapokuwa hawatoi fidia, inajuzu kuwatumikisha, kwa sababu lengo la kuwafanya kuwa wafungwa ni kuidhoofisha nguvu ya adui. Kama wafungwa wa vita wakusanywe tu na kuanza kulishwa bila ya kufanyishwa kazi ambayo itasaidia kukabiliana na adui, basi hapo nguvu ya adui itazidi, haitapungua. Lakini katika hayo pia kuna tofauti kubwa ya kiutendaji kati ya Islam na serikali za siku hizi.

## Wakati wa Kuwatumikia Wafungwa wa Vita, Agizo la Kuangalia Uwezo Wao na pia Kuangalia Chakula Chao na Mavazi yao

Siku hizi, miongoni mwa wafungwa wa vita, maafisa wa vyeo vya juu hawatumikishwi, lakini wafungwa wa kawaida wanapewa kazi nzito. Lakini Islam inasema: (1) msimfanyishe mfungwa yeyote kazi iliyo nzito kuliko uwezo wake. (2) mlisheni kama kile mnachokila wenyewe na mvisheni kama kile mkivaacho. Sasa serikali za Ulaya ziseme, je, hizo nazo pia zinafanya hivyo? Je Waingereza wanawalisha wafungwa wa vita wa Kijerumani na Kijapani chakula kama kile wakilacho wenyewe? Au Wajerumani wanawapa wafungwa wa vita wa Kiingereza wakilacho wenyewe? Hawafanyi hivyo hata kidogo. Lakini Islam inasema walisheni kile kile mnachokula na muwavishe kile kile mkivaacho. Na kuhusiana na jambo hili, masahaba wa Mtume[sas]

walikuwa wakilizingatia jambo hili kwa umakini kiasi ya kwamba safari moja masahaba walikuwa safarini wakiwa wameandamana na baadhi ya watumwa (wafungwa wa vita). Watumwa hao wenyewe wanasimulia kuwa njiani tende zilipokaribia kwisha, masahaba hao waliamua kuwa wao wenyewe watajikimu tu na kokwa za tende na sisi watatupatia tende zenyewe. Hivyo wakawa wakifanya hivyo juu ya kwamba kokwa hizo zilikuwa hazitoshelezi kuwashibisha. Basi, amri hii iliyotolewa na Islam kuwa walisheni watumwa wenu kile mnachokula, mfano wake haupatikani popote duniani isipokuwa katika maisha ya masahaba wa Mtume Muhammad[sas].

## Ndani ya Mafundisho ya Islam Imekatazwa Kuwadhikisha na Kuwapiga Wafungwa wa Vita

Kisha Anasema kwamba msiwapige wafungwa wenu, na kama kuna mtu aliyempiga mtumwa wake kimakosa, basi mtumwa huyo aliyepigwa atakuwa huru wakati huo huo. Imesimuliwa katika Hadithi kwamba safari moja Mtume[sas] alitoka nje ya nyumba yake na kumuona sahaba mmoja akimpiga mtumwa wake. Sahaba huyo mwenyewe anasimulia kuwa nilikuwa katika hali hiyo ya kumpiga mtumwa wangu, nikaisikia sauti ya Mtume[sas] nyuma yangu, Unafanya nini wewe? Hiki ni kitendo cha zama za kijahili.

Siku hizi watu wanawapiga hata watumishi wao wa nyumbani na hawalioni jambo hilo kuwa ni la aibu.

Lakini Mtume[sas] alimkaripia sahaba yule kwa kitendo cha kumpiga mtumwa na kasema: unafanya nini? Mamlaka uliyo nayo juu ya mtumwa huyu, mamlaka makubwa zaidi ya hayo Anayo Mwenyezi Mungu juu yako. Sahaba yule anasema nilitetemeka nilipoisikia sauti hiyo na kusema: Ewe Mtume wa Allah, mimi namuachia huru. Mtume[sas] akasema: Kama usingemwachia huru, ungeingia jahanamu.[19]

Kadhalika sahaba mwingine anasimulia kuwa tulikuwa ndugu saba, nasi tulikuwa na kijakazi mmoja tu. Siku moja mdogo wetu wa mwisho alimpiga kofi kutokana na kosa fulani. Habari ilipomfikia Mtume[sas] akasema, fidia ya kumpiga kibao ni moja tu, ni kumwachia huru, hivyo wakamuachia huru. Ndiyo kusema kwamba Mtume[sas] sio tu alikuwa hapendi kupigwa vikali kwa mtumwa au kijakazi, bali hakupenda wapigwe hata kofi moja, na fidia yake aliyokuwa akiisema ni moja tu kwamba yeye aachiwe huru. Siku hizi watu wanapiga sana hadi kuacha alama mwilini, lakini Mtume[sas] alisema: sio tu kumpiga mfungwa kwa fimbo, bali hata ukimpiga tu kofi, maana yake itakuwa ni kwamba wewe hustahili kuwa na mtumwa, nawe kwa kitendo chako umethibitisha kuwa huwezi kustahili kuwa na yeyote chini ya himaya yako, hivyo umwachie huru mara moja.[20]

## Miongozo ya Islam Kuhusiana na Kuwaozesha Wafungwa wa Vita wenye Uwezo wa Kuoa

Kisha Anasema kama wao ni wenye uwezo wa kuoa na wamebalehe basi muwaozeshe kwani haijulikani ni lini watakuwa huru. Hivyo kuhusiana na jambo hili, Mwenyezi Mungu Anaagiza ndani ya Kurani Tukufu kwa kusema:

وَ اَنْكِحُوا الْاَيَامٰى مِنْكُمْ وَ الصّٰلِحِيْنَ مِنْ عِبَادِكُمْ وَ اِمَآئِكُمْ [21]

> "Tunawaamuruni muwaozeshe wale miongoni mwa vijakazi na watumwa wenu wenye uwezo wa kufunga ndoa."

Sasa hebu semeni, je kanuni za kimataifa za siku hizi zinafundisha utendaji wa wema zaidi ya huu? Siku hizi hawawaruhusu hata wake zao kuwatembelea, achilia mbali kuwaozesha. Lakini Islam inasema muwalishe kile kile mnachokula wenyewe na muwavishe kile kile mkivaacho wenyewe. Miongoni mwao wenye uwezo wa kuoa waozeshwe, msiwatendee kwa ukali, na kama mkimpiga wakati wowote, basi fidia yake ni kumwachia huru mara moja. Isitoshe, je leo kuna serikali yoyote iliyo tayari kuwaachia huru wafungwa hao kwa kukiri tu kuwa hawatoshiriki katika vita nyingine dhidi yao, au yupo yeyote aiachiaye serikali yoyote inayopigana vita bila ya kuchukua mali ya fidia ya vita?

## Katika Mafundisho ya Islam Kuachiwa Huru kwa Wafungwa wa Vita kwa Kutoa Fidia ya Kujikomboa

Islam imerahisisha sana masharti ya kujikomboa kwa kulipa fidia ya vita kwa kiasi hiki kwamba Mungu Alisema, ama muwaachie huru kwa ihsani — ikitanguliza hisani; na iwapo hamuwezi kufanya hivyo, basi waacheni kwa kupokea toka kwao malipo ya kujikomboa, na fidai ya vita si kitu kingine ila ni malipo ya gharama ya vita. Naam, tofauti hii ipo kwamba mwanzoni vita ilikuwa ikipiganwa baina ya watu, hivyo fidia pia ilikuwa ikipokelewa kutoka kwa watu, lakini sasa vita inapiganwa baina ya mataifa, kwa hiyo njia itakuwa kwamba taifa lilipe fidia ya vita. Siku za nyuma kulikuwa hakuna majeshi maalumu, na watu wa taifa husika walikuwa wakilazimika, kila mmoja wao, kulipia gharama ya vita hiyo. Kwa hiyo wakati ule njia bora ya kuwatunza wafungwa wa vita ilikuwa ni kuwagawa baina ya watu, ili wafidie gharma zao za vita kwa kuwatumia katika shughuli mbalimbli. Lakini serikali inapokuwa na jeshi maalum na gharama za vita zinakuwa hazichangiwi na mtu mmoja mmoja, hapo wafungwa wa vita hawatagawiwa kwa watu, bali watakuwa chini ya ulinzi wa serikali. Na taifa jingine litakapolipa fidia, basi wafungwa hao hawatatumikishwa na wataachiliwa huru. Sasa hebu niambieni, wakati mfungwa ana hiari ya kujikomboa, kwa nini asilipe fidia na kujikomboa. Ikiwa

hawezi kulipa fidia, basi watu wa familia yake wanaweza kumlipia, na kama wao pia hawana uwezo, basi serikali inaweza kumwachisha kwa kumlipia fidia. Kwa vyovyote, hakuna sura yoyote ile ambapo mlango wa kuachiliwa kwake haukukweka wazi.

## Njia ya Kujikomboa kwa Mtu Asiyeweza Kulipa Fidia

Inawezekana mtu aseme kwamba labda mfungwa ni maskini sana asiye na uwezo wa kulipa fidia, serikali iwe ni dhalimu na isiwe na hisia yoyote ya kumwachisha huru, watu wa familia yake wawe wasiojali na katili na wawe wenye kutaka kuwa aendelee kubakia mfungwa ili waichukue mali yake, na upande mwingine mmiliki asiwe na uwezo wa kumwachia huru bila kupokea malipo ya fidia, kwa sababu inawezekana kabisa kwamba kiasi kile alichotumia vitani kikawa kimemharibia hali yake ya kifedha. Sasa katika hali kama hiyo mfungwa atawezaje kujikomboa?

Kurani Tukufu imejibu suala hilo. Mwenyezi Mungu Anasema:

وَالَّذِينَ يَبْتَغُونَ الْكِتَابَ مِمَّا مَلَكَتْ أَيْمَانُكُمْ فَكَاتِبُوهُمْ إِنْ عَلِمْتُمْ فِيهِمْ خَيْرًا ۖ وَآتُوهُمْ مِنْ مَالِ اللَّهِ الَّذِي آتَاكُمْ ۚ[22]

Na wale wanaotaka hati katika wale inaowamiliki mikono yenu ya kuume, basi waandikieni kama mkiona

wema kwao. Na wapeni katika mali ya Allah Aliyowapeni.

Yaani wale ambao Mwenyezi Mungu Amewafanya kuwa watumwa wenu, nanyi mkiwa mmewamiliki, kama wawaambieni: Bwana, hatuna yeyote wa kutukomboa wala hatuna fedha ya kutoa fidia ili tuweze kuwa huru, sisi ni maskini na tusio na uwezo. Tunakutolea sharti hili kwamba tutakulipa fedha zako ndani ya miaka miwili au mitatu au minne, na tutakuwa tunakulipa kiasi fulani kila mwezi, hivyo tuachie huru. Sasa, kulingana na aya hii: فَكَاتِبُوهُمْ إِنْ عَلِمْتُمْ فِيهِمْ خَيْرًا mwalazimika kuwaachia huru na kuwakadiria kiasi cha fidia watakacholipa kila mwezi sharti mfahamu kuwa wao wanao uwezo wa kuchuma mali, bali mnapaswa kuwasaidia kwa kile alichowaruzukuni Mwenyezi Mungu. Yaani muwapatie kiasi cha fedha, ili kwa njia hii wachume mali na kuweza kulipa fidia yao. Hivyo, kuanzia wakati ule viwango vyao vya kulipa vinapokuwa vimekadiriwa, mtumwa anakuwa huru katika mambo yake kama vile mtu yeyote mwingine aliye huru. Na atatambuliwa kuwa ni mwenye kumiliki mali yake.

Kama juu ya sura zote hizi, mtu anabakia kuwa mtumwa na hafanyi juhudi ya kujikomboa, basi hiyo yamaanisha kwamba yeye mwenyewe anapenda kubaki kuwa mtumwa na anafurahia utumwa. Ilmurdi sawa na mafundisho ya Islam, watu hawafanywi watumwa katika

vita za kidunia, bali hufanywa katika zile vita tu zilizo za kidini. Lakini kuhusiana na watumwa hawa imeamriwa pia kwamba kwanza waachiwe huru kwa hisani, na kama hii hamwezi, basi waachiwe huru kwa kuchukuliwa fidia. Na si lazima kwamba wenyewe waitoe fidia hiyo, jamaa zao pia wanaweza kuitoa fidia hiyo, serikali pia yaweza kutoa. Na kama serikali haijali na jamaa zake ni wadhalimu na yeye mwenyewe ni maskini, hapo anaweza kusema kwamba tukubaliane mimi na wewe kwamba ninawajibika kutoa kiasi gani cha fidia na unipe muhula fulani wa kuilipa fidia hii. Katika kipindi hicho nitamaliza fidia yangu ya vita kwa kutoa kiasi fulani cha fedha kila mwezi. Mara tu baada ya makubaliano haya atakuwa huru na mmiliki wake hatakuwa na haki yoyote ya kuweka kikwazo cha aina yoyote katika makubaliano haya. Kuzuiwa kwa makubaliano hayo kunawezekana tu katika hali hii kwamba ndani yake mnakuwa hamna heri, yaani kunakuwa na hatari ya kutokea kwa vita. Au mtumwa huyo awe ni mwendawazimu au mwenye akili kidogo na hivyo huwezi kuchuma chochote, na kuwepo na hatari kwamba badala ya kupata faida atapata hasara.

Katika sura ya mkataba wa aina hii, Islam inaagiza kumpatia mtaji mtumwa huyo, hata kama mtaji huo utolewe na mmiliki wake au serikali.

## Upeo wa Juhudi ya Islam Kuhusiana na Kuwaachia Huru Wafungwa wa Vita

Halafu yawezekana kwamba mtu aseme kwamba kama inajuzu kuuzuia mkataba wa mtu aliye mwehu au taahira, basi watu watasema kuwahusu watu wenye fahamu zao nzuri kuwa hawana akili na kuendelea kuwafanya watumwa wao, na hivyo hawatakuwa huru. Jibu lake ni hili kwamba ndani ya sheria ya Kiislamu, itokeapo hali ya aina hii, basi mtumwa huyo anaweza kutuma maombi serikalini kwamba mimi ni mtu mwenye akili timamu na nina uwezo wa kuchuma mali, lakini mmiliki wangu, kwa makusudi anaendelea kuniweka utumwani. Kwa hali hii Kadhi atatoa hukumu na kumpa haki ya kuachiwa huru. Kwa uchache, hakuna hali yoyote ambamo uhuru wa watumwa haukuzingatiwa. Kwanza, mmiliki ameagizwa afanye hisani na kumwachia huru. Pili, kama mmiliki hawezi kufanya hivyo, basi mtumwa amepewa hiari ya kulipa fidia na kujikomboa. Na kama hana uwezo wa kutoa fidia, basi afanye mkataba na aseme kwamba mimi nitatoa fedha kwa awamu kadhaa, nipatie muhula wa miaka miwili au mitatu. Afanyapo tu mkataba huo basi atafahamika kuwa tayari ameshakuwa huru. Na kama juu ya kuwepo kwa masharti yote haya, mtu aseme kwamba mimi sitaki kuwa huru, basi hakuna budi kukubali kwamba huyo anauona utumwa wake kuwa

bora kuliko huru wake. Na ukweli ndio huu kwamba wale watumwa waliokuwa wakimilikiwa na Masahaba wa Mtume[sas] wao, sawa na maagizo ya Mtume[sas], walikuwa wakiwaweka katika hali bora na ya raha kiasi ya kwamba wao walikuwa wakiuona utumwa wa masahaba[ra] kuwa ni bora kuliko huru wao.

## Masahaba[ra] Kuwatendea vyema Watumwa

Chochote walichokuwa wanakula masahaba ndicho hicho hicho walichokuwa wakiwalisha watumwa, walikuwa wakiwavisha kile kile walichokuwa wakivaa. Hawakuwapa adhabu ya kimwili. Hawakuwafanyisha kazi yoyote ambayo wao wenyewe walikuwa hawawezi kuifanya. Walikuwa hawawafanyishi kazi yoyote ambayo wao wenyewe hawakupenda kuifanya na kama waliwafanyisha basi na wao wenyewe walishiriki pamoja nao katika kuifanya. Na kama wakiomba kupewa uhuru, basi mara moja walikuwa wakiwaachia huru kwa sharti ya kujilipia fidia. Kwa kuiona hali hii, mioyo ya watumwa hao haikutamani kuwa wawe huru. Walifahamu kuwa hapa tunapata chakula kizuri, bali Bwana wao anawalisha kwanza halafu anakula mwenyewe, kama tukienda jumbani kwetu tutapata tu chakula cha kawaida. Kwa hiyo, walikuwa hawaombi waachiwe huru. Hivyo, ingawa wao walikuwa ni watumwa, lakini kwa hakika mioyo yao ilikuwa imeshatekwa na walikuwa vile kama alivyokuwa

mtumwa wa Hadhrat Khadija[ra], Hadhrat Zaid bin Harith, aliyependelea kumtumikia Mtume[sas] badala ya kuwa huru.

## Mfano wa Mtume[sas] wa Kumtendea vyema Mtumwa na Matokeo yake

Wakati Hadhrat Khadija[ra] alipoolewa na Mtume[sas], yeye alimpatia Mtume[sas] mali yake yote na pia kumkabidhi Bwana Zaid aliyekuwa mtumwa wake. Mtume[sas] akamwachia Zaid huru. Hadhrat Zaid kwa hakika alikuwa si mtumwa kama wengine bali alikuwa ni kijana aliyetokana na familia ya kiungwana ambaye alitekwa nyara na kufanywa mtumwa, aliyekuja hatimaye kuibukia kwa Mtume[sas]. Baba yake mzazi na baba yake mdogo wakiendelea kumtafuta wakafika Makka na wakamuomba Mtume[sas] kwamba zaid atumwe aende pamoja nasi. Mtume[sas] alikuwa tayari ameshamuachia huru Zaid, hivyo akasema: "Mimi simzuii, kama anataka kwenda, basi na aende. Wao wakamwambia Zaid, "Mwanangu, twende nyumbani, mama yako analia sana na ana huzuni kubwa sana kwa kutengana nawe, na wakiashiria kwa Mtume[sas] wakasema kuwa yeye tayari ameshakupa uhuru na kukuruhusa urjee pamoja nasi. Zaid akasema: 'Bila shaka ameniachia huru, lakini mimi kwa moyo wote ni mtumwa wake na sitaki kutengana na utumwa huu. Baba alijitahidi sana kumbembeleza na kusema tazama zingatia hali ya mama yako mzee. Baba

yake mdogo pia akajaribu sana na kusema kuwa ni nani awezaye kumtendea mtu vyema zaidi ya wazazi wake? Twende nasi na tutakuwa nawe kwa upendo mkubwa sana. Lakini Hadhrat Zaid akasema siwezi kwenda pamoja nanyi, kwani hakuna mama au baba wa duniani awezaye kunitendea wema kama anitendeavyo huyu.

Sasa hebu semeni, je utumwa kama huu unaweza kupingwa? Au moyo wa mtu hujaa tele jazba na shukrani na machozi yanamlengalenga na kustaajabu kwamba je uhusiano mwema wa aina hii waweza kupatikana duniani kati ya watu wawili?

## Sababu za Watu Kubakia Watumwa Siku za Mwanzoni za Islam

Hivyo, kama mnamo siku za mwanzoni za Islam baadhi ya watumwa waliendelea kubakia kuwa watumwa, hiyo inamaanisah kwamba Waislamu walikuwa wakiwatendea vyema watumwa kiasi ya kwamba watumwa wenyewe wakawa wanataka waendelee kubakia ndani ya himaya yao na kubakia utumwani mwao, maana, kwao kuwa mtumwa ni bora mno kuliko huru. Lakini mapadri wa Ulaya wakikaa mbali wanaendelea kulalamika kuwa Islam haikuuondoa utumwa. Wahadhiri katika mikutano mikubwa mikubwa, hata kama wakichukua dakika tano tu zaidi ya wakati wao waliowekwewa, watu huanza kupiga makelele. Lakini ni matokeo ya utumwa wa moyoni na ya kumuamini Hadhrat Masihi Mau'udi[as]

kwamba hapa katika mkutano wetu, hata kama wasikie baridi, njaa, mikono na miguu ife ganzi kutokana na baridi, lakini watu huendelea kukaa na hupenda kwamba hotuba iendelee tu. Je utumwa huu unastahili kupingwa au unakuwa ni wenye kukuza imani? Utumwa huu unakuwa sio wa watu bali unakuwa ni wa Mwenyezi Mungu.

Ilmuradi, hakuna yeyote awezaye kusema kwamba sasa dunia imepiga hatua zaidi ya maendeleo, na imeutokomeza utumwa, kwa sababu toka mwanzoni Islam iliufuta kabisa utumwa. Naam, imetoa ruhusa ya kuweka wafungwa wa vita, lakini kuhusiana nao pia imeweka kanuni ambazo hadi sasa dunia haijaweza kuziweka. Hivi sasa si Mwungano wa nchi za Uingereza, Ufaransa na Marekani — katika vita kuu ya pili — uwezao kuzitekeleza kanuni hizi wala shirikisho la nchi za Ujerumani, Italia na Japani.[23]

## Baadhi ya Nadharia za Kifalsafa Kuhusiana na Kuhalalisha Kuwadhulumu Watu

Kimuhtasari, Islam imefuta kabisa utumwa. Kilichobaki ni ule udhia unaopatikana kwa sababu ya utumwa wa undani, yaani kutokana na umaskini au kutokana na kumilikiwa na mtu. Ugonjwa huu nao umetibiwa na Islam, lakini kabla ya kuifhamu tiba yake ikumbukwe kwamba tofauti za wazi za kidunia huzalika kutokana na baadhi ya nadharia za kifalasfa, na nadharia hizo ni hizi:

## Nadharia ya Kwanza

Kwanza, baadhi wanasema 'mwenye nguvu umpishe', hivyo sisi pia tunapaswa kufanya hivyo hivyo. Waingereza walipokua na nguvu, wakaziteka nchi nyingi. Kadhalika Italia ilipoishambulia Abyssinia (Uhabeshi), basi Mussolini alitoa hotuba ambamo alisema kwamba sisi tumeishambulia ili kuwahudumia Wahabeshi na makusudio yetu katika hatua hizi ni yale yale waliyokusudia Waingereza kuhusu India. Wanasema kwamba sisi tuanitawala India ili tuwaelimishe majahili wa huko kuingiza katika nchi zilizoendelea. Je ndani mwetu hamna uanadamu hata kwamba tusiwahudumie wengine na tusiwaondolee ujahili kwa kuziteka nchi yao. Basi hii pia ni dalili mojawapo ambayo hutolewa na baadhi ya watu?

## Nadharia ya Pili

Pili, wengine wanasema kuwa mtu aliye juu anapaswa abaki kuwa juu, yaani anayeshinda kifedha na anachuma kwa bidii yake, basi asiingiliwe kati.

## Nadharia ya Tatu

Halikadhalika kuna nadharia nyingine inayotolewa kwamba ubora wa kiukoo pia ni ubora wa kweli ambao hauwezi kwa sura yoyote ile kupuuzwa. Hii ndiyo itikadi ipatikanayo ndani ya dini ya Kihindu kwamba *Shudar* atabakia kuwa *Shudar*, *Vesh* atabakia kuwa *Vesh*,

*Khashatri* atabakia kuwa *Khashatri* na *Barhaman* atabakia kuwa *Barhaman*. Kwa kauli yao, tofauti hii ya kiukoo ipatikanayo miongoni mwa watu haiwezi kufutika.

## Nadharia ya Nne

Kuna kanuni nyingine inayoelezwa kwamba wanaostahili kutawala duniani ni wale tu walio wengi, hivyo fanyeni dhuluma mtakavyo kwa wale walio wachache. Sawa na nadharia hii watu hawa huwaangamiza walio wachache na hawaisikilizi hata kidogo sauti ya wachache.

## Nadharia ya Tano

Kadhalika wanayo kanuni hii pia, ukikikuta kitu kilichodondoka basi ukichukue. Sisi tulipokuwa utotoni tukicheza, na kukiona kitu kilichokuwa kimedondoka, basi tulikuwa tukikiokota kwa kusema, 'Tumepata bure kitu cha Mungu.' Na tukayafahamu maneno hayo yanahalalisha kukiokota kitu kama hicho. Lakini kile kitu ambacho watoto wakaokota wakicheza huwa si chenye thamani. Pengine wakaokota punje ya hindi au choroko juu ya ardhi, pengine hukuta kifungo au kitu cha aina hiyo na kukiokota. Mtu fulani alimuuliza Mtume[sas] kwamba "Ewe Mtume wa Allah, kuna agizo gani kuhusiana na kitu cha kuokotwa? Kauliza, kwa mfano? Akasema, kwa mfano nimkute mbuzi porini, je nimchukue au nisimchukue? Mtume[sas] akasema: Kama

umkute mbuzi msituni, basi useme kwa sauti kubwa huku na huko ukisema huyu mbuzi ni wa nani? Na kama usimpate mmiliki wake baada ya kutangaza hivyo, basi umchukue na kumla, kwa sababu usipomla, ndugu yako mbwamwitu atamla. Akauliza tena: Ewe Mtume wa Allah, kuna hukumu gani kama nimkute ngamia msituni? Akamjibu, wewe una uhusiano gani na ngamia, chakula cha ngamia kipo mitini na maji yake yamo tumboni mwake, unahusikanaje na ngamia huyo? Mwache aende tu. Akauliza tena: Ewe Mtume wa Allah, kuna agizo gani kama niukute, mfuko sehemu fulani? Akamjibu ukipata mfuko, ukiokote na uendelee kuwatangazia watu mpaka umpate mwenye mfuko huo. Basi, kuna kanuni tofauti kwa kila kitu cha kuokotwa. Mbuzi au kuku, kwa kuwa ni vitu vinavyoliwa na wanyama, hivyo kama asipopatikana mwenye kuwamiliki, Mtume[sas] ametoa ruhusa yule aliyewapata kuwatumia. Lakini vitu vingine vilivyobakia vinavyoweza kubaki salama kuhusiana navyo ametoa agizo kwamba visiguswe, na vile visivyoweza kukaa kwa usalama, ameagiza, mvichukue lakini mfululize kuwatangazia watu hadi muvifikishe kwa mmiliki wake. Basi Isalm imetoa amri zilizojaa hekima sana na busara kuhusiana na vitu vilivyopatikana pasipo kujulikana anayevimiliki. Lakini sasa kanuni ya mataifa ya Ulaya ni kwamba taifa lisilokuwa na mwenyewe au ni dhaifu linastahili kutwaliwa nao. Austarlia ni nchi kubwa sana.

Kuhusu nchi hizo watu wa Ulaya wanasema tumeipata kwani haina mwenyewe. Kuhusi serikali ya India wanasema tumeipata, maana haikuwa na mwenyewe. Wanasema kuhusiana na Marekani ya kaskazini na kusini kwamba tumezitwaa kwani hazina mwenyewe. Ilmuradi, nadharia ya tano ya mataifa ya Ulaya ni hii kwamba aliyeigundua nchi mpya au popote pale palipo na serikali dhaifu, hiyo ni ya yule aliyefikia kwanza. Mbali na kanuni hizi zinazosababisha dhuluma duniani, pia kuna kasoro zingine za kiutendaji zinazosababisha dhuluma hizo.

## Dosari za Kiutendaji Zichangiazo Kuwadhulumu Watu

Dosari ya kwanza ni kutokuiwajibisha idara yoyote katika kuwatunza watu walemavu na walio wanyonge. Ingawaje sasa, katika baadhi ya nchi, kasoro hiyo imeanza kuondolewa hatua kwa hatua na zimeundwa idara ambazo zinashughulikia kuuondoa ukosefu huo, lakini hata sasa, mpango wao mpya waliouunda bado hauyafikii mafundisho ya Islam.

Pili, ziliachwa wazi njia ambazo kwa njia hizo utajiri wote uletwe mikononi mwa baadhi ya watu.

Tatu, zilibakizwa wazi njia kwamba utajiri usitoke mkononi mwa wale ambao wameishaupata.

Nne, fedha zinatumika bure juu ya fani na hupewa jina la 'Sanaa', na baadhi ya hizo zapatikana sehemu hii au ile na baadhi nyingine zapatikana kila mahali.

Islam imefunga njia zake hizo za uharibifu na kufungua njia mpya za maendeleo. Hivyo, Islam imeyatibu mambo yote hayo kwa njia hizi:

## Katika Islam Tiba ya Utumwa wa Undani, yaani Udhia Unaosababishwa na Kutawaliwa na Wengi

Kwanza kabisa Islam imetangaza kuwa kila kitu kilichoumbwa na Mwenyezi Mungu ni kwa ajili ya dunia nzima, hakikuumbwa kwa ajili ya mtu fulani. Hili ni jambo kama vile wazazi, wakati mwingine, wanampatia mtoto mmoja sahani ya tamutamu, naye anataka kuzila peke yake, ndipo wazazi wake humwambia kuwa hii si kwa ajili yako peke yako, bali nduguzo wote wana haki humo, vivyo hivyo Mwenyezi Mungu Asemavyo: هُوَ الَّذِىْ خَلَقَ لَكُمْ مَّا فِى الْاَرْضِ جَمِيْعًا[24]. Chochote kilichomo humu duniani ni miliki ya wanadamu wote kwa ujumla, kama vile mama, baada ya kumpa mtoto wake mmoja sahani yenye tamutamu, anavyomwambia kuwa hii ni kwa ajili ya nduguzo wote pamoja nawe.

Chini ya kanuni hii, Islam imeukataa kabisa Ubeberu, Ujamaa wa Kitaifa na Ujamaa wa Kimataifa wa siku hizi, kwani falsafa hizo zinatoa haki kwa mataifa yenye nguvu, yaliyoelimika na kujipanga vizuri, kuyatawala

mataifa mengine. Siku hizi pia mjadala huu unaendelea kuhusiana na suala hili kwamba kama ikubaliwe kuipa India uhuru, basi kesho Waafrika watataka uhuru wao, ilhali hao walikuwa wakitembea rabana, nasi tuliwafundisha ustaarabu. Lakini suali lenyewe ni kwamba kama walikuwa wakitembea uchi, nyingi msingeutazama utupu wao na mngebakia majumbani mwenu. Mnasema kwamba walikuwa wakila tu majani ya miti, nasi tukawafundisha ubinadamu, je sasa si haki yetu kuwatawala? Tunasema kama walikuwa wakila majani ya miti au matunda, sasa nyinyi mlikuwa na haki gani ya kuiteka nchi yao na kuwalisha keki. Basi kwa kusema 'Yeye ndiye Aliyewaumbieni vyote vilivyomo katika ardhi,' Mwenyezi Mungu Ametufahamisha kuwa vyote vilivyomo duniani ni kwa ajili ya watu wote wa dunia. Sio kama kanuni iliyoundwa siku hizi huko Afrika Kusini kwamba katika nchi yetu asiingie mgeni yeyote. Vivyo hivyo Marekani imetunga sheria kuwa hakuna mgeni yeyote anayeruhusiwa kuingia, ilhali dunia nzima inapaswa kufaidika na manufaa ya Afrika Kusini na kadhalika dunia nzima yapaswa kufaidika na manufaa ya Marekani. Sio kwamba watu wa Afrika Kusini au Wamarekani tu ndio wafaidike na nchi nyingine zinyimwe.

## Agizo la Islam Kuhusiana na Ugunduzi wa Migodi

Halikadhalika Islam imezipinga dhuluma za wale matajiri wanaojikusanyia mali za asili, imesema kuna hisa pia ya dunia iliyobaki katika mali yao. Wao wasingeweza kutajirika kiasi hicho bila ya kuzitumia mali hizo za asili. Lakini, kwa kutumia nguvu yao ya mali wanayatwaa machimbo ya madini na hivyo wanakuwa sababu ya kunyang'anya haki za wengine. Islam imetatua tatizo hilo kwa kuiwekea serikali sehemu ya tano ya machimbo. Halafu mali waikusanyao wenye kuimiliki migodi hiyo, kama mwaka mzima unapita bila kutumia zaka yake pia inatolewa. Kwa njia hii serikali inakuwa na hisa yake katika migodi na kwa njia hii hukusanyika fedha nyingi kwa ajili ya maskini, iwezayo kuwapatia haki zao, na kasoro ile ambayo inaibuka kutokana na ugunduzi wa migodi haitokei katika mfumo wa utamaduni.

## Utatuzi wa Islam Dhidi ya Kutwaa Mali za wengine kwa Kisingizio cha Kuzihifadhi

Utatuzi wa pili uliopendekezwa na Islam ni kutangaza duniani kwamba لَا تَمُدَّنَّ عَيۡنَيۡكَ اِلٰى مَا مَتَّعۡنَا بِهٖۤ اَزۡوَاجًا مِّنۡهُمۡ وَ لَا تَحۡزَنۡ عَلَيۡهِمۡ وَ اخۡفِضۡ جَنَاحَكَ لِلۡمُؤۡمِنِيۡنَ ﴿۸۹﴾[25]. Yaani msizichukue mali za wengine kwa kisingizio hiki kwamba sisi tutazitunza. لَا تَمُدَّنَّ عَيۡنَيۡكَ اِلٰى مَا مَتَّعۡنَا بِهٖۤ اَزۡوَاجًا مِّنۡهُمۡ Usizikodolee macho zile mali Tulizowapa watu wengine. وَ لَا تَحۡزَنۡ عَلَيۡهِمۡ Na wala msiseme kwamba sisi tunapata huzuni sana kwa kuiona

hali yao. Anasema hiyo huzuni muibakize kwa ajili yenu tu. وَ اخۡفِضۡ جَنَاحَكَ لِلۡمُؤۡمِنِيۡنَ Raia wenu wapo, fanyeni jitihada zozote muwezazo kuzifanya za kuuendeleza utamaduni wao, hakuna yeyote anayewakatazeni. Lakini kama mseme kwamba sisi tunasumbuliwa sana na huzuni za wengine, nasi tunataka kuwatawala ili tuwape maendeleo, basi hiyo hatuafikiani nayo. Ninyi kaeni majumbani mwenu na wao muwaache waishi majumbani mwao. Leo msingi wote wa ukoloni ni juu ya dai hili hili potofu kwamba sisi tumeiteka nchi yao kwa ajili ya manufaa yao. Kisingizio hiki hiki hutumika wakati wa kuitwaa kila nchi, lakini baada ya muda mfupi tu uhakika wa dai hili unatoboleka wakati wanapoupora utajiri wote wa nchi hiyo na hakuna yeyote awaulizaye hali wenyeji wa nchi hiyo. Nenda huko Afrika ya Mashariki ambako kuna serikali ya Kiingereza. Huko hali ndiyo hii kwamba Waingereza ni matajiri wakubwa, lakini wenyeji wenyewe wa huko wako katika hali ya umaskini na wanapitisha maisha wakiwa watumisi wao. Hivyo, Anasema kwamba fikirieni ustawi wa watu wenu, na muwaache wengine kitika hali zao. Wao hata wakiwa maskini namna gani, watajiangalia wenyewe. Kama isemwe kwamba je, wasisaidiwe? Basi jibu lake ni hili kwamba Islam haisemi kwamba msiwasaidie wengine, inachosema ni kwamba usitoe msaada kwa tamaa na kwa kujinufaisha. Sasa huduma, hata mwalimu pia huitoa, lakini huduma yake ni hii hii tu kwamba

hufundisha elimu na kupata mshahara. Lakini watu hawa waendapo katika nchi yoyote ile, basi huwagawia ardhi za nchi hiyo watu wao, na maelfu ya wenyeji kuangamia. Hivyo, Anasema kuwa njia hiyo siyo sawa.

Kwanza, msiende kwenye nchi za wengine kwa lengo la kisiasa, na kama mnaenda basi muende kama watoa huduma. Kwa hiyo kutoa msaada kwa ajili ya kuwanufaisha wengine bila ya kuteka nchi hakukukukatazwa. Kilichokatazwa ni kwamba mtu asiende huko akiwa si mtoa huduma, bali mteka nchi. Sasa tazameni hata Wabolsheviki nao hawakubaki nyuma katika haya. Waliivamia Finland na kuiteka na kisha kupiga kelele kwamba sisi twataka tu kustawisha amani huko. Hivyo Islam inasema kuwa njia hii sio sahihi, mnapaswa kujiepusha nayo. Ukweli ni huu kwamba suala la makoloni yote linaweza tu kutatuliwa na njia ile iliyoelezwa na Islam, waila njia zote za siku hizi ni zenye makosa na sio sahihi.

## Shirikisho la Kimataifa la Kiislamu na Kanuni zake nne za Msingi

Asili ya tatu ielezwayo na Islam ni hii kwamba maadamu dunia haiji kwenye egemeo moja, basi kwa ajili ya kuimarisha amani wote wawekwe ndani ya mipaka yao. Kanuni ya Islam ni hii kwamba dunia yote iletwe kwenye egemeo moja, na kama bado

haijafanyka hivyo, basi inatoa mwongozo huu kwa ajili ya utatuaji wa migogoro:

وَاِنْ طَآئِفَتٰنِ مِنَ الْمُؤْمِنِيْنَ اقْتَتَلُوْا فَاَصْلِحُوْا بَيْنَهُمَا ۚ فَاِنْۢ بَغَتْ اِحْدٰىهُمَا عَلَى الْاُخْرٰى فَقَاتِلُوا الَّتِيْ تَبْغِيْ حَتّٰى تَفِيْٓءَ اِلٰٓى اَمْرِ اللّٰهِ ۚ فَاِنْ فَآءَتْ فَاَصْلِحُوْا بَيْنَهُمَا بِالْعَدْلِ وَاَقْسِطُوْا ؕ اِنَّ اللّٰهَ يُحِبُّ الْمُقْسِطِيْنَ ۝١٠ [26]

> "Na ikiwa makundi mawili katika waaminio wanapigana, basi fanyeni suluhu kati yao; na ikiwa moja la hayo limerukia mwenziwe, basi piganeni na lile lililoruka mpaka hadi lirudie kwenye uamuzi wa Allah. Na kama likirudi, basi yapatanisheni baina yao kwa uadilifu, na hukumuni kwa haki. Hakika Allah Huwapenda watendao haki."

Yaani kama serikali mbili zipigane vita, basi mzisuluhishe, na kama zisiwe tayari kuumaliza mgogoro wao kwa amani na serikali moja iishambulie nyingine, basi hapo serikali zote ziungane na kukabiliana na serikali yenye kushambulia. Itakapokubali kushindwa na kusema sasa inakubali kuacha vita, basi hapo mfanye tena usuluhishi baina yao na mziwekee mkataba wa masharti ya suluhu hiyo. Lakini mkumbuke kwamba mtakapokuwa mkiweka masharti ya usuluhishaji, basi msiachane na haki na uadilifu kwa sababu ya hasira ya kwamba kwa nini serikali hiyo ilianzisha vita. Na

msianze kuomba ujira wenu pia, bali mjikite tu kwenye ule ule mzozo uliokuwepo.

Hebu tazameni, huu ni utabiri mkubwa kiasi gani! Wakati ilipoteremka aya hii, hayakuwepo makundi yoyote ya Waislamu yaliyokuwa katika hatari ya mapigano biana yao. Hivyo, hii kwa kwa hakika ilikuwa ni bishara ihusikanayo na siku zijazo. Maneno بغى na Qaatiluu pia yanadhihirisha kuwa hiyo inahusiana na serikali. Hivyo, Allah Anasema kwamba kama serikali mbili zigombane, basi mnaagizwa kwamba myalazimishe madola hayo kukubuli kuamuliwa mgororo na Baraza la Mataifa. Kama wakikubali, ni vizuri, na wasipokubali na nchi moja iishambulie nyingine, hapo mataifa mengine yote yaliyobakia yatalazimika kuungana dhidi ya taifa hilo na kulishambulia na kulishinda. Hatimaye, baada ya kushindwa likakubali kufanya suluhu, basi mpange masharti ya usuluhisho kwa haki na uadilifu. Kwa jazba ya ulipizaji kisasi dhidi ya taifa hilo, msilivujilie mbali vipande vipande kujinufaisha. Kanuni zilizoelezwa ndani ya aya hii ni hizi:

(1) Itokeapo hitilafu baina ya nchi mbili, basi nchi zingine zizilazimishe nchi hizo zitatue hitilafu zao kwa mazungumzo.

(2) Kama nchi moja ikatae na kuanzisha vita, basi nchi zote ziungane na kuipiga vita nchi ile iliyokaidi na kuanzisha vita.

(3) Ishindwapo nchi ile iliyoanzisha vita na kuridhia kurejea kwenye mazungumzo ya upatanishi, basi nchi zingine zote zikiwa pamoja zifanye upatanishi. (Ndani ya aya, 'Sulh' ya kwanza ina maana ya kufanya kazi kwa sababu na kukaa kuafikiana, na 'Sulh' ya pili ni ile suluhu nyingine inayomaanisha kupatanisha juu ya masharti kwa suluhu, kwani hakuna maana ya kuwa na masharti mara nyingine. Kuongeza neno 'adili', pia kunahakikisha maana hii.)

(4) Lakini msiwe na hamaki kwa sababu ya vita. Yule mwenye haki yake apewe. Wakati mwingine hata mwenye haki hupigana kutokana na hamaki, lakini hata hivyo haki inakuwa ni yake.

(5) Na neno *wa aksituu* linaashiria kwenye upande huu kwamba yale mataifa yaliyosuluhisha yasitafute kujinufaisha kutoka kwa nchi iliyoshindwa au iliyoshinda.

Shirikisho hili la Kimataifa lilitolewa na Islam katika wakati ule ambapo hakuna hata yeyote aliyeliwazia jambo la aina hii, na Mwenyezi Mungu Alinifahamisha jambo hilo la muhimu ambalo ni kazi kubwa inayofanywa na mitume na makhalifa tu.

Hakuna mtu anayeweza kuthibitisha kuwa minghairi ya manabii au makhalifa mtu aliweza kueleza jambo kutoka kwenye vitabu vya Mungu lililohusu dunia nzima na kwa karne na karne. Shirikisho la Ulaya lilishindwa kwa sababu ya kupinga mafundisho haya, nami nilikuwa nimekwishaashiria katika hotuba yangu **'Ahmadiyyat'** kwenye jambo hili kwamba kama mnataka kuunda Shirikisho la Mataifa, basi undeni kwa msingi huu uelezwao na Kurani Tukufu. Lakini wakati wa kuunda Shirikisho masharti haya hayakuzingatiwa, hivyo likashindwa.

## Sababu za Kushindwa kwa Shirikisho la Mataifa

Mwaka 1924 nilipoenda Uingereza, wakati ule Shirikisho la Mataifa lilikuwa liundwe muda kidogo hapo kabla, na Urusi na nchi nyingine zilikuwa zinaomba ziwe wanachama wake. Wakati huo niliandika kuwa Shirikisho hilo halitafanikiwa, na mambo ambayo nimeyaeleza sasa hivi niliyaeleza yote hayo kinaganaga katika hotuba yangu na nikasema kuwa Shirikisho haliwezai asilani kufanikiwa bila kuzingatiwa kanuni hizo tano. Shirikisho litakaloundwa kwa kuzingatia mafundisho ya Kurani Tukufu ndilo litakalofanikiwa, sio lile ambalo linahitaji msaada wa watu kwa kubaki. Basi, niliandika:

> "Kama kasoro hizo tano ziondolewe, Shirikisho la Mataifa litakuwa kama lililosemwa na Kurani

> Tukufu na hili ndilo Shirikisho liwezalo kufaa, si lile ambalo liwe linategemea kusaidiwa na watu ili lijistawishe".[27]

Kadhalia niliandika:

> "Fujo haitakwisha mpaka watu wapate kuelewe kama ifundishavyo Islam kuwa sisi sote tunatokana na asili moja, na kupata maendeleo na kuporomoka ni kitu kinachohusiana na mataifa yote. Hakuna kaumu yoyote iliyoendelea kuwa katika hali moja tangu mwanzo wala haitaendelea hivyo siku zijazo. Watu wapaswa kukumbuka kwamba 'volikano' zinazoyapindua mataifa juu chini bado hazijamalizika duniani. Kawaida ya asili inaendelea kufanya kazi kama ilivyokuwa ikifanya hapo awali. Hivyo, kaumu ile iitendeayo kaumu nyingine kwa chuki, basi kaumu hiyo inaanzisha silsila ya dhuluma isiyo na kikomo."[28]

Wakati walipoanzisha Shirikisho la Mataifa, walifurahi kupita kiasi, lakini mimi niliwasisitizia kwamba msipoweka sharti hili kwamba ile serikali itakayofanya kosa basi nchi zote zitaungana kuipiga vita, basi amani haitaweza kustawi. Lakini ikasemwa wakati huo kuwa hilo haliwezekani, kwani kufanya hivyo ni kuweka msingi wa vita badala ya suluhu. Na mipango yote iliyopangwa kwa kuleta nidhamu mpya si tu iliipinga

kanuni hii bali ilizipinga kanuni zitolewazo na Islam. Lakini sasa baada ya kuhangaika kwa miaka ishirini na miwili, wameelekea kwenye njia ielezwayo mapema na Islam, na makala zinaandikwa kwamba wakati wa kuunda Shirikisho jipya, sharti hili litawekwa kwamba kama kuna serikali ambayo itakataa kukubali suluhu, basi itapigwa vita na mataifa yote, lakini sasa pia mtaona kwamba kama hawatafuata nidhamu ya Kiislamu kikamilifu, basi watashindwa.

## Amri Nne ndani ya Islam kwa ajili ya Kuondoa Matatizo ya Maskini

Kanuni hizi ni kwa kuleta amani ya kitaifa na bila ya kuwepo suluhu ya kimataifa, suluhu ya ndani haileti manufaa yoyote. Lakini kwa kuwa pamoja na suluhu baina ya mataifa, marekebisho ya ndani pia ni muhimu, hivyo sasa naeleza kuwa Islam imependekeza njia zipi kwa ajili ya kuleta marekebisho ya ndani.

## Amri ya Kwanza: Ugawaji wa Mirathi

Kwa kusudio hili, Islam imeimarisha nadharia nne na makusudio ya zote hizo nne ni kwamba shida za maskini ziondoke. Kama ikitafakariwa, sababu kubwa ya kutokea uharibifu ndani ya utamaduni ni hii kwamba rasilimali huwa hazigawanywi, matokeo huwa kwamba zinabakia ndani ya miliki ya watu wachache na maskini wanakuwa hawapati fursa ya kuzalisha mali. Kwa kuiondoa kasoro hii, Islam imetoa agizo la

kugawanya mirathi. Hivyo, sawa na maamrisho ya Islam, mali ya kila anayefariki hugawanywa katika warithi wake; na mama, baba, watoto, mume, mke, ilmuradi kila mwenye haki hupata haki yake aliyowekewa. Na mtu yeyote hana hiari ya kubadilisha apendavyo mgawanyo huu. Bali, Kurani Tukufu inatoa mwongozo huu kwamba kama hamtaigawa mali kwa njia hii, basi mtakuwa ni wenye dhambi. Dini zingine zilizopo, miongoni mwao zipo zenye kumtambua tu mtoto wa kwanza wa kiume kuwa ndiye mrithi, na zingine humtambua mwingine. Imeandikwa ndani ya *Manu* — kitabu cha Wahidnu — kwamba urithi wapewe tu wana, wasipewe mabinti. Matokeo yalikuwa ni kwamba mali zote zilikuwa zikimilikiwa na mtu mmoja au watu wachache na maskini walikuwa wakikosa fursa ya kupata maendeleo. Islam inasema kwamba msipoeneza utajiri wenu baina ya watu , kaumu haitaweza kupata maendeleo. Hebu tazameni, kama mtu ana rupia laki moja, naye ana watoto kumi, basi kila mmoja atapata rupia elfu kumi kumi. Kama watoto hao kila mmoja awe na watoto watatu au wanne, basi kiasi hicho cha fedha cha rupia elfu kumi, kitakuja kuwa rupia elfu mbili mia tano hadi elfu tatu kwa kila mmoja. Na kwa njia hii, kwa kujichumia mali itawabidi wote wafanye juhudi upya. Haitakuwa kwamba wakae tu wakitegemea mali za mababu zao. Na sio tu kwamba watakuwa hawafai bali watazuia mali yao

isizunguke baina ya watu. Waingereza waliweka sharti hili kwamba wakati wa kugawa ardhi katika vijiji vipya vya Panjab kwamba mwana mkubwa tu anaweza kuwa mrithi wao. Lakini, sasa wameliondoa sharti hili.

## Amri ya Pili: Kukataza Kuhodhi Fedha

Pili, Islam imezuia ulimbikizaji wa fedha, yaani haitaki kwamba fedha zisizunguke baina ya watu, bali inalazimisha kwamba ama watu wazitumie fedha au kuziwekeza katika shughuli fulani, kwani katika sura zote hizo mbili fedha zitakuwa zinazunguka na watu watapata faida. Lakini mtu asipofanya hivyo, basi kumhusu yeye Islam inatoa onyo hili kwamba yeye atapata adhabu kutoka kwa Mwenyezi Mungu siku ya Kiama. Allah Anasema kwamba zile dhahabu na fedha atakazozilimbikiza mtu duniani, hizo zitatiwa katika moto siku ya kiama na mtu huyo atachomwa nazo zikiwa moto-moto. Katika hukumu hii kuna hekima hii hii kwamba kama watu watalimbikiza dhahabu na fedha, basi maskini hawatapata kazi. Lakini kama fedha hizo watazitumikisha basi wale watu watakaokuwa wakizifanyia shughuli watapata faida. Vivyo hivyo baadhi ya watu watafaidika kama wafanyakazi na vibarua. Kwa mfano, kama yeye atajenga jengo, basi ingawa jengo hilo atajijengea, lakini kutokana na kuzitumia fedha, watu wengi watapata ajira. Kwa kawaida Islam inakataza kupoteza mali kwa kujenga

majengo yasiyo na kazi, lakini, kwa vyovyote, kama asijenge majengo pasipo faida yoyote, bali ajenge kwa ajili ya faida yake mwenyewe, hapo pia wahunzi maseremala, vibarua na watu wengine wengi watapata ajira. Lakini kama asifanye hivyo, bali aanze kutengeneza mapambo ya dhahbu na fedha na aanze kulimbikiza nyumbani, basi hiyo haitawafaidisha wengine chochote. Hivyo, Islam inakataza kulimbikiza fedha. Halikadhalika haipendelei kuwatengenezea mapambo mengi wanawake. Inajuzu kuwatengenezea mapambo kiasi kidogo.

## Amri ya Tatu: Ukatazaji wa Riba

Tatu, Islam inakataza riba. Riba pia ni kitu kinachoivutia fedha kwake. Kupitia hiyo, wale wafanyabiashara ambao tangu mwanzo wameishajijengea itibari na ambao wakati fulani hawana mtaji wowote, huchukua kwa urahisi kutoka benki kiasi chochote cha fedha anachokihitaji. Au mtu fulani mwenye mtaji kidogo, lakini ana akili yake nzuri sana, akifanya urafiki na katibu au Raisi wa benki fulani, huchukua toka kwake rupia laki moja au mbili, na kwa muda mchache tu anakuwa na laki kumi kutokana na hizo laki mbili, na kisha baada ya miaka michache anakuwa bilionea. Kutokana na hali hii dunia pia hupata hasara kubwa sana. Wakulima wa nchi yetu wanafahamu vyema kwamba ni kiasi gani cha mali zao huenda kwa

wakopeshaji wa Kibaniani. Kama wangeweza kumudu bila ya riba, basi hali ya kifedha ya kila familia ya mkulima ingekuwa bora mno kuliko ilivyo leo. Lakini kutokana na riba, kama mkulima achukue mkopo wa rupia elfu mbili kutoka kwa mkopeshaji wa Kibaniani, basi ndani ya miaka michache, wakati mwingine hulipa riba ya rupia hadi elfu kumi. Lakini zile rupia elfu mbili alizozikopa, hizo huendelea kubakia vile vile. Hivyo riba ni laana kubwa sana inayowatawala wanadamu. Hiyo ni ruba inayofyonza damu ya maskini. Kama dunia inataka kuwa na amani, basi njia yake ni hii hii kwamba riba ifutwe duniani, na hivyo utajiri usikusanywe kwenye mikono ya watu wachache.

## Amri ya Nne: Kutoa zaka na Sadaka

Swali linazuka sasa kwamba bila shaka Islam kwa upande mmoja hairuhusu fedha kulimbikizwa kwa mtu mmoja, bali inaigawa, na upande wa pili inakataza kulimbikiza mali, lakini kwa njia hii umaskini hauondolewi. Jibu la swali hilo ni kwamba Islam imetoa amri ya nne ya kutoa zaka na sadaka kwa ajili ya kutoa haki za maskini. Yaani kiasi chochote cha mali alicho nacho mwanadamu, iwe dhahabu, sarafu za fedha au aina za mali ya biashara na ambazo zimepitisha mwaka, basi ni lazima kwamba serikali ichukue kutoka kwake kodi ya asilimia mbili na nusu kwa mwaka na kuziingiza ndani ya hazina ya serikali na zitumike kwa maskini wa

nchini. Kodi hii inayoitwa zaka haichukuliwi tu kutoka kwenye kipato, bali hutozwa kwa kuchanganya vyote, mtaji na faida. Na kwa njia hii asilimia mbili na nusu wakati mwingine inakuwa asilimia hamsini ya faida na pengine zaidi ya hiyo. Kulingana na hukumu hii, mtu ambaye nyumbani mwake rupia mia moja zitakusanyika, yeye baada ya kupita mwaka atalazimika kulipa zaka ya asilimia mbili na nusu, hapo atakerwa na jambo hili kwamba kama fedha hizi zikikaa hivyo, basi baada ya muda mfupi tu fedha zote zitamalizika kwa kuzilipia kodi. Hivyo, mara moja yeye ataziwekeza fedha katika biashara ili kujaza iliyopungua. Na atakapowekeza katika biashara, basi fedha hizo zitapata kuzunguka. Na hivyo mbali na maskini kupata asilimia mbili na nusu toka kwenye fedha zake, ile hasara iliyoweza kupatikana kwa kulimbikiza fedha, haitaipata nchi wala kaumu. Siku hizi maradhi haya yameanza kuzuka miongoni mwa watu kwamba wanakusanya dhahabu na fedha na kuzilimbikiza. Maskini wana mahitaji ya aina mbali mbali. Nao pia wanafahamu kwamba siku hizi dhahabu ni ghali. Kwa kutimiza mahitaji yao wanafikiria kwamba wauze mapambo. Matokeo ni kwamba yuko anayeuza pete, yuko anayeziuza hereni, yuko anayeuza mkufu, yuko anayeuza furungu. Lakini je mnafahamu kwamba dhahabu na fedha hizi hukusanyika wapi? Zote hizi zaenda nyumbani mwa wafanyabiashara wa Kibaniani.

Na baadhi ya watu hukusanya dhahabu na fedha kutokana na hofu hii kwamba kama Mjapani akiiteka India basi noti zitakuwa hazina thamani. Wao hawafahamu kwamba Japani ikija kutawala, noti hazitafaa. Hawajui kuwa ikija Japani, kwanza kabisa itazipora hizo hizo dhahabu na fedha. Lakini hao wanadhani kwamba dhahabu zitabakia tu majumbani mwao na wale wenye kuwa na noti hawatabakiwa na chochote. Ndio sababu siku hadi siku dhahabu inaendelea kupanda bei. Ilianza kupanda bei toka rupia arobaini na sasa imeshafikia hadi rupia sabini. Nami nimewasikia wafanyabiashara wa Kibaniani wakisema kwamba sisi tuna mpango wa kuongeza bei hadi kufikia rupia mia moja. Lakini Islam inasema kwamba kwanza msilimbikize mali na kama mkilimbikiza basi mlipe kodi yetu ya asilimia mbili na nusu. Kwa njia hii Islam inazirejesha tena fedha zilizolimbikizwa kwa maskini ili wapate kufaidika nazo. Na inalazimisha kwamba watu wazisambaze fedha zao na waendelee kuzisambaza. Kama amri za Kiislamu zitekelezwe, basi dunia itafaidika na fedha za hata bahili wa kupindukia, na maskini watapata ajira na zaidi ya hiyo asilmia mbili na nusu ya fedha zitapatikana.

## Hifadhi ya Haki ya Kumiliki Mali Binafsi Ndani ya Islam

Lakini yapaswa kukumbukwa kwamba ingawa Islam imesema kuwa mali ni haki ya wote, haikukataza haki ya

mtu kumiliki mali binafsi, bali imeikubali. Hata hivyo mwenye kuimiliki atakuwa kama wakala. Na isitoshe, ile nguvu aipatayo kutokana na kuimiliki mali hiyo, Islam imeidhoofisha kwa mbinu zinazofaa, kama vile inavyodhihirika katika amri za hapo juu.

## Sababu ya Kuipendelea Nidhamu ya Kiislamu Kuliko Ile ya Kibolsheviki

Hapa swali hili lazuka kwamba kwa nini nidhamu ya Kibolsheviki isipendelewe kuliko nidhamu hii? Jibu lake ni hili kwamba lengo hasa la nidhamu huwa ni kustawisha amani, uadilifu na roho ya maendeleo. Lakini nidhamu ya Kibolsheviki huleta mabadiliko ya haraka sana ambayo huihasiri isiyovumilika sehemu fulani ya wenye nguvu katika nchi nao huwa tayari kupambana nayo. Kwa mfano, kusema kwamba ichukueni nyumba ya kila mwenye mali, inyang'anyeni raslimali yake, itwaeni mali yake, hii humpatia mwanadamu uchungu asioweza kuvumilia. Hivyo, Urusi inapingwa zaidi na Waursi wenyewe kuliko wengine; na katika kila nchi wapo Warusi wenye kuipinga vikali nidhamu hii. Mimi binafsi nimewaona Warusi katika safari yangu ya Ulaya walio maadui wa kupindukia wa serikali ya Urusi. Na sababu yake ni hii hii tu kwamba hao walikuwa wakiishi kwa utulivu ndani ya nyumba zao, ghafla wakaja wawakilishi wa serikali na kupora malalo yao na vitanda vyao na vifaa vingine, wakawatoa

majumbani, wakazitwaa mali na vitu vyao na wakapokonya miliki yao. Ni sawa kwamba chochote walichokichuma ndani yake kulikuwemo na haki za wengine, lakini walikuwa wameshazoea, vizazi hata vizazi, kwamba hivi vyote ni vyetu. Kwa hiyo, miliki na raslimali zao zilipochukuliwa kwa nguvu, wakaona vibaya mno. Ni kutokana na sababu hii hii Mtume[sas] alisema kwamba hatutaufuta umiliki wa hapo awali. Yaani hatutawafanyia namna ambayo wafikirie kwamba sisi tunadhulumiwa.

## Ubolsheviki Umepuuza Jambo Hili kwamba Akili pia ni Mtaji

Pili, nidhamu ya Kibolsheviki inalipuuza jambo hili kwamba kama vile mali ilivyo ni mtaji, akili nayo ni mtaji, na nidhamu hii inawezaje kuugawanya mtaji huu. Mfumo huu unauangamiza kabisa uwezo wa kipaji cha akili, kwani hiyo inakiona kipaji cha akili kuwa hakina thamani kama ilivyo thamani ya kufanya kazi kwa mikono. Na hii ni kanuni ya asili kwamba kile kitu kisicho na thamani nchini, basi huwa kinaanza kuporomoka. Wale watu ambao kwao fedha haina thamnai yoyote, fehea zao huangamia. Na wale ambao kwao rasilimali hazina thamani yoyote, rasilimali zao huangamia. Halikadhalika wale ambao kwao kipaji cha akili hakina thamani yoyote kipaji chao huanza kuzorota. Hivyo ndani ya nidhamu ya Ubolsheviki hii ni

kasoro kubwa sana kwamba mali wanaitambua kuwa ndio mtaji lakini akili hawaitambui kuwa ni mtaji. Kwa sababu yanaweza kuigawa mali lakini haiwezi kuigawa akili, na hivyo sawa na kanuni zake akili inakuwa haina thamani, na kwa sababu hii siku moja ukuaji wa akili utaathirika. Lakini Islam inasonga mbele hatua kwa hatua. Haileti mabadiliko mara moja, bali kwa huba na upendo inatoa amri ya kuwapa watu kila aina ya mtaji. Na kwa njia hii inazigawa zote, mali na akili. Uthibitisho wa tabia ya asili pia unapingana na kanuni za Kibolsheviki. Kawani, asili hutoa nguvu nyingi za akili kwa baadhi ya watu na kidogo kwa wengi. Lakini baada ya hayo unastawishwa uadilifu kwa njia hii kwamba wale waliopata vipawa vingi vya akili wanaamrishwa na dini kwamba wavitumie hivyo pia kwa kuwatumikia wanadamu. Hivyo, Kurani Tukufu inasema: 'Na hutoa katika vile Tulivyowapa.[29] Yaani, waaminio na wach-Mungu wa kweli ni watu ambao chochote walichopata kutoka kwa Allah, ni ubongo, au nguvu ya mwili, au mali au akili, avitumie hivyo katika kuwahudumia viumbe wengine. Na kadhalika Islam hutenda hivyo hivyo kuhusiana na mali, inaigawanaya. Lakini sio kwa kulazimisha na kwa kudhulumu kama ilivyo katika Ubolsheviki, bali huigawanya mali kwa mikono ya hao hao wenye kuimiliki mali, kama vile huwafikishia faida ya akili ya wenye vipawa vya kiakili wenyewe. Kwa njia

hii, faida pia hupatikana na mbegu ya uadui pia haipandwi mioyoni.

## Utendaji Usio wa Uadilifu chini ya Ubolsheviki

Ninasema pia kwamba hata sasa Ubolsheviki haujaweza kufanaya uadilifu barabara. Hata sasa bado kuna tofauti kati ya wakubwa wao na wadogo wao. Hata sasa kuna tofauti kati ya matajiri wao na maskini wao. Na hata sasa kuna tofauti kati ya vyakula vyao. Je kuna mtu awezaye kusema kwamba chakula cha Stalin na cha watu wa vijiji vya huko ni cha namna moja? Halikadhalika katika karamu za kifalme hutumiwa fedha nyingi kupita kiasi. Mnamo siku chache zilizopita, Bwana Wendell Wallkie, alipoenda huko, yakachapishwa maelezo ya karamu moja ya kifalme ambamo mlitajwa kwamba vyakula vya aina sitini vilitayarishwa katika chakula rasmi cha jioni, na Stalin na watu wengine walioshiriki katika karamu hiyo wakala chakula hicho. Kama kweli usawa unapatikana huko na hakuna tofauti yoyote kati ya wakubwa na wadogo, basi kulingana na kanuni za Kibolsheviki, kila mwenyeji wa Moscow anaweza kusema kwamba mimi napaswa kupata vyakula vya aina sitini. Na sio tu kila mwenyeji wa Moscow, bali wenyeji milioni 170 wa nchi nzima wana haki ya kusema kwamba sisi pia tuna haki ya kupata vyote hivi. Lakini, je hii yawezekana? Kama

mseme kwamba hii haiwezekani, basi jibu hili hili linapaswa kufahamika kwenye ugawanyaji mwingine. Kama tofauti zinalazimika kubaki, kwa nini kuleta fujo katika kuondoa hizo tofauti. Kwa nini tusiiondoe kasoro hii kwa njia iliyo bora.

### Ubolsheviki Kuamua kuwa Vipawa vya Akili Havina Thamani na Matokeo yake

Halafu matokeo mengine ya nidhamu ya sasa ya Kibolsheviki yatakuwa kwamba kwa kuwa hiyo haikithamini kipawa cha akili pekee, bila ya kufanya kazi ya mikono, kwa hiyo, ingawa athari yake haidhihiriki wakati huu, lakini baada ya kupita muda wavumbuzi Warusi watakapoona kwamba kipawa chao cha akili hakithaminiwi basi wataenda ujerumani au Amerika au Uingereza au nchi zingine kwa kisingizio cha kutalii na baada ya kwenda huko watausajili uvumbuzi wao huko. Hawataishi Urusi, kwa sababu chini ya mfumo huu hawawezi kunufaika na vumbuzi huo. Hivyo, matokeo yatakuwa kwamba nchi nyingine zitanufaika na vipawa vya akili vya watu wenye ubongo bora lakini Urusi haitanufaika. Na polepole, wote hao wataenda nchi zingine. Wakati huu, kukubalika kwa mfumo wa Kibolsheviki ni kama fundisho hili la Injili kwamba kama mtu akupigaye shavu moja, umgeuzie na la pili. Fundisho hili liishiapo mazungumzo tu, lapendeza masikioni, lakini ukija wakati wa kulitekeleza, basi

hakuna mtu yeyote awezaye kulitekeleza. Hili ni tukio fulani la kihistoria kwamba katika mtaa mmoja wa maduku huko Cairo kulikuwa na Padri fulani aliyeanza kutoa hotuba kila siku kwamba mafundisho ya Yesu Masihi yamejaa upendo. Kwani anasema kwamba kama ukipigwa kofi shavu moja basi umgeuzie la pili pia. Lakini katika dini zingine kuna dhuluma hii na ile. Ilmuradi, alikuwa akitoa hotuba kwa namna ambavyo watu walikuwa wakitokwa na machozi. Mwislamu mmoja alikuwa kila siku akiisikiliza hotuba yake na alikuwa anateseka moyoni mwake kwamba kwa nini Sheikh yeyote hamjibu Padri huyu. Hatimaye baada ya muda fulani alipoona kwamba watu wanaathirika vibaya, basi siku moja, wakati Padri yule alipokuwa akitoa mawaidha, alimuendea na kumwambia: Bwana Padri! Ninataka nikuambie jambo fulani. Kwa ajili ya kumsikiliza, yeye akamuinamishia kichwa mtu huyo na kumwambia: Sema unachotaka kusema. Badala ya kusema neno lolote, aliinua mkono na kumzaba usoni. Kwanza Padri alisita lakini kisha akafikiri isije akanizaba kibao kingine. Hapo naye pia akainua mkono wake kwa kumpiga. Bwana yule akamwambia Padri: Bwana wafanya nini? Fundisho lako ni hili kwamba kama mtu akikupiga kofi shavu moja basi umgeuzie na la pili. Mimi nilikuwa tu nikisubiri kwamba utanigeuzia na shavu la pili, Lakini wewe unateremka kuja kupambana.

Akasema leo sitotekeleza fundisho la Injili, bali nitalitekeleza fundisho la Nabii wako.

## Hatari ya Kutokea Uasi Nchini Kutokana na Ubolsheviki

Hivyo, baadhi ya mafundisho yanavutia sana yanaposemwa lakini kiutendaji ni mabovu sana. Halikadhalika haipaswi kutia maanani mfumo wa sasa wa Kibolsheviki. Wakati huu bado wanazikumbuka dhuluma za Tzar – matamshi yake Zaar. Siku wazo hili litakaposahaulika mioyoni mwao, basi hisia hii ya asili kwamba tunapaswa kupata malipo ya huduma tuzitoazo itazalika mioyoni mwao. Kizazi kipya kitaasi na ubaya wa fundisho hili utadhihirika kiasi ya kwamba dunia nzima itastaajabu. Lakini ndani ya mfumo wa Kiislamu hakuna uwezekano wowote wa uasi. Yawezekana uwe uvivu, kwani hilo ni jambo la tabia asili.

## Haja ya Serikali Kuwa na Mamlaka juu ya Mali za Nchi

Sasa ninakuja kwenye swali hili la muhimu ambalo kwa hakika ndio msingi wa madhumuni yangu, lakini kabla ya hapo limebakia swali moja ambalo hakuna budi kulijibu, nalo ni hili kwamba kutokana na mifumo yote mipya iliyoelezwa hapo juu, tumefikia kwenye natija hii kwamba mifumo yote, juu ya kuhitilafiana, inaafikiana katika jambo hili kwamba serikali inapaswa kuwa na mamlaka makubwa juu ya mali ya nchi. Kodi za zamani

hazikuweza kuitimiza mpango uliomo ndani ya fikara za wenye mifumo hiyo. Nao wanataka kwamba kodi mpya zitozwe. Njia mpya zivumbuliwe ili mali ya matajiri itolewe mikononi mwao na kuweza kugawanywa miongoni mwa maskini. Wanasema kama lengo ni kutimiza mahitaji ya maskini, basi itabidi kodi ziongezwe. Kutokana na kodi za sasa tatizo hili haliwezi kutatulika. Sasa swali ni hili kwamba Islam imeshika njia gani kuhusiana na jambo hili.

Wao wanasema: Ninyi mmetoa fundisho la zaka, lakini je, kwa rai yenu, zakati inaweza kutimiza kusudio hili kwamba kila maskini apate nguo, kila maskini apate chakula, kila maskini apate maskani na kila maskini apate dawa. Jibu langu la uaminifu ni hili kwamba hapana. Yaani, jibu langu la uaminifu ni hili kwamba kulingana na zama hizi kwa yakini serikali inapaswa kuwa na fedha zaidi ya zile ambazo ilikuwa nazo hapo kabla kwa mfumo wa zaka na kadhalika. Hapo kabla, serikali ilikuwa na majukumu haya tu kwamba baada ya kukusanya kodi, itengeneze barabara, ijenge hospitali, ijenge shule, iweke majeshi, na kadhalika kwa ajili ya ustawi wa raia ifanye mipango mingine. Lakini sasa kuna jukumu lingine linalobebwa na serikali kwamba dunia imeishaona kuwa haikuweza kuwalisha maskini, dunia imeishaona kuwa haikuwezi kuwatimizia mahitaji yao hayo, dunia

ilijitahidi kuwapatia dawa lakini haikuweza kufanikiwa katika jambo hili. Sasa inadaiwa kwamba mahitaji yote haya pia yatimizwe na serikali. Serikali impatie kila mtu nguo kwa ajili ya kuvuaa, chakula kwa ajili ya kula, nyumba kwa ajili ya kuishi na itoe dawa ya kuponya maradhi. Na Isalm pia inakubali kwamba shughuli zote hizi ni jukumu l serikali. Hivyo, kama imeisha kubaliwa kwamba shughuli hizi zinapaswa kufanywa na serikali na Islam pia inapokubali hayo, basi ni sawa kwamba ama Islam ituambie kwamba fedha za zaka zinaweza kutimiza mahitaji yote hayo, au zaidi ya zaka utatuzi mwingine wa taabu hii uletwe uliotolewa na Islam.

## Kuwatimizia Maskini Mahitaji yao Kuna Haja ya Michango Mingine Mbali na Zaka

Hili ni swali muhimu ambalo huzalika kwa wakati kama huu na kulitafakari ni muhimu sana kwetu. Kama tusingekuwa tunadai kwamba Islam imeibebesha serikali majukumu ya kutimiza mahitaji hayo kusingezuka swali hili. Lakini tunapokubali kwamba Islam ndiyo ile dini iliyotoa fundisho hili kwamba yapasa kustawishwa usawa wa kweli kati ya maskini na tajiri na wote hao wawili wanapaswa kukurubishwa kwa kiasi hiki kwamba wasihisi kwamba huyo ni kiumbe mwingine na yule ni kiumbe mwingine. Bali kama vile matajiri wanavyotimiza mahitaji yao, vivyo hivyo maskini nao

wayatimize mahitaji yao, wasiishi bila ya kutibiwa, wasiishi na njaa, wasikose mavazi, wasibaki kuwa majahili, wasiishi bila ya nyumba, hapo hakuna budi kwamba tatizo hili litatuliwe kwa mafundisho ya Islam tu. Islam iliamuru kutoa zaka, lakini nimeshakubali kwamba zaka sio utatuzi kamili wa tatizo hili. Basi, swali linazuka kwamba Islam inatoa ushauri gani wa kuiondoa kasoro hii.

## Sawa na Nadharia ya Ujamaa Njia ya Kwanza ya Kuwatimizia Maskini Mahitaji yao, na Kuthibitisha kuwa Hii siyo Sahihi

Ujamaa unasema kwamba njia yake ni kwamba wafanyakazi nao wawe na hisa kwenye faida ipatikanayo, isiwe tu kwamba wapewe mshahara kila mwezi, baadhi yao kupewa kidogo na wengine zaidi, bali tegemeo liwe ni faida iliyopatikana. Yaani, ipatikanapo faida, basi iamuliwe kwamba safari hii tumepata kipato kadhaa, na katika hicho mmiliki apewe hisa kadhaa na wafanyakazi wapewe hisa kadhaa. Lakini ni dhahiri kwamba njia hii ni potovu, kwa sababu katika biashara fulani faida itakuwa kidogo na katika biashara nyingie itakuwa zaidi. Kila siku tunaona duniani kwamba kunakuwa na wafanyabiashara wawili wa nafaka, mmoja wao anakaa kutwa nzima bure pasipo kupata mnumizi na mwingine kila siku anajaza sefu yake na kuileta nyumbani. Mtu mmoja anauza nguo, basi kila

siku anauza hata majora 200 na mwingine hufanya kazi hiyo hiyo na siku nzima anashindwa kuuza hata jora moja. Hivyo, kutokana na tofauti hii matokeo yatakuwa kwamba wafanyakazi wa mfanyabiashara fualni watakuwa na kipato zaidi kwa kazi ya aina ile ile na wafanyakazi wa mwingine watapata kidogo. Yaani, wafanyakazi wa mfanyabiashara hodari watakuwa na kipato zaidi na wafanyakazi wa wengine watakuwa na kipato pungufu. Hivyo, mgawanyo huu utakuwa umepingana kabisa na akili. Itakuwa na maana kwamba kwanza kipato kilikuwa kikitegemea kipaji cha mtu kisha kitakuwa kikitegemea kamari na bahati, na halafu watu watagombania kufanya kazi katika karakana ya fulani na kutofanya katika kurakana ya mwingie. Sasa ni nani atakayetoa uamuzi kwamba wafanyakazi fulani wafanye kazi wapi. Kama ikisemwa kuwa Ujamaa utaandaa mpango na kukadiria kwa wafanyakazi wa karakona zote wawe na kiasi bora cha mshahar, hata hivyo yule mfanayabiashara mahiri atapata faida zaidi kuliko ile iliyopendekezwa na Ujamaa, na mfanyabiashara mwingine atakuwa kwenye hasara. Na hivyo ujamaa tena utakuwa utashindwa katika mpango wake na wale ambao biashara zao hazitoenda vizuri, wafanyakazi wao watakula hata mtaji kwa kukosa faida. Jambo la asili ni kwamba kuna njia mbili zenye kufaa za kupatia riziki: 1. Uhodari 2. Mahitaji kwa akali ya kuishi. Lakini njia zote

hizi mbili zilizotajwa hazipatikani ndani ya mfumo wa kijamaa uliotajwa hapo juu.

## Njia ya Pili ya Kutimiza Mahitaji ya Maskini

Sura ya pili inayotolewa na Ujamaa ni hii kwamba tasnia zote za muhimu zimilikiwe na serikali, mathalan, Reli, Machimbo ya Madini, Umeme n.k. Kadhalika biashara muhimu zikiritimbwe na serikali na ziwe mikononi mwake. Lakini hiyo nayo inalaumiwa kwa namna mbalimbali. Mathalani, mfumo huu hauwezi kuwa wa kimataifa, bali utakuwa kivyake katika kila nchi, ilhali swali lilikuwa kwamba mpango ufanywe kwa wenye njaa duniani kote, kwa walio rabana duniani kote, kwa wagonjwa duniani kote, kwa majahili duniani kote na kwa mahawinde duniani kote. Lakini kwa njia hii hawataondolewa shida wenye mahitaji wa dunia nzima. Kila serikali inawaagalia tu masikini wa nchi yake. Kwa hiyo, mfumo huu sio wa kimataifa. Pili, kwa mfano, hutolewa lawama hii kwamba hata ndani yake pia nafasi ya kudhihirisha kipawa binafsi inakuwa finyu, na kwa njia hii mwili tu unatiliwa maanani lakini akili ambayo ni yenye thamani zaidi hupatwa na madhara.

## Mpango wa Hitler na Goering Kukusanya Mchango kwa Mahitaji ya Maskini

Siuelewi mpango huu kinaganaga wa Ujamaa wa Kitaifa, lakini ninauelewa mpango huu wa Hitler[30] na Goering[31] kwamba wenye mtaji watoao hisa kubwa kwenye

huduma ya kitaifa, hao wapewe sehemu kubwa ya msaada wa serikali. Wanasema kwamba wale watakaoichangia zaidi serikali fedha na kushiriki kwa moyo mkunjufu katika shughuli za kitaifa, hao wataangaliwa zaidi na watapatiwa kondarati n.k. Lakini mfumo huu pia sio kamili, kwani kwa njia hii pia mtaji kamili unaotosheleza hauwezi kukusanywa, na pia humo kwamba jukumu kiasi gani la mahitaji ya nchi litakuwa juu ya serikali.

## Mipango ya Kuondoa Shida za Maskini Kwa Mtazamo wa Nadharia ya Kibolsheviki

Mpango ya Kibolsheviki ni kwamba biashara na viwanda vyote muhimu vimilikiwe na serikali, na serikali iyachukue kwa nguvu mapato yote ya ziada ya mkulima. Mali zote za matajiri zinyang'anywe. Lawama zitolewazo kwa hali hii nimeshazieleza hapo awali. Muhtasari ni huu kwamba kutokana na hayo vipawa vya mtu mmoja mmoja vitaangamia kabisa, na utawala wa aina hii utakapodhoofika, humo hayatazalika mageuzi kidogo bali utawala kama wa Tzar ndio utakaoibuka. Uzoefu wa huko Ufaransa unatoa ushahidi. Ukoo wa Bourbon Ulianzisha utawala huria (utawala wa umma ulio tofauti na jamhuri), na Utawala huria ukazaa katili kama Bonaparte.[32] Halikadalika Tzar alianzisha Ubolsheviki na akaufanikisha. Na Ubolsheviki ukidhoofika baada ya muda mfupia utazaa tena katili mwingie. Kadhalia mna

kasoro hii ndani ya Ubolsheviki kwamba umewafanya sehemu moja ya wananchi kuwa ni maadui bila ya sababu yoyote na kuanza kuwatendea kama maadui. Yaani imezifanya koo zote za zamani na watu wenye kutoa huduma ya kielimu kuwa maadui.

Mfumo wa Islam umetofautiana na mifumo yote hiyo. Kwanza Islam imetoa nadharia hii kupingana na mifumo yote hiyo mitatu, kwamba utulivu hauna maana ile msemayo, yaani nyie mnatoa maana hii ya utulivu wa maisha kwamba mambo ya anasa yapatikane kwa watu wote, njia za kwenda sinema ziwe wazi kwa wote, kutazama michezo na tamasha kuwezekane kwa wote. Lakini Islam imechukua maana hii ya utulivu kwamba hata matajiri pia wasiachiwe nafasi ya kuwa na mambo ya anasa, na kwa njia hii wanadamu waletwe kwenye usawa. Kusudio lenyewe hasa ni utulivu. Lakini Islam, pamoja na utulivu, inataka pia kuinua kiwango cha khulka na mwenendo bora. Kisha kuhusiana na utulivu, kuna tofauti hii pia kati ya nadharia ya Kiislamu na ya mifumo hii kwamba hao walitaka kuupata utulivu kwa kuviongeza vitu vya anasa na Islam inasema kwamba tutakupatieni tu mahitaji ya lazima hatutakupeni vitu vya anasa. Kana kwamba badala ya vitu vya anasa, Islam inapendekeza maisha ya kawaida kwa ajili ya wote, ndiyo sababu Islam imeharamisha muziki, dansi, pombe n.k. Huko Uingereza maskini wapigapo kelele na kusema kwamba tunayo shida kubwa, basi hutoa dalili hii kwamba sisi tulio maskini tunapata bilauri mbili tu za

kileo lakini mtu tajiri anakunywa hata bilauri kumi za kileo, na serikali ina wajibu kwamba madai yenu yanajuzu na ni sahihi, basi nanyi pia tutawapatieni bilauri kumi za pombe. Lakini Islam inasema kwamba tuondoe malalamiko yenu haya kwa njia hii kwamba tutawanyang'anyeni hizo bilauri zenu mbili na kuwanyanga'nya pia matajiri hizo bilauri zao kumi, kwa sababu vitu hivi vinadhuru mwili na roho.

Halikadhalika kama huko maskini wakilalamika kwa kusema kwamba hawa matajiri kila siku wanacheza dansi lakini sisi maskini hatuna njia yoyote ya kucheza dansi. Na serikali inasema: Vizuri, serikali yenyewe itawajengeeeni ukumbi wa dansi. Basi, huwaambia matajiri: Enye matajiri, toeni fedha ili tuwajengee ndugu zenu pia walio maskini nyumba ya dansi. Lakini Islam inasema: Hapana kabisa, uanadamu huangamia kwa kujenga nyumba ya dansi, nasi hatutaki ipatikane ila ndani ya uanadamu wenu. Hivyo, badala ya kuwajengeeni ukumbi wa dansi, tutazibomba kumbi za dansi za matajiri ili nao pia waingie ndani ya wigo wa uanadamu na wasiwe na harakati yoyote yenye kupingana na ustaarabu na utu.

## Islam Yaimarisha Usawa Baina ya Matajiri na Maskini kwa Kuvifutilia Mbali Vitu vya Anasa

Basi, vile vitu visivyo vya lazima katika maisha, bali ni miongoni mwa vitu vya anasa, Islam imeviondoa na kustawisha usawa kati ya maskini na matajiri. Na ni

dhahiri kwamba serikali zenye kutengeneza vitu vya anasa kwa ajili ya wote haziwezi kujizuia kuwapora majirani zao. Lakini serikali zenye kuhamasisha maisha ya kawaida kwa wote, badala ya kuwapora wengine, zitajaribu kuwafanya matajiri wake waishi maisha ya kawaida. Na hii pia ni dhahiri kwamba ni rahisi kuweka mipaka ya maisah ya kawaida, lakini ni vigumu sana kuyawekea mipaka maisah ya anasa. Hivyo kwa hakika mafundisho ya Islam, kwa yakini yapo karibu sana kiakili na mafanikio, na kwa nija hii, Islam, kwa kutumia kiasi kidogo tu cha fedha, itafanikiwa kuondoa hali ya mashaka ya maskini. Ilmuradi, serikali za siku hizi zinadhani kwamba maana ya utulivu ni kuwapa maskini vitu vya anasa, na Islam inasema kwamba maana ya utulivu ni kuwapa maskini mahitaji ya lazima na kuwanyang'anya vitu vya anasa wote matajiri kwa maskini. Hivyo kwa kiasi cha fedha Ukristo utaweza kuipa dunia utulivu, Islam itaweza kuipa dunia utulivu kwa kiasi kidogo sana cha fedha kuliko hicho. Hivyo, Islam imewakataza wanaume kuvaa nguo za hariri. Kadhalika hairuhusiwi kuweka majumbani vyombo vya dhahabu na fedha kwa kuvitumia. Imekatazwa kujenga majengo makubwa makubwa pasipo sababu na bila ya haja. Halikadhalika Islam imekataza kutengeneza mapambo mengi kwa ajili ya wanawake. Imezuia pombe, imeiharamisha kamari ili usizalike utashi

wenyewe mioyoni mwa maskini kupata vitu hiyvo, na kwa njia hii zile fedha zinazobakia wapewe maskini.

## Katika Islam Namna ya Kupata Michango ya Ziada kwa Moyo wa Upendo Mbali na Kodi za Lazima

Pendekezo la pili lililotolewa na Islam ni hili kwamba badala ya kuzifutilia mbali juhudi za mtu mmoja mmoja, imezistawisha; na badala ya kulazimisha, imetumia njia ya uhamasishaji  kwa kuchukua mali ya ziada kutoka kwa matajiri mbali na kodi za lazima. Na ni dhahiri kwamba kuna madhara pia kwa kuzifuta juhudi za mtu mmoja mmoja, kwani kwa hiyo jadhba kubwa za kiukoo na maendeleo ya kielimu hufutika. Na kuchukua kwa nguvu pia kuna madhara. Kama kuwepo na mfumo wa aina hii kwamba juhudi za mtu mmoja mmoja pia ziwepo na mali ya ziada ichukuliwe kwa kuhimiza na kuhamasisha, hapo mfumo huo huo utakuwa njia ya kuleta ustawi na amani duniani, kuleta utulivu kwa ajili ya wote na kuongeza huba na upendo miongoni mwa watu. Ndivyo Islam ifanyavyo hivyo. Ndani ya mifumo isiyo ya Kiislamu kuna kanuni hii kwamba uzichukue kwa nguvu mali za ziada zilizopo kwa kila mtu. Lakini Islam inasema kwamba usimlazimishe yeyote yule. Zile kodi za lazima mzichukue kwa nguvu, lakini msitumie nguvu kuzichukua mali za ziada kutoka kwa matajiri, bali tumieni kuhimiza na kuhamasisha. Faida yake

itakuwa kwamba yatazalika mapenzi ya maskini ndani ya mioyo ya matajiri, na ndani ya mioyo ya maskini mapenzi ya matajiri. Kama serikali ichukue kwa nguvu mali kutoka kwa mtu, hapo ndani ya moyo wake hamtakuwa na mapenzi kwa wengine wala hatopendeka ndani ya mioyo ya watu wengine. Lakini kama mtu kwa upendo wake akitoa mali kwa ajili ya kuwastawisha watu, hapo ndani ya moyo wake pia kutakuwa na mapenzi ya wengine na pia atapendwa mioyoni mwa wengine. Kwa njia hii fungamano la kibinadamu litaendelea kuimarika katika jamii.

## Faida za Kuimarisha Juhudi za Mtu Mmoja Mmoja

Kisha faida yake nyingine ni hii kwamba juhudi za mtu mmoja mmoja zikistawi, kila mtu atajaribu kuchuma fedha kwa kufanya kazi kwa bidii sana. Daktari ataiendesha hospitali yake, mhandisi atadhihirisha ubingwa wake katika fani yake wafanyabiashara wataendesha viwanda vyao, na kwa hivyo akili itaendelea kupiga hatua mbele. Na watakapojikusanyia fedha, basi mali yao itachukuliwa toka kwao kwa njia ya kuhamasisha na kuhimiza. Kana kwamba faida zote mbili zitapatikana kwa wakati mmoja. Akili pia itaboreka na mali pia itapatikana. Ndani ya mfumo wa Kibolsheviki kuna kasoro hii kwamba kimatokeo huua kabisa vipawa vya kiakili. Na hata fedha zipatikanazo, wakati wa kuzitoa ndani ya mioyo ya matajiri huwa hakuna upendo wowote kwa maskini. Kwani wao

hufahamu kwamba fedha hizi zinachukuliwa kwa kutulazimisha na kwa dhuluma. Lakini kama daktari aambiwe nenda ukachume kadiri uwezavyo, wakili naye aambiwe fanya kazi yako ya uwakili na uchukue malipo upendavyo, mhandisi naye aambiwe nenda ukachume maelfu ya rupia kwa kuiboresha kwa kiwango cha juu fani yako ya uhandisi, halafu baada ya wao kwisha zichuma fedha hizo, wahimizwe kwamba watumie pesa zao kwa ajili ya mahitaji ya ndugu zao pia walio maskini, basi matokeo yatakuwa kwamba watakuwa tayari kwa furaha kutoa maelfu ya rupia. Matamanio yao pia yatabakia wala hawatakuwa na hisia ya kudhulumiwa, bali watoapo watakuwa na furaha kwamba mali zao zinatumika kwa ndugu zao maskini. Hivyo, kama mali zao za ziada zichukuliwe kwa kuhamasisha na kuhimiza, haki na uadilifu pia vitastawi na hii itakuwa pia njia ya yakini ya kuongeza kupendana baina ya watu.

## Madhara ya Kuchukua Mali za Wengine kwa Nguvu

Kinyume na haya, yule mtu ambaye serikali iichukue mali yake kwa nguvu, mwaweza kufahamu kwamba moyoni mwa mtu huyo mtazalikaje upendo kwa maskini! Wafanyakazi wa serikali watachukua tu kwa nguvu mali toka kwake, lakini ndani ya moyo wake utapenya uadui dhidi ya watu maskini, naye kila saa atasema, "Mungu Aiangamize serikali hii inayotudhulumu na Mungu Awaangamize pia maskini

hao ambao kwa sababu yao sisi tunadhulumiwa. Upande mwingine hakutakuwa na upendo wowote ndani ya mioyo ya maskini, watasema kwamba kwa hakika matajiri walikuwa wadhalimu wakubwa, ni vizuri sana kuwa serikali imewanyang'anya mali yao. Lakini, kama kwa kuhamasisha na kutimiza mtu atoe kiasi kidogo cha fedha, basi ndani ya moyo wake utazalika upendo kwa ajili ya maskini, na maskini pia watasema kwamba mtu fulani ni mwema sana, Mungu Atie baraka ndani ya mali yake kwani yeye anatutunza sisi tulio maskini. Hivyo, kitu kitakuwa ni kile kile, lakini huku kutazalika upendo wa maskini ndani ya mioyo ya matajiri na kule ndani ya mioyo ya maskini kutazalika upendo wa matajiri, na akili pia itastawi. Hivyo, Islam imechaghua njia hii hii.

## Islam Inawataka Matajiri Kutoa Kodi za Hiari Mbali na Kodi za Lazima

Kwa lengo hili, Islam imeweka kodi za lazima za Zaka na *Ushr* — sehemu ya kumi — na pamoja na hayo imesema pia kwamba:

وَأَنْفِقُوا فِي سَبِيلِ اللَّهِ وَلَا تُلْقُوا بِأَيْدِيكُمْ إِلَى التَّهْلُكَةِ ۛ وَأَحْسِنُوا ۛ إِنَّ اللَّهَ يُحِبُّ الْمُحْسِنِينَ ﴿١٩٥﴾ [33]

Na toeni katika njia ya Allah, wala msijitupe kwa mikono yenu katika maangamizo, na fanyeni wema, hakika Allah Huwapenda wafanyao wema.

Yaani toeni pia kodi iliyokadiriwa lakini mbali na hiyo tunakuombeni pia baadhi ya kodi za hiari na ni faradhi kwenu kushiriki katika zote hizo mbili.

Hivyo, Tunakuamuruni kwamba اَنۡفِقُوۡا فِیۡ سَبِیۡلِ اللّٰہِ, dumuni kutoa fedha kwa kuwasaidia maskini وَ لَا تُلۡقُوۡا بِاَیۡدِیۡکُمۡ اِلَی التَّہۡلُکَۃِ na msijiangamize nafsi zenu. Yaani, enyi matajiri, kama mtazitoa kwa furaha mali zenu za ziada, nazo ndizo za ziada tu, hamtopata hasara yoyote ya kweli. Lakini kama hamtofanya hivyo basi mtaangamia. Kwa kusema maneno haya, Allah Ameeleza hali kamilifu ya mambo ya Urusi, na Amesema kwamba msipofanya hivyo, hali ile iliyomkumba Tzar wa Urusi, au matajiri wa Urusi au matajiri wa Ufaransa, hiyo hiyo itakuwa hali yenu. Hatimaye siku moja watu watachoka na kuanza kupora mali na sawa na msemo wa Kishahpuri, 'watasoma dua ya kheri'. Hadhrat Khalifatul Masih I[ra] alikuwa akitoa maelezo ya msemo huu hivi kwamba huko kwetu muda kidogo uliopita wakulima walikuwa wakichukua mikopo kutoka kwa mkulima wa Kibaniani na Baniani aliendelea tu kukopesha. Kwa muda fulani hawakufikiria matokeo yake, lakini eneo lote lilipokuwa linadaiwa na Baniani huyo na mapato yote ya wakulima yakawa yanakwenda kwake, basi baada ya kuona hali hii, mkulima mmojawapo maarufu wa eneno hilo akawakusanya waheshimiwa wote na kusema hebu

semeni deni lote la Baniani huyo ni kiasi gani? Wakasema, ni kiasi kadha wa kadha. Hapo akauliza: Je kuna njia yoyote ile ya kulipa deni hili au la? Wakawa wanajibu kwamba hatuioni njia yoyote ile. Hapo akasema, vizuri basi someni dua ya kheri. Basi, wote wakawa wanasoma dua ya kheri. Baada ya hapo wote wakachukua silaha na kuelekea nyumbani kwa Baniani na kumuua na kuzichoma moto leja zake zote.

## Maangamio ya Watu Kutokana na Kutotoa Katika Njia ya Allah Mali ya Ziada Mbali na Ile ya Lazima

Allah ndani ya aya hii Anaashiria kwenye hali hii hii kwamba tazameni Sisi Tunakuamuruni kwamba kama mnayo mali ya ziada basi itumieni katika njia ya Allah na msijiingize nafsi zenu ndani ya maangamio. Yaani, bila shaka chumeni tu kwa furaha, lakini utajiri huu msiulimbikize majumbani mwenu, waila siku moja watu watainuka dhidi yenu nanyi mtaangamia. Kisha anasema: وَاَحۡسِنُوۡا , bali fanyeni wema zaidi ya hayo kwa njia hii kwamba mkipunguza mahitaji yenu wenyewe na kuokoa mali na kuzitoa katika nja ya Allah. Lakini kumbukeni kwamba msifanye amali hii kwa kuwaogopa watu, bali fanyeni kwa furaha. Kama mkifanya kutokana na hofu, basi maskini watakuwa wamesaidiwa lakini Mungu hatafurahi. Lakini kama mtajitolea kwa furaha, basi maskini nao watafurahi, nanyi pia mtasalimika na

maangamio, na Allah pia Atawaridhieni. Kisha Anasema إِنَّ ٱللَّهَ يُحِبُّ ٱلْمُحْسِنِينَ , kama mioyoni mwenu lizalike wazo hili kwamba sasa sisi tumepata jaza gani ya tuliyoyachuma, basi jibu laki ni hili kwamba mtapata jaza zaidi kuliko mali, nayo ni mapenzi ya Mungu Wako Aliyekuumba. Dunia yenu itarekebeshika pamwe na Akhera yenu, nanyi mtaishi kwa raha na utulivu hapa na huko Akhera. Tazameni, kwa fundisho hili, juu ya kuhifadhi vitu vya muhimu kama vile juhudi za mtu mmoja mmoja na juhuzi za kiukoo, makusudio yale pia hutimia ambayo Ubolsheviki unataka kuyatimiza.

## Fundisho la Islam la Kutimiza Mahitaji ya Maskini katika Kila Zama

Sasa swali lazalika kwamba hili ni fundisho tu la kutamkwa, ninyi mlisema kwamba Islam inaandaa hata mpango wa kuwalisha maskini, inaandaa pia mpango wa kuwapatia nguo, inaandaa pia mpango wa kuwapatia maskani na pia inaandaa mpango wa kuwapatia tiba na elimu, lakini hamkusema kwamba Islam ilifanikiwa katika hayo au la? Kama imeshafanikiwa, basi tuonyesheni mfano wake wowote ule. Jibu lake ni hili kwamba mafundisho yenye kufanikiwa na yaliyo bora ni yale ambayo yawe yanalingana na mazingira ya kila zama, yaani yawe yenye kukubali mazingira yote na kutimiza makusudio yake kulingana na mahitaji ya zama husika. Lile fundisho lisilokubali mazingira yote litafaa katika

sehemu moja na halitafaa katika sehemu nyingine. Kwa mfano, kama kukiwa na benchi basi halitaweza kutumika kila mahali. Kama sehemu ni ndogo basi ni lazima kwamba benchi halitaweza kutumika kwa sababu ya nafasi ndogo. Lakini kama mtu ana shuka, basi hilo linaweza kukunjwa katika sehemu ndogo na kukunjuliwa katika sehemu iliyo kubwa. Hivyo fundisho lenye mafanikio ni lile ambalo linaweza kunepa kuafikiana na mahitaji ya kila zama. Usiwe unepaji ule unaofahamiwa na wasomi wa siku hizi ambao katika unepaji huo wemeweka kando Kurani nzima.

## Njia ya Kutimiza Mahitaji ya Maskini Iliyotumika Mnamo Siku za Mwanzoni mwa Islam

Katika zama za mwanzo za Islam fundisho hili lilifanikiwa kikamilifu sawa na mahitaji ya zama hizo. Hivyo, katika zama za Mtume Mkarimu[sas] sio tu watu walifanywa kuishi maisha ya kawaida, bali Waislamu walipotwishwa majukumu ya utawala, basi inafahamika kutokana na historia kwamba, mbali na zaka, Mtume[sas] alikuwa akitimiza mahitaji yote ya maskini kutokana na michango, na kuhusiana na haya, wakati mwingine, masahaba walikuwa wakijitolea sana mno. Safari moja, Hadhrat Abu Bakr Siddik[ra] alitoa mali yake yote. Hadhrat Uthman[ra] naye wakati fulani alitoa takriban mali yake yote, na hiyo haikuwa zaka. Hivyo, fundisho

hili lilifanya kazi sawa na mahitaji. Na njia hii, kulingana na mahitaji ya zama zile, ilikuwa inatosha sana.

## Juhudi ya Kutimiza Mahitaji ya Maskini Chini ya Utaratibu Maalum katika Zama za Makhalifa wa Islam

Utawala ulipoenea zaidi na zikaja zama za Makhalifa, hapo chini ya utaratibu maalumu juhudi ilikuwa ikifanywa kwa kuwatimizia maskini mahitaji yao. Katika zama za Hadhrat Umar[ra] rejesta zilitayarishwa zenye majina ya watu wote, na kila mmoja kapewa chakula na nguo, na ilikuwa ikiamuliwa kwamba kila mwanaume apewe nafaka kiasi fulani, samli kiasi fulani, nguo kiasi fulani na apewe vitu kadha wa kadha. Kadhalika kila mtu, awe tajiri au maskini, alikuwa akipata mahitaji yake ya maisha, na njia hii kulingana na zama zile, ilikuwa inatosha kabisa.

Leo dunia inadhani kwamba ni Ubolsheviki ndio ulioanzisha kanuni hii kwamba kila mtu apewe mahitaji ya maisha yake, ilhali njia hii ilitolewa na Islam, ilikwisha tekelezwa kwa mpangilio bora kabisa katika zama za Hadhrat Umar[ra]. Bali imeelezwa ndani ya historia kwamba ule uamuzi alioutoa Hadhrat Umar[ra] mwanzoni haukuzingatia wale watoto wanaonyonya. Mtoto alikuwa akianza kupata msaada kutoka kwenye Hazina ya serikali ya Kiislamu wakati ambapo mama akamwachisha ziwa. Kwa kuona hali hii, mama fulani

alimuachisha mtoto wake ziwa ili kupata posho toka hazina kwa ajili ya mtoto yule. Usiku mmoja Hadhrat Umar[ra] alikuwa akizunguka mitaani akasikia sauti ya mtoto mmoja akilia ndani ya kibanda fulani. Hadhrat Umar[ra] akaingia ndani na kuuliza kwa nini mtoto huyu analia? Mama huyo akasema, 'Umar[ra] ameunda kanuni hii kwamba mtoto hatapewa posho yoyote maadam anaendelea kunyonya, basi, nimemuachisha ziwa ili apate posho, na analia kutokana na sababu hii. Hadhrat Umar[ra] anasema kwamba nikasema moyoni mwangu, "Ewe Umar, huelewi kwamba umewaachisha ziwa watoto wangapi wa Kiarabu na kudhoofisha kizazi kijacho. Hivyo, akatoa amri kwamba kila mtoto apate posho pindi tu azaliwapo. Hivyo, wakati huo kulikuwepo mpango huu, na kama nilivyosema, mpango huu ulikuwa unatosha kwa ajili ya wakati huo na kwa ajili ya mahitaji ya zama hizo. Naam, hii ni sahihi kwamba katika zama hizo umaskini na utajiri haukuwa na tofauti kubwa kama ilivyo siku hizi. Wakati huo kodi iliyokadiriwa na serikali na msaada uliokuwa ukitolewa na matajiri kwa wakati muafaka ulikuwa ukiyatimiza mahitaji haya. Mashindano ya kibiashara hayakuwa kadri yalivyo sasa. Nchi zilikuwa hazina kawaida ya kupora utajiri wa nchi za jirani kama zinavyopora sasa. Kwa hiyo tunakubali kwamba mpango ule hauwezi kufaa leo. Lakini kimsingi fundisho hilo hata leo laweza kufaa. Katika zama hizo, bila hata ya kuvumbua njia mpya,

iliwezekana kupitisha maisha kwa kipato kile kile kilichopatikana kwa njia ya kodi zilizokadiriwa au kwa michango ya hiari. Basi, kwa wakati huo ilifahamika kuwa kinatosha, lakini siku hizi mpango huo hauwezi kutosheleza. Zama hizi ni zama za mipangilio. Hivi sasa baada ya kuona ukosefu wa utulivu duniani, serikali zimeamua kwamba sehemu kubwa ya utajiri iwe mikononi mwao. Na kama mifumo hiyo iliyotajwa juu ifanikiwe, yaani wowote mmojawapo katika hiyo ufanikiwe, basi ni lazima fedha zitapungua mikononi mwa watu na zitakwenda zaidi mikononi mwa serikali. Hata kama Ubolsheviki ufanikiwe au Ujamaa ufanikiwe, matokeo yatakuwa tu haya haya kwamba fedha chache zitabaki mikononi mwa watu na sehemu kubwa ya utajiri itahodhiwa na serikali. Lakini mbali na kasoro zilizotajwa hapo juu, kutakuwepo pia na hasara hii kwamba ingawaje baadhi ya nchi zitakuwa na amani zaidi na zingine zitapatwa na mateso zaidi.

## Haja ya kuwa na Nidhamu Mpya kwa ajili ya Kuwapatia Maskini Utulivu Kulingana na Mahitaji ya Zama hizi

Badala ya nidhamu hii, kwa kulipa fundisho la Islam sura makhsus, mpango uliopangwa kwa watu wa zama za Mtume[sas], hauwezi asilan kufanikiwa leo, kwani sasa hali zipo tofauti. Halikadhalika baadaye maagizo hayo yalipewa sura nyingine na Hadhrat Abu Bakr[ra], Hadhrat

Umar[ra], Hadhrat Uthman[ra] na Hadhrat Ali[ra] haiwezi kufanikiwa siku hizi. Hivyo yahitajika kwamba katika zama hizi za sasa, utekelezaji wa mafundisho ya Islam uwe katika sura ambayo kusizalike kasoro zile zilizomo ndani ya mifumo hiyo ya kidunia. Na fedha kiasi hiki ziingie mikononi mwa nidhamu ya Kiislamu ambazo ni za lazima kwa kustawisha usawa na kutimiza haja za watu wote sawa na mahitaji ya zama hizi. Makhalifa walieleza maagizo ya Kiislamu kulingana na mahitaji ya zama zao. Kama nilivyosema, katika zama za Hadhrat Umar[ra] kulikuwa na mpango maalum wa kufanya. Jina la kila mtu lilikuwa likiorodheshwa ndani ya rejesta na Baitul Mal ya Kiislamu ilikuwa ndio yenye jukumu la kutimiza mahitaji thabiti ya kila mtu. Mwanzoni, fedha zote zilizokuwa zikija zilikuwa zikigawanywa miongoni mwa maaskari, lakini Hadhrat Umar[ra] alisema kwamba iwepo hazina ya Kiislamu na watu wengine nao wana haki zao, kwa hiyo fedha hazitagawiwa zote baina ya maaskari, bali sehemu yake kubwa itahifadhiwa. Hivyo kutokana na fedha hizi maskini wa nchini walikuwa wanapatiwa posho ya kujikimu.

Ilmuradi, makhalifa, kulingana na mahitaji ya zama zao, walitoa ufafanuzi wa maagizo ya Islam. Lakini kwa ajili ya kutimiza mahitaji ya zama za sasa, kulihitajika nidhamu nyingine. Na kwa kuistawisha nidhamu hii ilikuwa ni lazima kwamba aje mtu mmoja toka kwa

Mwenyezi Mungu na kwa kuzifuta shida na maumivu yote atoe nidhamu ambayo sio ya kiardhi bali ya kimbingu. Na atoe muundo wa aina ambayo itimize mahitaji yote yanayowahusu maskini na kuyaondolea mbali mashaka ya dunia. Sasa kila mtu ambaye anakubali kwamba Mtume[sas] alitoa bishara ya kuja kwa muahidiwa fulani, kila mtu anayekubali kwamba Mtume[sas] alitoa bishara ya kuja kwa Masihi mmoja na Mahdi, atalazimika pia kukiri kwamba kazi ya kuondoa fitina, ufisadi na taabu zinazoonekana katika zama hizi inapaswa kukabidhiwa kwa huyu huyu aliyetumwa ili zisizalike pia zile kasoro zinazozalika kutokana na Ubolsheviki, zisizalike kasoro zile zinazozalika kutokana na Ujamaa na zisizalike kasoro zinazozalika kutokana na Ujamaa wa Kitaifa.

Watu wote wapate chakula, wapate mavazi, wapate maskani, wapate matibabu, wapate pia elimu, kisha akili zisiwe finyu, jazba bora za juhudi za mtu binafsi na za kafamilia kumiliki mali zisiangamie, kusiwe pia na dhuluma, pia watu wasiporwe, amani na upendo pia viwepo, lakini na fedha pia zipatikane.

## Mfumo wa Khatamul Khulafaa kwa Kuiondoa Shida Duniani Kulingana na Mahitaji ya Zama hizi

Hivyo, kwa ajili ya kutimiza mahitaji ya zama hizi, lilikuwa ni jukumu la Khatamul-Khulafaa kuunda

mfumo kulingana na mafundisho ya Kiislamu na kuutokomeza msiba huu duniani. Hivyo, kama nitakavyoeleza mbele, yeye, chini ya agizo la Mwenyezi Mungu, ameishatoa njia ya kutimiza haja hii ya muhimu.

## Mfumo wa Kiislamu na Kanuni zake Muhimu za Kuwaondolea Shida Maskini

Nimeshaeleza hapo juu kwamba kanuni za muhimu za mfumo wa Kiislamu ni hizi:

**Kwanza** mahitaji ya wanadamu wote yatimizwe.

**Pili,** lakini katika utekelezaji wa shughuli hii, zisipate kuangamizwa jazba nyepesi za juhudi za mtu mmoja mmoja na za maisha ya kifamilia.

**Tatu,** kazi hii itekelezeshwe na matajiri kwa hiari na upendo, na nguvu isitumiwe.

**Nne,** mfumo huu usiwe wa kitaifa bali uwe wa kimataifa. Siku hizi mifumo yote iliyopo ni ya kitaifa, lakini Islam imetoa mfumo ule usiokuwa wa kitaifa bali wa kimataifa.

Sifa zote nzuri za mafundisho ya Kiislamu zimejumuika ndani ya kanunni hizi nne. Kama kanuni zote hizi nne zipatikane ndani ya mfumo wowote ule, basi tunaweza kusema kwamba mfumo huo ndio ulio bora kabisa na uliokamilika zaidi kuliko mifumo yote.

## Msingi wa Nidhamu Mpya yenye Kuiondolea Dunia Shida Uliowekwa na Hadhrat Masihi Mau'udi[as] mnamo Mwaka 1905

Sasa ninaeleza kwamba ni namna gani mjumbe wa zama hizi, aliye naibu wa Mtume[sas], alivyoyatimiza makusudio haya manne kwa amri ya Allah, na namna alivyoweka msingi wa nidhamu mpya ya dunia kwa kuafikiana kabisa na mafundisho ya Kiislamu. Mifumo yote hii ya Ubolsheviki, Ujamaa na Ujamaa wa kitaifa iliundwa baada ya Vita Kuu. Hitler aliibuka baada ya vita, Musolini[34] aliibuka baada ya vita, na Stalin aliibuka baada ya vita. Ilmuradi, mifumo yote hiyo inayodai kuleta nidhamu mpya duniani, takriban yote hiyo imeibuka baina ya mwaka 1919 na 1921. Lakini Mjumbe wa Mwenyezi Mungu aliweka msingi wa nidhamu mpya mnamo mwaka 1905, na aliuweka kwa njia ya mfumo wa Wasia.

## Kurani Tukufu Inaashiria Kujitolea kwa Hiari Wakati wa Mahitaji Mbali Mbali

Kurani Tukufu, kimsingi ilieleza:

وَ اَنۡفِقُوۡا فِیۡ سَبِیۡلِ اللّٰہِ وَ لَا تُلۡقُوۡا بِاَیۡدِیۡکُمۡ اِلَی التَّہۡلُکَۃِ ۚۖۛ وَ اَحۡسِنُوۡا ۚۛ اِنَّ اللّٰہَ یُحِبُّ الۡمُحۡسِنِیۡنَ ﴿۱۹۶﴾

Na toeni katika njia ya Allah, wala msijitupe kwa mikono yenu katika maangamizo, na fanyeni wema, hakika Allah Huwapenda wafanyao wema. (2:196).

Lakini ndani ya fundisho hili, Allah Hakuainisha kanuni za kujitolea kwa hiari, Alisema tu, 'Enyi Waislamu!

Mbali na kodi za lazima, mtapaswa pia kutoa kodi zingine', lakini hakusema kwamba kodi hizo zitakuwa ni ngapi na zitakuwa na sura gani maalum. Kama katika zama fulani, serikali ya Kiislamu ilihitaji rupia moja kati ya mia, basi Khalifa wa zama akasema: Enyi ndugu! Toeni Rupia moja kati ya mia kwa ridhaa yenu wenyewe. Na kama katika zama nyingine serikali ya Kiislamu ilikuwa na haja ya rupia mbili kati ya mia, basi Khalifa wa zama alikuwa akisema: Enyi ndugu! Toeni kwa hiari yenu rupia mbili kati ya mia moja. Ni kutokana na sababu hii hii kwamba katika kila zama imekuwa ikitolewa ufafanuzi tofauti. Mtume[sas] aliitolea ufafanuzi kwa njia hii kwamba mara kwa mara alikuwa akichukua michango ya ziada, na Makhalifa walitoa ufafanuzi huu kulingana na zama zao kwamba zile mali zilizokuwa zikija kwa ajili ya kuwagawia wanajeshi, walihifadhi kiasi kikubwa cha fedha hizo na kuwaambia wanajeshi kwamba ninyi muiache haki yenu kwa furaha. Na Hadhrat Masihi Mau'udi[as] alitoa ufafanuzi kulingana na zama zake. Kama serikali ya Kiislamu iwajibike kuipatia chakula dunia nzima, kuvisha mavazi dunia nzima, kuandaa makazi kwa dunia nzima, kuandaa matibabu kwa dunia nzima, kuandaa mipango ya elimu kwa kuondoa ujahili duniani kote, basi kwa yakini serikali itapaswa kuwa na fedha nyingi mno kuliko zilizokuwa katika zama za awali. Hivyo, Hadhrat Masihi Mau'udi[as] alitangaza kwa amri ya Allah kwamba katika

zama hizi Allah Ameandaa mfumo huu kwa wale wanaotaka kuipata Pepo ya kweli, kwamba wao, kwa ridhaa yao wenyewe, wafanye wasia wa kutoa kwa uchache sehemu ya kumi au kwa wingi theluthi ya mali zao. Na anasema kwamba kile kipato kitakachotokana na wasia huu kitatumika "kwa ajili ya maendeleo ya Islam, uenezaji wa elimu ya Kurani na vitabu vya kidini na kwa ajili ya watoaji wa mawaidha wa Jumuiya." (Sharti la 2). Kadhalika kila jambo lililomo ndani ya uenezaji wa Islam, ambalo haujafika wakati wa kulifafanua hivi sasa, mambo yote hayo yatatekelezwa na fedha hizi. (Sharti la 2). Yaani, kwa kuimarisha na kustawisha mafundisho ya Kiislamu duniani, mambo yote yanayohitajika na ambayo kuyafafanua haujafika wakati wake. Naam, mambo haya yatafafanuliwa na mtu mwingine katika zama zake. Fedha hizi zitatumika kwa ajili ya kuyafanikisha mambo yote hayo.

## Habari za Nidhamu Mpya ya Wasia

Hili ndilo lile fundisho alilolitoa Hadhrat Masihi Mau'udi[as]. Anasema kwa uwazi kabisa kwamba kila jambo linaloingia ndani ya uenezaji wa Islam na ambalo si wakati wake kulitolea ufafanuzi kwa sasa, fedha hizi zitatumika juu yake. Hiyo ilimaanisha kabisa kwamba kuna mambo mengine pia ambayo hayawezi kubainishwa hivi sasa, na kwamba wakati unakaribia ambapo dunia itapaza sauti ikisema: Tunahitaji nidhamu

mpya. Ndipo sauti itapazwa tokea kila upande kwamba njooni, tukupeni nidhamu mpya. Urusi itasema, njooni nikupeni nidhamu mpya. India itasema, njooni nikupeni nidhamu mpya. Ujerumani na pia Italia itasema, njooni nikupeni nidhamu mpya. Amerika itasema, njooni nikupeni nidhamu mpya. Wakati huo Khalifa wangu atasema kutokea Qadian kwamba nidhamu mpya imo ndani ya 'Wasia'. Kama dunia inataka kufuata njia ya mafanikio na ustawi, basi njia yake ni moja tu, nayo ni hii kwamba nidhamu ya 'Wasia' itekelezwe duniani.

## Katika Mali ya Wasia mna Haki ya Mayatima, Maskini na Waislamu Wapya Wasio na Njia za Kutosha za Kujikimu

Kisha anasema:

> "Ndani ya mali hizo mtakuwa pia na haki ya wale mayatima na maskini ambao hawana njia za kutosha za kujikimu."
>
> (Sharti namba 2).

Kisha anasema:

> "Itajuzu kwamba Anjuman ikuze mai hii, kwa maafikiano, kwa njia ya biashara."
>
> (Dhamima Sharti Namba 9).

Yaani, itajuzu kufanya biashara kwa kutumia fedha hizi, nanyi mtakuwa na ruhusa ya kwamba mchukue kwa

watu sehemu ya kumi, ya nane, ya tano au ya tatu, halafu mfanye biashara na kuziongeza fedha hizi.

## Hatari kwa Imani ya Walio Nje ya Nidhamu hii Mpya

Kisha anasema, jaribio la imani ya kila mwaminio limo katika hii kwamba aingie ndani ya nidhamu hii na kuzipata fadhili makhsus za Mwenyezi Mungu. Ni mnafiki tu ndiye atakayebaki nje ya nidhamu hii. Ingawa halazimishwi yeyote, lakini pamoja na hayo amesema pia kwamba humo mna jaribio kwa imani yenu. Kama mnataka kuipata pepo, basi ni lazima kwenu kutoa dhabihu hii. Naam, kama mioyoni mwenu hamuithamini pepo, basi jiwekeeni mali zenu, hatuna haja ya mali zenu.

## Tofauti Iliyopo Kati ya Mali Zichukuliwazo kwa Njia ya Ubolsheviki na kwa Njia ya Wasia

Tazameni kwamba Ubolsheviki unanyang'anya mali za watu kwa nguvu, lakini Masihi Mau'udi[as] anasema kwamba kama mtu akiritadi, basi mrudishieni mali yake, kwani Mungu si mhitaji wa mali ya mtu yeyote, na kwa Mwenyezi Mungu mali ya aina hiyo ni yenye kuchukiza na kustahili kukataliwa. (Dhamima Sharti Na. 12) Kubwa ilioje tofauti hii kwamba nidhamu mpya inayotoa dunia, ndani yake inawanyang'anya watu mali zao kwa nguvu, lakini ile nidhamu mpya aliyoitoa Hadhrat Masihi Mau'udi[as], humo anasisitiza kujitolea

kwa hiari, na anasema kwamba kama yeyote yule akiritadi, basi mrudishieni mali yake, kwani mali kama hiyo ni yenye kukataliwa na haipaswi kuwa nayo.

## Kupata Makusudio kwa Amani Kabisa kwa Njia ya 'Wasia' Kinyume na Ubolsheviki

Tazameni, kwa kuzizingatia kanuni hizo kwamba makusudio ambayo Ubolsheviki umejaribu kuyapata nusu-nusu kwa kutumia mabavu, Hadhrat Masihi Mau'udi[as] aliyatimiza makusudio haya kikamilifu kwa huba na upendo. Ubolsheviki unasema nini? Unasema hii tu kwamba wanyang'anyeni matajiri milki zao ili zitumiwe kwa maskini. Hadhrat Masihi Mau'udi[as] alizichukua hizo kwa huba na upendo sawa na mafundisho ya Kiislamu na kulingana na mahitaji ya zama zake na akasema kwamba nyote mtoe angalau sehemu ya kumi ya milki zenu ambazo zitatumika kwa mayatima na maskini na kazi ya kuueneza Uislamu. Sawa na kanuni ya wasia huu, kila Muahmadiyya mwenye kuusia hutoa kwa manufaa ya Uislamu na ya binadamu kwa hiari yake kwa kuzingatia faida yake ya maisah yake ya Akhera.

## Mapinduzi Adhimu Yatokanayo na Dunia Nzima Kuingia katika Uahmadiyya

Kama dunia nzima iingie katika Uahmadiyya, Hadhrat Masihi Mau'udi[as] ataiambia dunia nzima kwamba Mwenyezi Mungu Anataka kuipima imani yenu. Kama ninyi ni waaminio wa kweli, kama ninyi mwaitaka pepo,

kama mnataka kupata radhi na furaha ya Mwenyezi Mungu, basi toeni sehemu ya kumi au hadi sehemu ya tatu ya milki zenu kwa kuueneza Uislamu na kwa mambo yafaayo kwa Islamu. Kwa njia hii, milki zote za dunia zitaingia ndani ya mfuko wa taifa, na bila ya kushurutisha au kupigana vita, Makao Makuu ya Kiislamu yatakuwa, katika zama za kizazi kimoja tu, mmiliki wa sehemu ya kumi hadi ya tatu ya milki zote duniani na kutokana na mfuko huo wa taifa maskini wote wataweza kutunzwa.

## Katika Vizazi Vichache tu Milki zote za Waahmadiyya Zitakuwa Zinamilikiwa na Nidhamu ya Ahmadiyya

Kumbukeni kwamba Wasia sio kwa ajili tu ya kizazi cha kwanza, bali ni kwa kizazi cha pili pia, nao pia wataombwa kujitolea hivyo hivyo. Na kwa sababu kwa njia ya Wasia dunia inatolewa Pepo, kizazi kijacho kitawezaje kukataa kuichukua. Hivyo, kizazi cha pili kitatoa milki iliyobakia, kwa moyo mkunjufu, sehemu ya kumi ya mali hiyo hadi ya tatu kwa ajili ya mahitaji ya kitaifa. Kisha kizazi cha tatu na halafu cha nne pia kitafanya hivyo hivyo na kwa njia hii, ndani ya vizazi vichache tu, milki za Waahmadiyya zitamilikiwa na ndidhamu ya Ahmadiyya. Fikirieni, kama dunia nzima iingie katika Ahmadiyya, je mnafahmau nini itakuwa natija yake? Itakuwa ni hii tu kamba ndani ya vizazi

vichache, dunia nzima itakuwa imezitoa kwa furaha milki zake kwa ajili ya shughuli za kitaifa, na hali yao ya kumiliki mali binafsi haitaangamia, ndihambu ya nyumbani nayo haitaangamia. Kisha watu watazalisha mali zingine kwa ajili yao na vizazi vyao, na tena watatoa kwa furaha sehemu yake ya kumi hadi ya tatu kwa ajili ya mahitaji ya Taifa. Kisha mali hii mpya nayo katika zama za vizazi vichache itaingia ndani ya mfuko wa Taifa. Na hivyo, hii silsila itaendelea. Kwa namna ya mfano, fahamuni hivi kwamba kama mtu fulani ana rupia mia moja, naye atoe wasia wa kutoa sehemu yake ya 5, basi rupia 20 zitakuja ndani ya mfuko wa Taifa na rupia 80 zitabakia kwake ambazo atazipata mtoto wake. Kisha kama mtoto wake atafanya wasia wa kutoa sehemu ya tano ya mali hiyo, basi rupia zingine 16 zitakuja ndani ya mfuko wa Taifa. Hivyo, asilimia 36 itaingia ndani ya mfuko wa Taifa na asilimia 64 zitabakia kwake. Kisha kwa mfano mtoto wake naye atakapotoa wasia wa sehemu ya tano, basi karibu rupia 12 tena zitaingia ndani ya mfuko wa Taifa, na hivyo asilimia 48 itamilikiwa na serikali na asilimia 52 itabakia kwa familia hiyo. Baadaye mtoto wake atatoa wasia wa kutoa sehemu ya tano ya rupia 52 basi rupia kumi tena zitatoka mkononi mwao. Kwa njia hii asilimia 58 zitakuja ndani ya mfuko wa Taifa na familia hii itabakia tu na asilimia 42. Ilmuradi, makusudio yale yale ambayo chini ya Ubolsheviki hupatikana kwa njia ya upanga na

kumwaga damu, kama nidhamu ya wasia ienee mno, basi makusudio pia yatatimia na fujo na umwagaji damu pia hautaonekana, na pia kutakuwepo na huba na upendo, hataonekana yeyote duniani mwenye njaa na aliye rabana. Na ndani ya vizazi vichache, bila ya kuiangamiza hali ya umilikaji mali binafsi, milki zote za dunia zitahamia ndani ya mfuko wa Taifa.

## Nidhamu ya Wasia Haitakuwa ya Kitaifa bali ya Kimataifa

Kisha nidhamu hii haitakuwa ya kitaifa bali kwa sababu ya kuwa ya kidini itakuwa ni ya kimataifa. Wajamaa wa Uingereza huipenda nidhamu ile ambayo athari yake inakomea humo humo Uingereza. Wabolsheviki wa Kirusi huipenda nidhamu ile ambayo athari yake huishia humo humo ndani ya Urusi. Lakini Uahmadiyya ni madhehebu yanayoiita Urusi kwenye nidhamu hii, yanaiita pia Ujerumani, yanaiita pia Uingereza, yanaiita pia Amerika, yanaiita pia Uholanzi, yanaiita pia China na Japani. Hivyo, mali ile itakayokusanywa kwa njia ya Uahmadiyya, hiyo haitatumiwa kwa nchi moja, bali itatumika kwa maskini wa dunia nzima. Itawafaa maskini wa Bara Hindi, itawafaa maskini wa Uchina, itawafaa pia maskini wa Japani, itawafaa pia maskini wa Afrika, itawafaa pia maskini wa Bara Arabu, itawafaa pia maskini wa Uingereza, Amerika, Italia, Ujerumani na Urusi.

## Nidhamu ya Kukuza Kimataifa Undugu Iliyotolewa na Masihi Mau'udi[as]

Ilmuadi, nidhamu zile zilizo za kidunia huwa zinaongeza jadhba ya utaifa, lakini Hadhrat Masihi Mau'udi[as] alitoa nidhamu ile yenye kukuza udugu wa kimataifa. Halafu, huko Urusi mwenyeji wa Urusi hutoa miliki yake kwa kushurutishwa kwa ajili ya Urusi, lakini chini ya mfumo wa Wasia, mwenyeji wa India hutoa kwa ridhaa yake binafsi, kwa ajili ya dunia nzima. Mwenyeji wa Misri, kwa ridhaa yake, hutoa mali yake kwa ajili ya dunia nzima. Mwenyeji wa Shamu kwa ridhaa yake, hutoa mali yake kwa ajili ya dunia nzima. Tofauti ya wazi ilioje hii kati ya Nidhamu Mpya ya Kiislamu na Nidhamu Mpya ya kidunia.

## Bashasha na Furaha Iliyomo Mioyoni mwa Wanaotoa Mali kwa ajili ya Maskini chini ya Nidhamu mpya ya Kiislamu

Halafu, mfumo wa Kirusi, kwa kuwa unatumia nguvu, matokeo yake huwa kwamba kwanza matajiri huihama Urusi na kufanya jitihada za kuipinga, na haizaliki furaha wala bashasha mioyoni mwao baada ya kuwapa maskini mali zao. Mrusi anyang'anywapo mali yake, yeye hacheki, bali huelekea nyumbani kwake akilia na huwaambia jamaa zake kuwa serikali hii laanifu imeninyang'anya mali zangu. Lakini katika nidhamu hii mpya, mkulima mwenye ekari kumi, halii baada ya kutoa ekari zake mbili

au tatu, bali keshoye tu humuendea ndugu yake na kumwambia: Ewe ndugu yangu! Nipongeze, kwani nimepata fursa ya kufanya wasia na kupata radhi ya Mwenyezi Mungu. Na maana yake nyingine ni hii kwamba ‘nimenyang'anywa’ ekari 2 au 3 kwa ajili ya maskini, lakini halii. Hahuzuniki bali anasema, nipongeze ndugu yangu kwani nimefanya wasia, na anasema Mungu Anioneshe pia siku ambapo nawe pia utafanya wasia ili nami niweze kukupongeza. Amwambiapo mkewe habari hii, mke hasemi kwamba Mungu Awaangamize watu wale waliotunyang'anya mali zetu, bali midomo yake hutetemeka, machozi humlengalenga machoni na humtazama mumewe kwa mtazamo wa kushawishi na kusema: Tazama, Allah Amekupa uwezo kwamba wewe umefanya wasia. Mimi sina milki, nitawezaje kufanya wasia? Basi, wewe nipatie chochote kati ya milki yako ili nami pia nipate neema hii. Yeye hutumia mbinu na mishale ya akina mama ambayo waume hawawezi kuvumilia sana. Hatimaye humfanya akubali na humkabidhi sehemu fulani toka kwenye mali yake. Na mkewe naye hutoa wasia kutoka kwenye mali hiyo hiyo akisema mimi nafanya wasia wa sehemu ya kumi au ya nane au ya sita, kana kwamba kutoka katika mali hii hii iliyosalia, imani tena inachukua, na sehemu nyingine inaingia ndani ya mfuko wa Taifa. Wakati huo huo mtoto naye anaingia nyumbani. Anaposikia kwamba baba yake na mama yake wamefanya wasia, basi hupatwa na

simanzi na kukaa chini na kumwambia baba yake: Baba! Mpendwa Mwenyezi Mungu Akupe umri mrefu na tuwe chini ya himaya yako. Mimi sina chochote, sasa nitawezaje kufanya na Mwenyezi Mungu biashara hii iliyo rahisi? Kama unipe chochote ili nami pia nifanye biashara na Mwenyezi Mungu kupata Pepo. Kama baba yake anampenda sana, basi baada ya kufikiria kwamba hatimaye milki yangu itaenda kwake, wakati huo huo anampa sehemu fulani ya miliki yake, naye pia akifanya wasia anafanya biashara ya pepo na Mola Wake. Kwa njia hii, mali iliyosalia tena inajumuika ndani ya mfuko wa Taifa. Na kama baba yake ni mgumu kiasi fulani na haamini kumpatia mtoto wake milki yake katika uhai wake, basi mtoto huyo mwenye bahati njema hufanya biashara na milki ile ambayo bado hajaipta na hufanya wasia kwamba ingawa kwa wakati huu sina milki yoyote, lakini mimi nafanya wasia kwamba kutoka katia kipato changu nilicho nacho sasa nitakuwa nikitoa sehemu ya kumi ya mchango wa wasia. Na kama nikapata milki yoyote katika siku zijazo, basi nitatoa pia sehemu yake ya kumi. Kwa maneno mengine, hii inamaanisha kwamba wakati baba atakapofariki na milki yake nitapata mimi, basi sehemu ile itakayobakia baada ya kutoa wasia wa baba, naitolea sasa hivi ahadi ya kutoa sehemu yake ya kumi. Kwa njia hii, mali iliyobakia sehemu yake ya kumi itaenda tena kwenye mfuko wa Taifa.

Kisha tazameni, chini ya nidhamu ya kidunia, wale wanaotozwa kodi huwa hawafurahi, na wale wasiotozwa hufurahia. Matajiri wanachukia kwamba kwa nini tunatozwa kodi, na maskini hufurahi kwamba sisi tumezipata mali za matajiri. Lakini chini ya kanuni ya wasia inakuwa nini? Usomeni 'Wasia' kwa makini. Chanzo cha wasia ndicho rasilimali. Lakini, kwa kuwa mali hazinyang'anywi kwa nguvu, bali badala yake inatolewa neema ya pepo, hivyo wale ambao kwa ajili yao mali ile ilitolewa, wao hawakusema kwamba matajiri ambao mali zao zilichukuliwa wameporwa kweli kweli, bali wao huhuzunika kwamba kwa nini sisi tumenyimwa biashara hii nzuri, nao wakamuomba Hadhrat Masihi Mau'udi[as] kwamba pia tufunguliwe njia, naye kwa idhini ya Mwenyezi Mungu akawapa ruhusa ya kufanya wasia wa mapato yao. Tuseme kwamba njia ile aliyoianzisha Hadhrat Masihi Aliyeahidiwa[as], mwanzoni mwake ilikuwa inatokana na rasilimali, lakini kutokana na msisitizo wa watu wale ambao hawakuwa na raslimali, kwa idhini ya Allah, akawapa pia ruhusa ya kufanya wasia wa mapato yao na kwa njia hii raslimali na mapato mengine yote yakaanza kujumuika ndani ya mfuko wa Taifa.

## Msingi wa Nidhamu mpya Uliwekwa Huko Qadian mnamo Mwaka 1905

Ilmuradi, msingi wa nidhamu mpya haukuwekwa huko Urusi mnamo mwaka 1910, wala hautawekwa katika

mwaka wowote ule katika siku zijazo huko Ulaya baada ya vita hii, bali msingi wa Nidhamu Mpya yenye kuipatia utulivu dunia, yenye kuboreshea maisha ya kila mtu na pamoja na hayo yenye kuihifadhi dini ulishawekwa huko Qadian tangu mwaka 1905. Sasa dunia haina haja ya nidhamu mpya yoyote nyingine. Sasa kupigia kelele nidhamu mpya ni sawa na msemo wa Kiurdu ambayo muradi wake ni kwamba wakati ufaao umeishapita, iliyobaki ni masikitiko.

Kazi iliyokuwa ifanyike imeshafanyika. Sasa wanazuoni wa Ulaya wanapiga tu makelele.

Nidhamu Mpya ya Islam na ya Ahmadiyya ni ile ambayo msingi wake sio kushurutisha, bali uko juu ya huba na upendo. Ndani yake mmezingatiwa pia uhuru wa mwanadamu. Pia yametiwa maanani humo maendeleo ya kiakili ya watu, na humo pia mmeimarishwa umilikaji wa kila mtu binafsi na wa kifamilia.

## Nafasi Mbalimbali za Matumizi ya Mali za Wasia

Nimeshaeleza kwamba ni makosa kufikiria kuhusiana na Wasia kwamba fedha zake zinaweza kutumiwa tu kwa ajili ya kuihubiri Islam. Maneno ya kitabu cha 'Wasia' yanaeleza kwa uwazi kabisa kwamba makusudio mengine pia yatatekelezwa kwa fedha hizi, kwani Hadhrat Masihi Mau'udi[as] amesema : Kila jambo lile lililomo ndani ya maslahi ya uenezaji wa Islam, ambalo kulitolea ufafanuzi kwa sasa haujafika wakati wake,

mambo hayo yote yatatekelezwa na fedha hizi. Yaani, katika zama zijazo yatadhihirika maslahi ya aina hii ya kueneza Islam, yaani baada ya kuifuata Islam kwa matendo, zitatokeza fursa za kudhihirisha uzuri wake ambazo juu yao kuzitumia fedha za wasia si tu inajuzu bali itakuwa ni lazima. Tena Hadhrat Masihi Mau'udi[as] alitumia pia maneno ya 'mayatima na maskini', na akasema kwamba wenye mahitaji wanayo haki juu ya fedha hizi. Hivyo, kwa hakika ndani ya maneno haya imeashiriwa kwenye nidhamu ile ile ambayo Islam inataka kuianzisha kwamba chakula kipatikane kwa kila mwanadamu mavazi yapatikane kwa kila mwanadamu, makazi yapatikane kwa kila mwanadamu, nyenzo za elimu na tiba zipatikane kwa kila mtu. Na kazi hii haiwezi kutekelezeka kwa kodi. Inaweza tu kutekelezeka kwa njia hii kwamba rasilimali zichukuliwe na kutumiwa kwenye mahitaji haya.

Mtu anaweza kusema kwamba wewe una uwezo gani wa kutoa madai kama haya na kuyatekelezesha matamanio haya ya nadharia tu. Lakini shaka hii pia sio sahihi, kwa sababu wakati tunapolieleza jambo hili, huwa tunalieleza kwa sababu hii kwamba sisi tuna yakini kamili ya kwamba Jumuiya yetu haina budi kuenea dunia nzima. Hivyo, tunapokuwa na yakini hii kutokana na funuo za Mwenyezi Mungu na ahadi Zake, kwamba baada ya miaka hamsini au sitini au mia kutoka sasa,

Jumuiya ya Ahmadiyya kwa vyovyote vile itakuwa imeishinda dunia, basi tunayo yakini kamili pia ya kwamba nidhamu hii aliyoieleza Hadhrat Masihi Mau'udi[as] itakuja kustawi siku moja. Ardhi na mbingu zaweza kutetereka lakini maneno ya Mwenyezi Mungu hayawezi asilan kutetereka.

## Ustawishaji wa Uhakika wa Nidhamu Iliyotolewa kwa Njia ya Wasia

Baadhi ya watu wasema hivi pia kwamba hajulikani nidhamu hii itaanza kufanya kazi lini. Kwani, Jumuiya inasonga mbele pole pole sana. Jibu lake ni hili kwamba mambo huwa hayaendi kwa papara. Jengo lisilo na msingi huporomoka haraka sana. Nidhamu zile zinazojengwa kwa papara zinaporomoka kwa haraka. Nidhamu itakayostawi ni ile itakayostawishwa kutokana na kupendwa kwa dhati na kila mtu, mdogo au mkubwa. Nyasi humea leo na kesho hukauka, lakini mtunda hukua katika muda mrefu na halafu hubakia kwa karne na karne.

Hivyo, kadiri Jumuiya yetu itakavyoendelea kukua katika siku zijazo, ndivyo itakavyoendelea kukua ile nidhamu ambayo Mwenyezi Mungu Ameisimamisha duniani kwa njia ya wasia. Hivyo Hadhrat Masihi Mau'udi[as] amesema ndani ya kitabu chake 'Wasia' kwa kuizingatia kanuni hii hii kwamba:

"Msidhani ya kwamba hayo ndiyo mambo yasiyowezekana, bali ndiyo matakwa ya yule Mweza Aliye Mfalme wa ardhi na mbingu. Sina wasiwasi ya kwamba mali hizo zitakusanyikaje na kwamba Jumuiya hiyo itapatikanaje ambayo kwa jazba ya uaminifu itajitolea muhanga kufanya kazi hii kubwa, bali nina kiherehere ya kwamba baada ya zama zetu wale watu watakaoachiwa usimamizi wa mali hizo wasije wakateleza kwa kuona wingi wa mali na wakaipenda dunia. Hivyo, naomba ya kwamba daima Jumuiya hii iendelee kuwa na wale waaminifu watakaotumikia kwa ajili ya Mungu. Naam, itajuzu wapewe posho kama msaada wale wasio na mapato yoyote."[35]

## Wingi wa Kustaajabisha wa Fedha Zikusanywazo kwa Njia ya Wasia

Yaani, mimi sijali kwamba kutokana na Wasia fedha zote hizi zitatoka wapi, bali mimi nina wasiwasi huu kwamba isije watu baada ya kuona wingi wa mali wakateleza. Yaani, nyinyi mnasema kwamba mtafanyaje mpango kwa ajili ya maskini wa dunia nzima na fedha hizo zitatoka wapi zitakazotimiza mahitaji yao? Lakini mimi sina wasiwasi wowote kwamba fedha hizi zitatoka wapi. Mali hizi zitakuja na lazima zitakuja. Wasiwasi wangu ni huu tu kwamba isije baada ya kuziona mali nyingi, macho ya dunia yakabumbuaza, na wale

waliokabidhiwa mali hizi wasije wakaanza kuipenda dunia na kutozitumia, kwa uroho, fedha hizo katika mifuko iliyokusudiwa.

Basi, Hadhrat Masihi Mau'udi[as] mwenyewe ameleta swali hili na kulijibu mwenyewe kwamba watu wasifikirie kwamba hazina kiasi hiki zitatoka wapi. zitakuja na lazima zitakuja. Kama ninayo hofu yoyote, basi ni hii tu kwamba watu baada ya kuona wingi wa mali wasije wakaanza kuipenda dunia, kwa sababu fedha zitakusanywa mabilioni kwa mabilioni hata kwamba Amerika itakuwa hajaona kiasi hicho wala Urusi wala Uingereza. Wala Ujerumani, Italia na Japani hazitakuwa zimewahi kuona mali kiasi hicho. Bali huenda hata serikali zote zikijumuika pamoja zitakuwa hazijawahi kukusanya fedha nyingi zitakazokusanywa kwa njia ya Wasia. Hivyo, kwa kuwa fedha nyingi zitakusanywa kwa njia hii ambazo kiasi hiki hapo kabla dunia haijawahi asilani kuona, kwa hiyo mimi nina hofu kwamba isije ukosefu wa uaminifu ukazalika ndani ya mioyo ya watu. Basi, msiwe na wasiwasi kwamba Nidhamu hii itaimarika vipi. Ninyi mfikirie tu kwamba ni namna gani mtaweza kuwa wenye uwezo wa kuzitumia kwa usahihi. Rasilimali za dunia lazima zitawajieni, lakini ninyi mnatakiwa mjirekebishe nafsi zenu hivi kwamba mali hizo, kwa mikono yenu, zitumike kwa usahihi kwa ajili ya manufaa ya dunia.

## Nidhamu Mpya Iliyoelezwa Ndani ya 'Wasia' Ilivyomwathiri Khawaja Kamalud Din

Wakati huu siwezi kutomsifu adui fulani. Siku ile Hadhrat Masihi Mau'udi[as] alipoandika Wasia na kuutuma nje mswada wake, Khwaja Kamalud Din akaanza kuusoma. Alipoendelea kuusoma na kufikia sehemu hii akafurahi sana kupita kiasi. Mtazamo wake uliuona kwa kiasi fulani uzuri wa Wasia. Aliendlea kusoma mswada huku akipiga mkono wake mapajani mwake akasema, "Hario! Ewe Mirza, hakika umeiimarisha mizizi ya Uahmadiyya. Bila shaka mtazamo wa Bwana Khawaja uliuona uzuri wake kwa kiasi fulani tu, lakini hata hivyo hakuufahamu kikamilifu. Kwa hakika, kama kitabu cha Wasia kisomwe kwa umakini, basi itabidi isemwe, 'Hario! Ewe Mirza, hakika umeiimarisha mizizi ya Islam. Hario! Ewe Mirza, hakika umeiimarisha kwa kudumu mizizi ya ubinadamu.

اَللّٰهُمَّ صَلِّ عَلٰى مُحَمَّدٍ وَعَلٰى آلِ مُحَمَّدٍ وَعَلٰى عَبْدِكَ الْمَسِيْحِ الْمَوْعُوْدِ وَبَارِكْ وَسَلِّمْ اِنَّكَ حَمِيْدٌ مَّجِيْدٌ

## Taswira Ndogo ya Nidhamu Mpya kwa Sura ya Tahrike Jadid

Kama nilivyoishasema, kazi hii yahitaji muda na inaihitaji siku ile ambapo Waahmadiyya watakuwa wengi duniani kote. Hivi sasa mapato yaliyopo hayawezi hata kuyatekeleza barabara mahitaji ya Makao Makuu. Ndio sababu Mwenyezi Mungu

Amenitilia moyoni mwangu kuanzisha Tahrike Jadid, ili kwa njia hii, kuanzia sasa uanzishwe Mfuko Mkuu na zizalishwe rasilimali ya Makao Makuu ambayo kwayo mahubiri ya Uahmadiyya yapanuliwe.

Basi, Tahrike Jadid ni nini? Ni zawadi ya upendo ya kuiwasilisha mbele ya Mwenyezi Mungu kwamba ile nidhamu Unayotaka kuistawisha duniani kwa njia ya Wasia, kwa sasa bado iko mbali, kwa hiyo tunatoa Kwako, kwa njia ya Tahrike Jadid, taswira ndogo ya nidhamu hiyo hadi wakati ule nidhamu ya Wasia itakapokuwa na nguvu, ili kwa njia hii, raslimali zile za Makao Makuu zitakazozalika zipanue mahubiri ya Uahmadiyya na kutokana na mahubiri Mpango wa 'Wasia' uenezwe.

## Njia ya Kusogeza Karibu Sana Nidhamu Mpya

Hivyo, kadiri mahubiri yatakavyoendelea na watu kuwa Waahmadiyya, nidhamu ya Wasia itaendelea kupanuka zaidi na mali nyingi zitaanza kukusanyika. Ni kawaida kwamba treni iondakapo huenda taratibu, lakini baadaye huongeza sana kasi. Kadhalika hata tuanzapo kukimbia, kunakuwa na tofauti kubwa kati ya kasi ya mwanzo na ya baadaye. Hivyo, mali inayokusanywa sasa kwa njia ya Wasia bila shaka kasi yake sio kubwa, lakini Uahmadiyya utakapoenea kwa wingi na watu watakapoanza kujiunga ndani ya silsila yetu makundi kwa makundi, wakati huo mali zitaanza hasa kukusanyika na kitabia lundo la

rasilimali litaanza kulivuta lundo lingine la mali. Na kadiri Wasia utakavyozidi kupanuka, basi Inshaallah, siku za Nidhamu Mpya zitakuwa zinaendelea kukaribia.

## Tahrike Jadid ni Kitangulizi cha Nidhamu Mpya

Ilmuradi, ingawa Tahrike Jadid imekuja baada ya Wasia, lakini imekuwa ni kitangulizi kwa ajili yake. Kana kwamba nidhamu hii ni kama Eliya kwa Masihi wake, na kudhihiri kwake kumekuwa ni kitangulizi kwa kudhihiri kwa ushindi wa Hadhrat Masihi Mau'udi[as]. Kila mtu anayejiunga ndani ya Tahrike Jadid anasaidia kuipanua nidhamu ya Wasia, na kila mtu anayeipanua nidhamu ya Wasia, yeye anasaidia kuijenga Nidhamu Mpya.

Kimuhtasari, kama nilivyosema, Wasia umezizingira nidhamu nzima iliyostawishwa na Islam. Baadhi ya watu wanadhani kwa makosa kwamba mali ya Wasia ni kwa ajili tu ya kuueneza Uislamu kimatamshi, lakini jambo hili si sahihi. Wasia ni kwa yote mawili, uenezaji wa kimaneno na pia uenejazi wa kimatendo. Kama vile Tabligh ilivyojumuika humo, ndivyo hivyo ulivyojumuika pia ukamilishaji wa Nidhamu Mpya ambayo chini yake kila mtu atapata riziki ya stara. Nidhamu ya Wasia itakapokamilika, basi haitaitekeleza tu Tabligh, bali chini ya utashi wa Islam, itatimiza mahitaji ya kila mtu na shida na dhiki zitafutwa duniani. Inshaallah yatima hataombaomba, mjane hatahangaika

akiwaomba watu, asiye na chochote hatatataharuki, kwa sababu Wasia utakuwa ni mama wa watoto, baba wa vijana, mwangalizi wa wanawake, na bila ya kushurutishwa, kwa huba na upendo wa moyo, ndugu atamsaidia nduguye kwa kupitia Wasia. Na kutoa kwake hakutakosa malipo, bali kila atoaye atapata malipo bora kutoka kwa Allah. Si tajiri atakayepata hasara wala masikini. Wala kaumu haitapigana na kaumu nyingine. Bali hisani yake itaenea dunia nzima.

Hivyo enyi marafiki! Si Bwana Churchil[36] awezaye kuitengeneza nidhamu mpya ya dunia wala Bwana Roosevelt.[37] Madai haya ya Atlantic Charter yote ni ulaghai. Ndani yake mna kasoro nyingi, aibu nyingi na mapungufu mengi. Nidhamu Mpya huleta tu wale waliotumwa duniani na Mwenyezi Mungu, ambao mioyoni mwao hamna uadui wowote dhidi ya matajiri wala hawana upendo wa maskini pale pasipostahili. Huwa sio wa kimashariki wala wa kimagharibi. Wao huwa ni wajumbe wa Mwenyezi Mungu, na hutoa mafundisho yale yaliyo njia ya kweli ya kustawisha amani. Hivyo, leo mafundisho yale tu yatastawisha amani ambayo yalikuja kwa njia ya Hadhrat Masihi Mau'udi[as] na ambayo msingi wake uliwekwa mnamo mwaka 1905 kwa njia ya 'Wasia'.

## Nasaha kwa Wanajumuiya wote

Hivyo, marafiki wote wanapaswa waufahamu umuhimu wake na kuzikumbuka vema dalili zile nilizozitoa kwa

sababu karibu kila sehemu hupatikana watu ambao huusifu Ubolsheviki. Kwa hiyo, nilizitaja pia sifa njema za mfumo wa Ubolsheveki na nikataja pia kasoro zake. Kadhalika nilizitaja sifa njema na pia kasoro za mifumo mingine. Kwa hiyo, zitafakarini na jadilini na wenye elimu kwa kuzizingatia dalili hizo. Mimi ninakuhakikishieni kwamba hizi ni dalili ambazo wanaoihami mifumo hiyo hawana hoja kabisa dhidi yake. Kama amani inaweza kustawi duniani, basi ni katika njia hii hii niliyoieleza leo. Halikadhalika miaka 18 kabla ya leo, mnamo mwaka 1924, kuhusiana na kustawisha amani, Mwenyezi Mungu, kwa njia yangu, Alifichua habari kubwa kabisa ndani ya kitabu cha 'Ahmadiyyat',[38] ambayo ninaweza kusema kwa yakini kabisa kwamba katika kipindi cha karne kumi na tatu zilizopita, hakuna mfasiri yeyote aliyewahi kuifichua. Na kwa yakini hayo ni mafundiho ambayo, ingawa kutoa madai kama haya ni kinyume na tabia yangu, lakini ninaweza kusema kwa yakini kabisa kwamba kufichua mambo kama hayo hadi sasa hajafanya yeyote minghairi ya manabii na makhalfa wao. Kama yeyote amewahi kufanya hivyo, basi nileteeni mfano wake.

## Mwenye Kufanya Wasia Anakuwa na Hisa Katika Uwekaji Msingi wa Nidhamu Mpya

Hivyo, Enyi marafiki ambao mmefanya Wasia! Fahamuni kwamba yeyote miongoni mwenu aliyefanya

wasia, huyo ameweka msingi wa Nidhamu Mpya, ile Nidhamu Mpya ambayo ni jiwe la msini la kumhifadhi yeye na familia yake. Na yule aliyeshiriki ndani ya Tahrike Jadidi, na pia yule ambaye hakuweza kushirki katika Tahrike Jadid kutokana na unyonge wake lakini anadumu kuuombea mafanikio mfumo huu, yeye ameweka msingi wa kuipanua nidhamu ya Wasia. Hivyo, Enyi marafiki! Nidhamu mpya ya dunia inaundwa kwa kuifutilia mbali dini. Nyinyi mkiistawisha dini tayarisheni nidhamu nyingine iliyo bora ya hiyo kwa njia ya Tahrike Jadid na Wasia. Lakini fanyeni haraka, kwani yule atanguliaye kwenye mashindano ya mbio ndiye huyo huyo anayeshinda.

## Haja ya Kuharakisha Kufanya Wasia

Basi, harakisheni kufanya wasia ili ujenzi wa Nidhamu Mpya ufanyike haraka, na ije siku ile yenye baraka ambapo kila mahali ipepee bendera ya Islam na Uahmadiyya. Pamoja na haya ninawapongeza marafiki wote waliopata fursa ya kufanya Wasia, nami ninamwomba Mwenyezi Mungu kwamba Awape uwezo wale watu ambao hadi sasa bado hawajajiunga ndani ya nidhamu hii, kwamba wao pia wajumuike, na waweze kupata neema na baraka tele za dini na dunia, na dunia ifaidike na Nidhamu hii kwa namna hii kwamba hatimaye ilazimike kukiri kwamba kijiji cha Qadian ambacho kilikuwa kinaitwa kuwa ni kijii kilicho nyuma

kabisa kimaendeleo, ambacho kiliitwa kuwa ni kijiji cha ujahili, humo ilitoka nuru iliyoliondoa giza la dunia nzima, iliyouondoa ujahili wa dunia nzima, iliyoziondoa shida na machungu yote duniani, iliyompa kila tajiri na maskini, kila mdogo na mkubwa uwezo wa kuishi kwa mapenzi, huba na upendo.

---

[1] Carl Marx: Mwanafalsafa wa Kijerumani na mwanzilishi wa Ukomonisti. Alizaliwa mwaka 1818 na akafariki mwaka 1883.

Traves alikuwa mwana wa mwanasheria Myahudi. Alisoma katika mji wa Bonn na Barlini. Mnamo mwaka 1844 alianza kufanya kazi pamoja na Engels na akishirikiana naye akaandika kitabu kiitwacho The Holy Family, na kuipa nguvu falsafa yake kisha akaiunda ilani ya kikomunisti.

(Urdu Ensaiklopidia Jalada, la 2, uk. 1377, chapa ya mwaka 1988, Lahore)

[2] Lenin-Vladimir Llyich (22 Aprili 1870 — 21 Januari 1924), mwanasiasa wa Kirusi. Mnamo mwaka 1887 baada ya kumaliza masomo ya awali alipata nafasi ya kusoma somo la sheria katika chuo cha Kazaan, lakini muda si muda kutokana na kushiriki kwake katika harakati za wanafunzi zilizolenga mapinduzi, akakamatwa, na mwaka 1888 akaachiliwa huru. Mwaka 1897 akafukuzwa nchini. Katika muda huo akamaliza kitabu chake kiitwacho 'The development of Capitalism

in Russia'. Mwaka 1914 akahamia Uswisi. Mwaka 1917 utawala uliokwepo nchini Urusi ukashindwa, na 7 Novemba 1917 chini ya uraisi wa Lenin utawala mpya wa Kirusi ukatangazwa.

(Urdu Ensaiklopidia, Jalada la pili, kurasa 1362-1363, chapa ya mwaka 1988, Lahore)

[3] Ludendroff Erich (1865-1937), Jenerali Mjerumani. Katika Vita Kuu ya Kwanza chini ya Hindenburg, akiwa kiongozi mkuu, aliweza kupata ushindi mkubwa ulionasibishwa kwa mtu mwingine. Katika mji wa Munich mnamo mwaka 1923 akishirikiana na mke wake wa pili akaweka msingi wa itikadi ya Kiaria.

(Urdu Ensaiklopidia, Jalada la 2, Uk. 1334, chapa ya mwaka 1988, Lahore)

[4] Stalin: Dikteta wa Kirusi wa kikomonisti, ambaye jina lake hasa lilikuwa Loseb Dzhugashvili. Baada ya kushiriki katika harakati za kimapinduzi aliamua aitwe jina Stalin (pande la mtu). Akajifunza upadre, lakini akashika mwelekeo wa Kimaksi na kwa sababu hii akafukuzwa chuoni. Mnamo mwaka 1945 akamwondoa Moltof madarakani na kushika cheo cha Waziri Mkuu na pale Hitler alipoishambulia Urusi, akashika uongozi wa kijeshi. (Urdu Ensaiklopidia, Jalada I, Uk. 739 chapa ya mwaka 1987, Lahore)

[5] Molotov Mikhailovich (1890-1986), mwanasiasa wa Kirusi. Mnamo mwaka 1906 alishiriki katika chama cha

Bolsheviki. Kuanzia mwaka 1930 hadi mwaka 1941 akabaki kuwa mjumbe wa Bunge la Kirusi. Kuanzia mwaka wa 1946 hadi 1949 alikuwa waziri wa mambo ya nje wa Urusi, na kutoka mwaka 1953 hadi 1957 akawa Waziri Mkuu wa Urusi. Katika mwaka 1956 hadi 1957 kwa muda mfupi akafanya kazi kama waziri wa serikali. (Urdu Ensaiklopidia, Jalada la 2, uk. 1646, chapa ya mwaka 1988, Lahore)

[6] Sura Al-An'aam, 6:12

[7] Kumbukumbu la Torati (23:19) Mambo ya Walawi (25:35-37)

[8] Kumbukumbu la Torati(15:12)

[9] Kumbukumbu la Torati(15:12)

[10] Kumbukumbu la Torati 20: 10-17

[11] Wagalatia (3:10-13)

[12] Maru Smurti (10:121)

[13] Manu Smurti (9:151)

[14] Manu Smurti (8:417)

[15] Manu Smurti (8:117)

[16] Sura Al-Anfaal 8:68

[17] Sura Al-Hajj 22:40-42

[18] Sura Muhammad, 47:5

[19] Muslim Kitabul imaan mlango suhbatul mamaaliik

[20] Muslim Kitabul imaan mlango suhbatul mamaaliik

[21] Sura An-Nuur, 24:33

[22] Sura An-Nuur, 24:34

[23] Axis Powers katika Vita Kuu ya Pili muungano wa chama cha Nazi cha Ujerumani na chama cha Fashisti cha Italia.

[24] Sura Al-Baqara, 2:30

[25] Sura Al-Hijr, 15:89

[26] Sura Al-Hujuraat, 49:10

[27] Ahmadiyyat yaani Hakiki Islam, uk. 231, chapa ya mwaka 1977

[28] Ahmadiyyat yaani Hakiki Islam, uk. 232-233 chapa ya mwaka 1977

[29]Sura Al-Baqara, 2:4

[30] Hitler Adolf (1889-1945), dikteta wa Ujerumani. Mwanzilishi wa chama cha Nazi. Baada ya Vita Kuu ya Kwanza yeye akishirikiana na baadhi ya wanaharakati aliweka msingi wa chama cha Nazi katika mji wa Munich. Mwaka 1933 akachukua mamlaka kamili ya udikteta na akawa mkuu wa idara zote za Ujerumani na akawamaliza maadui wote wa chama cha Nazi.

Mwishowe sera zake zikasababisha itokee Vita Kuu ya Pili.

Mwaka 1941 Hitler akaongoza mwenyewe wanajeshi wake dhidi ya Urusi.

(Urdu Ensaiklopidia, Jalada la 2, uk. 1846, chapa ya mwaka 1988, Lahore)

[31] Goering: (1893-1946), Kiongozi wa chama cha Nazi cha Ujerumani. Katika Vita Kuu ya Kwanza alikuwa afisa hodari wa jeshi la anga. Katika siku za awali akaungana na Wanazi. Mnamo mwaka 1933 akateuliwa kuwa waziri wa idara ya anga na Waziri Mkuu wa Prussia. Yeye ndiye aliyeweka msingi wa idara ya Ujasusi na Upelelezi naye akabaki kuwa mkuu wa idara hiyo hadi mwaka 1936. Yeye akaongoza nidhamu ya kiuchumi ya Ujerumani kwa kutumia mamlaka ya udikteta. Hitler akamfanya kuwa mrithi wake. Katika Vita Kuu ya Pili akasimamia vita ya angani. Mnamo mwaka 1945 akasarenda kwa wanajeshi wa Kimarekani. Kutokana na uhalifu wake katika vita akahukumiwa kupewa adhabu ya kifo, lakini kabla ya kunyongwa akajiua.

(Urdu Ensaiklopidia, Jalada la 2, uk. 1294 chapa ya mwaka 1988, Lahore)

[32] Bonaparte: Jina la kiukoo la Napoleon wa kwanza. Pamoja na majina ya watu wengi maarufu wa ukoo wa Napoleon limeandikwa neno la 'Bonaparte', kana

kwamba hilo lilikuwa ni jina la heshima la ukoo wa Napoleon.

(Urdu Ensaiklopidia, Jalada I, uk. 272, chapa ya mwaka 1987, Lahore)

[33] Al-Baqara, 2:196

[34] Mussolni-Benito (1883-1945): Dikteta wa Italia. Alikuwa mwana wa mhunzi. Mwanzoni alifanya kazi akiwa mwalimu na mwandishi wa habari. Akachangia mchango wake mkubwa katika harakati za Ujamaa. Katika Vita Kuu ya Kwanza akaingilia kati mambo ya vita, na kutokana na shughuli zake hizi akafukuzwa katika Mwendeleo wa Ujamaa. Mnamo mwaka 1919 akaunda chama chake. Mnamo mwaka 1922 akateuliwa na mfalme wa Italia na Jeshi kuwa Waziri Mkuu. Mwaka 1925 akachukua mamlaka ya kuwa dikteta. Mnamo mwaka 1926 akatangaza vyama vyote vya upinzani kuwa vyama visivyo halali. Mnamo mwaka 1935 akateka Uhabeshi. Mnamo mwaka 1939 akaiteka Albania na kutokana na sera zake hizi akawa karibu na Wanazi. Mnamo Juni 1940 akashiriki katika Vita Kuu ya Pili. Washirika wa vita wakaishambulia Sisli na kuiteka na kutokana na shambulizi lao heshima yake ilipungua. Mnamo Julai 1943 Baraza Kuu la chama cha Fashisti likamlazimisha kujiuzulu, kisha akakamatwa. Mnamo Septemba 15, 1943 ndege za Ujerumani zikamwachisha huru na kumpeleka Ujerumani, lakini kwa mara ya tena

yeye akaunda serikali ya kidemokarasia ya kifashisti kaskazini mwa Italia. Aprili 1945, akakamatwa pamoja na hawara wake, na wote wakapigwa risasi. Maiti yake ikapelekwa Mailaan ambapo ikaburutwa barabarani. (Urdu Ensaiklopidia, jalada 2, uk. 1565, chapa ya mwaka 1988, Lahore)

[35] Kitabu cha Wasia, uk. 24

[36] Sir Winston-Leonard-Spencer, Churchill (30 Novemba 1874 — 24 Januari 1965): Mwanasiasa Mwingereza, askari, mwandishi. Alishiriki katika mapigano ya India, Sudani na Afrika kusini. Mnamo mwaka 1900 akawa mbunge. Kuanzia mwaka 1940 hadi mwaka 1945 akawa Waziri Mkuu. Akaandika vitabu vingi. Mnamo mwaka 1953 akapata tuzo ya Nobeli katika fasihi.

(Urdu Ensaiklopidia, Jalada I, uk. 514, chapa ya mwaka 1987, Lahore)

[37] Theodorer Roosevelt (1858-1919): Gavana wa New York, Makamu wa Rais wa Marekani wa mwaka 1901. Mnamo mwaka 1901 hadi mwaka 1909, baada ya kifo cha Rais Makenli, akawa Rais wa Marekani. Akaandika vitabu juu ya historia, wanyama wa porini na siasa. Mnamo mwaka 1906, akapata tuzo ya Nobeli ya amani. (Urdu Ensaiklopidia, Jalada I, uk. 679, chapa ya mwaka 1987, Lahore)

---

[38] Ahmadiyyat: Muradi wake ni kitabu cha Hadhrat Muslih Mau'udi[ra] kiitwacho "Ahmadiyyat yaani Hakiki Islam." Kitabu hiki kiliandikwa na Hadhrat Muslih Mau'udi[ra] kwa ajili ya mkutano wa Wembley. Chaudhry Sir Muhammad Zafurullah Khan alitoa kimuhtasari yaliyomo humo katika mkutano wa Wembley katika uwepo wa Hadhrat Muslih Mau'ud[ra].